

BUNGE LA TANZANIA

---

MAJADILIANO YA BUNGE

---

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Nne - Tarehe 6 Desemba, 2013

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mtakuwa mmesikia taarifa ya msiba wa Kiongozi wetu wa Bara la Afrika na Kiongozi wa Nchi ya Afrika ya Kusini, ambaye ametutoka Duniani usiku wa kuamkia leo. Kwa heshima yake pamoja na kwamba nitaagiza Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa niaba yetu waandaye *resolution* tutaisoma kesho.

Lakini kwa ajili ya leo ili tuweze kuanza kazi yetu vizuri naomba tusimame kwa dakika moja ili tumkumbuke kiongozi huyu. Mwenyezi Mungu aipumzishe Roho yake Peponi.

*(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja Kuombeleza Kifo cha Mzee Nelson Mandela)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**SPIKA:** Kamati ya Hesabu za Serikali watawasilisha kesho kwa kuwa hawakuarifiwa jana usiku wakati tulipokuwa tumeshatayarisha *Order Paper*.

**MHE. SELEMANI JUMANNE ZEDI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA):**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Kamati hiyo kwa Mwaka 2013.

**MHE. ANDREW J. CHENG - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Kamati hiyo kwa Mwaka 2013.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 40

**Vigezo vya Mji kuwa Makao Makuu ya Nchi**

**MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS** aliuliza:-

Nchi nyingi Duniani zina Makao Makuu ya Serikali katika miji mbalimbali:-

Je, nini vigezo gani vitatumika kufanya Mji uwe na hadhi ya Makao Makuu ya Serikali?

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi nyingi Duniani ziliamua kuweka Makao Makuu ya Serikali katika Miji mbalimbali kwa kuitamka katika Katiba, Sheria au vinginevyo kwa kufuatia mazingira yafuatayo:-

(a) Kuwa kitovu cha uchumi na biashara katika Nchi husika kama vile Bahdad ya Zamani, Berlin, London, Constatinople, Athaens, Madrid, Moscow, Rome, Stockholm, Tokyo na Vienna;

(b) Kuongoza katika nyanja za utamaduni, kiutawala, au kuwa mbele katika masuala ya Kitaaluma. fano Athens, Belgrade, Brussels, Cairo, London, Manila, Lisbon, Sofia na Vienna;

(c) Uwamuzi wa Serikali kuweka Makao Makuu yake katika mji inaoona unafaa zaidi kwa madhumuni hayo kwa mfano Dodoma - Tanzania Canberra -Australia, Ottawa – Canada, Abuja – Nigeria, Wellington- New Zealand, Washington DC - Marekani, Brasilia – Brazil na Islamabad- Pakistan; na

(d) Kuwa vituo maalum vyta dini mfano Rome, Jerusalem, Baghdad ya Zamani, Moscow, Belgrade na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kuufanya mji uwe na hadhi ya Makao Makuu ya Serikali ni pamoja na kuwepo kwa:-

(i) Majengo ya kutosha kwa ajili ya ofisi za Serikali na Makazi ya watu;

(ii) Huduma muhimu za kijamii za kutosha kama vile Shule, Vyuo na kadhalika;

(iii) Huduma za maji ya kutosha;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, SERA, URATIBU NA BUNGE]*

- (iv) Mtandao wa uhakika wa kufikika kwa njia ya barabara, reli, uwanja wa ndege na kadhalika;
- (v) Huduma mbalimbali za kibiashara;
- (vi) Huduma ya umeme ya uhakika;
- (vii) Mazingira mazuri ya hali ya hewa nzuri; na
- (viii) Maamuzi yanayoambatana na hali halisi ya Nchi.

**MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, juzi siku ya Jumatano Mheshimiwa Waziri huyu huyu aliojibu sasahivi hapa akijibu swalii la Dkt. Malole Mbunge wa Dodoma Mjini alisema kwamba Serikali inatarajia kutunga Sheria itakayofanya Mji wa Dodoma uwe Makao Makuu ya Serikali.

Serikali inatarajia kwa maana hiyo kwamba Serikali imetanganza Mji wa Dodoma ni Makao Makuu wameufanya bila ya Sheria kuwepo, na hapa majibu yake ya leo anasema kwamba Mji Mkuu hutangazwa na Sheria ya Serikali ambayo ni Makao Makuu. Je ni kwanini Serikali imeanza kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu kabla ya Sheria na Kuleta Mkanganyiko katika Nchi?

Mheshimiwa Spika, vigezo alivyovitaja Mheshimiwa Waziri katika majibu yake hapa kwamba Majengo ya kutosha kwa ajili ya ofisi ya Serikali na mengineyo hayapo Dodoma. Ya kufanya mji wa Dodoma uwe na hadhi yaku Makao Makuu ya Serikali inakuwaje Serikali ipange Dodoma kuwa Mji Mkuu wa Serikali bila kuwa na huduma hizi muhimu ambazo ni vigezo viliviyoweka na Serikali hiyo hiyo hatuoni hapa nikuyumbisha nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba uamuzi ya kuja Dodoma ulifanywa bila utaratibu nimesema tunatunga Sheria, lakini Mji huu ulikuja Kisheria vilevile kwasababu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, SERA, URATIBU NA BUNGE]*

pamoja na mazungumzo mengi tangu mwaka 1961 uhuru ulipopatikana mazungumzo yalianza na katika miaka hiyo hiyo ya 1961 mazungumzo yalianza ndani ya Nchi na kupendekeza Mji wa Makao Makuu uhame Dar es Salaam, wakati ule ilipendekezwa iwe katika miji ya Dodoma, Iringa , Arusha na Tabora.

Lakini Bunge hili katika kikao chake cha mwezi Februari,1966, kwa Muswada Binafsi ya Mbunge wa Musoma, Mheshimiwa Joseph Nyerere. Alileta Muswada Binafsi hapa na Bunge likaunga mkono kwamba Makao Makuu sasa yahame kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma.

Baada ya hapo na mfumo uliokuwepo vikao mbalimbali vyatya chama na Serikali viliendelea vikaazimia lakini hiyo haikutosha Serikali ilitayarisha *General Notice* Namba 230 ambayo ilitangazwa tarehe 12 Oktoba, 1973 ambayo ndiyo ilianzisha na ku-establish Dodoma kuwa Makao Makuu.

Kwa hiyo labda tu tofauti Mheshimiwa Mbunge hajui kati ya hii *General Notice* inaweza kufanya kazi kama Sheria na Sheria, lakini Dodoma ipo Kisheria na sababu ni nyingi sana wale watu wa zamani kama sisi tunajua tumeshiriki wote katika kufanya maamuzi ya Dodoma kuwa Makao Makuu.

Lakini la pili, Mheshimiwa Mbunge kinachoanza kwanza ni wazo na uwamuzi, hamwezi kuwanza kujenga kutenga Bajeti na nchi hizo mkaanza kujenga, kutenga Bajeji kukusanya mapesa kujenga majengo kabla hamjafanya uwamuzi. Kwa hiyo, sisi tumeanza kwa utaratibu tumeanza kufanya uwamuzi kwamba Makao Makuu yetu ni Dodoma, halafu ndiyo tunaanza maandalizi.

Sehemu zote wanafanya hivyo kwanza unaanza uwamuzi maana kwanza hamuwezi kufanya kujenga, kujenga *infrastructure* majengo bila kufanya uwamuzi wa makusudi kwamba tunajenga kwa ajili ya nini. Kwa hiyo sisi tunakwenda vizuri tumefanya uwamuzi inachukua muda mrefu hatukusema lazima iwe leo lakini baadaye tutakuja kukaa wote. (*Makofii*)

### **Upungufu wa Watendaji wa Vijiji Nchini**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI (K.n.y. MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA) aliuliza:-**

Maeneo mengi ya vijiji nchini yamekuwa na upungufu mkubwa wa watendaji wa vijiji hali inayochelewesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

(a) Je, ni Vijiji vingapi vya Jimbo la Mchinga havina Watendaji wa Vijiji?

(b) Je, ni kwa kiwango gani ukosefu wa watendaji hao umechangia kuzorotesha Maendeleo ya Wananchi?

(c) Je, ni lini Watendaji wa Vijiji wataajiriwa na kupangwa kwenye vijiji husika?

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mchinga lina vijiji 46 katika ya vijiji hivyo vijiji 37 vina Watendaji wa vijiji na 9 havina Watendaji wa vijiji wakauajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi. Vijiji ambavyo havina Watendaji nafasi hizo zinakaimiwa na Watendaji ambao hupangiwa kukaimu nafasi hizo na Mkurugenzi wa Halmashauri ili shughuli za maendeleo ziweze kuendelea katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, inapotokea kijiji hakina kabisa mtedaji ni dhahiri kuwa shughuli za maendeleo zitazorota kutokana na pengo hilo. Aidha, kama nilivyoeleza katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA]*  
sehemu (a) hapo juu Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwakaimisha Watendaji wa vijiji jirani kufanya kazi katika vijiji ambavyo havina watendaji ili kuziba pengo wakati jitihada za Serikali zinafanyika kupata Watendaji wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali Kuu ilirejesha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa nafasi 10 za Watumishi wenye kada za chini ili watumishi hao wakiwemo Maafisa Watendaji wa Vijiji wajiriwe na Halmashauri wenyewe baada ya kupata kibali cha kuajiri kutoka Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi wa Umma.

Katika mwaka 2012/2013 Halmashauri iliomba kibali cha kuajiri Watendaji wa vijiji 10 na mwaka 2013/2014 Halmashauri iliomba kuajiri watendaji watatu (3) kuitia barua yenyе Kumbukumbu Namba *LDW/W.20/21/20* ya tarehe 3 Desemba, 2012. Tunaomba rai Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira wakati kibali cha kuajiri na mamlaka husika kitakapotolewa.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na hayo nina maswali mawili ya kuuliza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kumekuwa na utataka mkubwa wa kuajili watendaji kwa sababu ya vigezo vinavyotumika kwamba vijijini huwezi kumpata mtendaji ambaye amesoma sana hivi ndiyo maana tukakosa kuajili au kuwapata Watendaji.

Kwa hiyo swali langu ni kwamba je, Serikali itaangalia upya vigezo vyta kuajiri watendaji wa vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali itatupatia nafasi zilizobaki ambazo hazijajazwa katika Jimbo la Mchingga? Kwa sababu Uchaguzi Mkuu unakuja, Katiba mpya inataka ifanyiwe kazi, kama hakuna utendaji vijijini kwa kweli kazi haifanyiki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi nchi yetu ina vijana wengi sana ambao wamesoma katika *level* ya *Certificate na level ya Diploma*. Kwa hiyo, hatuna uhaba wa watu wenye sifa katika sehemu mbalimbali. Watendaji wa vijiji lazima tuchukue wenye *Certificate* na kwa Watendaji wa Kata lazima tuchukue wenye *Diploma*.

Tukumbuke kwamba watendaji hawa ndiyo wanasi mamia Miradi ya Maendeleo kama hawana sifa husika hawataweza kuelewa jinsi ya kuongoza *Word District Council* na jinsi ya kuongozi wananchi katika vijiji husika kuhusu vibali vya Lindi kama nilivyosema kwamba tutatoa vibali hivyo na kama mnavyofahamu wenyewe mlipitisha *Miscellaneous Amendment* ambayo imeshasainiwa na Mheshimiwa Rais kuhusu nafasi za chini kuajiliwa katika level ya Halmashauri na katika level ya Taasisi mbalimbali.

Kwa hiyo sisi ofisi ya Rais *Management* ya Utumishi wa Umma tumeishalifanya kazi hilo na hivi karibuni labda kwenye mwezi huu wa Desemba tuta *delegate power* kwa Halmashauri ili waajiriwe watendaji wa vijiji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mikidadi kibali hicho kitatolewa baada ya utaratibu wetu kukamilika.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri je, Viongozi wa Siasa katika Halmashauri yoyote ile wanaruhusiwa kufanya kazi za utendaji kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, labda ningefahamu ni Viongozi wa Kisiasa wa aina gani ambao anawasema, kwa sababu swali lake ni *blanket statement*. Lakini kwa kifupi Viongozi wa Kisiasa na Watendaji ni vitu viwili tofauti. Kila mtu ana kazi zake ambazo zimeinishwa katika muundo wake wa utumishi. Kwa hiyo, Kiongozi wa Kisiasa haruhusiwi kufanya kazi za kiutendaji.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la vijiji na Kata kukosa Watendaji ni kubwa katika Halmashauri karibu zote Nchini, na kwavile Bunge hili kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tulishafanya marekebisho ya Sheria ili kuruhusu sasa Halmashauri ziajili wandaji wa ngazi za chini, hii tulifanya Bunge la mwezi juni.

Mpaka sasa Serikali hajiatelemsha ule uwamuzi wa Bunge kwenye Halmashauri nataka kujua kwa uhakika lini tutegemee sasa uwamuzi Bunge utafika kwenye Halmashauri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Capt. Chiligati, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama anavyosema, ni kwamba kuna Vijiji karibuni 13,000, kuna kata karibuni 4,000 na Watendaji wengi hawako katika vijiji na Kata husika. Hili kama Utumishi tumeliona, na kwa miaka ya nyuma tulikuwa tunaweka vipaumbele kwa ajili ya afya, elimu na kadhalika. Lakini kwa suala nyeti sasa hivi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutatoa nafasi nyingi sana kwa ajili ya Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata.

Ni lini tutateremsha hayo madaraka kwa watendaji, mimi niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba *GN* tutaitoa mwisho wa mwezi wa Desemba ili Halmashauri na Taasisi mbalimbali ziweze kuajiri watumishi wa kada ya chini katika taasisi husika. (*Makofii*)

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mntangi.

Na. 42

### **Huduma Kituo cha Afya Kisesa**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS BULUGU LIMBU) aliuliza:-**

Idadi ya wakazi katika Mji Mdogo wa Kisesa inaongezeka kwa kasi kubwa na kuifanya huduma zitolewazo na Kituo cha Afya Kisesa kutokishi mahitaji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipanua kituo hicho ili kiwe Hospitali kamili?

(b) Je, Serikali iko tayari kuunga mkono juhudzi za wananchi wa Kisesa na Halmashauri ya Wilaya kujenga zahanati mbili kwenye mji huo ili kupunguza msongamano kwenye Kituo cha Afya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA aliijibu:-**

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri Wilaya ya Magu kwa kushirikiana na wananchi na wadau wa maendeleo ambao ni *Japanese Counterpart and Food Security* wamejenga Wodi tatu (3) kwa gharama ya shilingi milioni 75, kila wodi ina uwezo wa kulaza wagonjwa au vitanda 22. Wodi moja (1) kati ya hizo imeshaanza kutumika na wodi mbili (2) zimekamilika, lakini hazijawekewa samani.

Aidha, mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri ya Wilaya ya Magu imetenga shilingi milioni 22 katika Bajeti yake kwa ajili ya kuweka samani na vifaa tiba katika wodi hizo mbili (2) zilizobakia. Hivyo, kukamilika kwa wodi hizi tatu kunafanya kituo hiki cha Kisesa kuwa na wodi nne (4) badala ya moja (1) iliyouwepo hapo awali.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA]

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ya Magu ilitenga jumla ya shilingi milioni 40 na mwaka 2013/2014 imetenga shilingi milioni 60 kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji mkubwa (*Major Theatre*) katika Kituo cha Afya Kisesa. Mpaka sasa hivi hilo jengo lipo kwenye hatua za mwisho (yaani upauaji, kuweka madirisha, kupiga lipu na kadhalika. Dhamira ya Serikali ni kuimarisha miundombinu na utoaji wa huduma inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Magu imeongeza idadi ya watumishi katika Zahanati ya Kisesa, na mpaka sasa wamefikia watumishi 22.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wananchi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya *Global Peace Network (GPN)* kutoka Canada na *Tanzania Home Economic Association (TAHEA)* kutoka Mkoani Mwanza tayari imejenga zahanati moja (1) katika kitongoji cha Kanyama kilichopo katika Mji Mdogo wa Kisesa. Zahanati hiyo ilianza kazi tangu tarehe 14/8/2012 na inaendelea kuwahudumia wananchi wa Kisesa. Juhudi za kujenga zahanati zaidi zitaendelea kufanyika kadiri Mahitaji na hali ya uchumi wa Taifa letu itakavyokuwa inaruhusu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mntangi, swali la nyongeza.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshikiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyotoa.

(1) Lakini kutokana na jitihada ambazo zimefanywa na Halmashauri hiyo ya Magu pamoja na wahisani wale wa *Japanese Counterpart*, pamoja na *Global Peace Network* ya Canada.

Je, ni utaratibu gani ambao sasa ufuatwe ili kuwezesha Kituo hicho cha Afya kuweza kuwa Hospitali kamili yenye hadhi ya Wilaya?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HERBERT J. MNTANGI]

(2) Kitaifa upo mkakati wa kujenga Vituo vya Afya katika kila Kata. Lakini viko Vituo vya Afya katika Bajeti iliyopita vimekwishaanza kujenga, lakini bado havijakamilika na kuma mkakati wa kujenga vituo vipyta.

(3) Je, ni maandalizi gani ya kifedha ambayo yamefanywa kuwezesha kukamilisha vituo ambavyo bado havijakamilika, na ni vituo gani vipyta ambavyo vitaweza kuanza kujengwa katika Bajeti hii inayokuja sasa?

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Waziri wa Nchi, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshikiwa Mntangi kama ifuatavyo:-

Kuhusu kukamilika kwa Hospitali ya Kisesa kutoka kwenye Kituo cha Afya mpaka kuwa Hospitali kamili. Ili Kituo cha Afya kipandishwe hadhi kuwa Hospitali, kuna vigezo mbalimbali ambavyo lazima vifikiwe, na kuna huduma za msingi lazima zifikiwe. Huduma hizo kwa mfano, lazima kuwe na *Department* ya *OPD*, kuwe na *MCH*, Stoo ya kuwekea madawa, Maabara ya Benki ya Damu, Kitengo cha *X-Ray*, Chumba cha kuwekea maiti na vigezo vingine vingi ambavyo lazima vifikiwe.

Kwa hiyo, Kituo cha Afya ili kiweze kuwa Hospitali, lazima vigezo hivi vifikiwe. Kwa hiyo, Serikali itatenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha kwamba Kituo cha Afya kinapanda hadhi kuwa Hospitali.

Kuhusu ujenzi wa Vituo vya Afya kila Kata na Zahanati katika kila kijiji. Katika mpango wa MMAM (yaani Mpango wa Afya ya Msingi), tumejiwekea malengo kwamba lazima tunakamilisha kwanza vile Vituo vya Afya ambavyo vimekwishajengwa, halafu tuanze miradi mingine mipyta.

Kwa hiyo, tunaziagiza Halmashauri kwamba fedha za MMAM zikija, badala ya kuanzisha miradi mingine, ni vyema

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMAJ]*  
wakakamilisha vile Vituo vya Afya na Zahanati ambazo zimekwishajengwa. Wakianza miradi mingine ina maana kwamba kutakuwa na Zahanati nyingi na Vituo vya Afya vingi ambavyo havijamalizika.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ningewaomba hata kwenye Halmashauri zenu msaidie kuhamkisha fedha zikija wasizitawanye katika miradi mipya, bali tumalize kwanza miradi iliyopo. Iwe miradi ya Shule, iwe miradi ya Zahanati na Vituo vya Afya; ndipo tuanze miradi mingine. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Richard Ndassa, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD MGANGA NDASSA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Spika.

Naomba Mheshimiwa Spika, uniruhusu niwapongeze sana wananchi wa Kisesa pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwa kutenga kiasi kikubwa cha pesa. Swali langu ni kwamba Muuliza swali mbali na pesa ambazo Halmashauri imetenga, alikuwa anaiomba Serikali Kuu itenye pesa. Ndiyo maana akauliza je, Serikali kuu iko tayari kuiunga mkono Halmashauri ya Wilaya ya Magu? (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa kama ifuatavyo:-

Hizo hela za MMAM zinatoka Serikali Kuu. Na fedha ni fedha, aidha ziwe za Serikali za Mitaa au za Serikali Kuu; lakini zote zinatoka Serikali Kuu. Serikali za Mitaa, *all sources* zake ni kidogo sana. Kwa hiyo, bado wanategemea Serikali kuu katika michango mingi na katika Bajeti yake karibu kwa asilimia 95%.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake katika swali la msingi, amekuwa akisisitiza kwamba hela za MMAM zinatolewa na Serikali Kuu. Lakini fedha hizo zimekuwa haziwafikii Halmashauri kwa takriban miaka mitatu (3) sasa.

Mfano, katika Halmashauri yangu ya Mji wa Babati, Zahanati ya Nako kwa miaka mitatu (3) fedha haziendi. Labda nifahamu ni kwa nini fedha hizo hazipelekwi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna ucheleweshwaji wa fedha za miradi katika miradi mbalimbali, siyo miradi ya MMAM peke yake. Kwa hiyo, zinapochelewa mara nyingi haziendi kwa wakati. Lakini kwa sasa tunajitahidi kuhakikisha kwamba fedha hizo zinafika kwa wakati. Lakini tatizo kubwa lilitoko kwenye Halmashauri ni kwamba fedha hizo zikifika, wanaangalia vipaumbele ambavyo wao wanaviona kwa Zahanati au Vituo vya Afya, wanavyoviona kwamba vina uharaka zaidi.

Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Mbunge ahahakishe hela za MMAM zikifika, wazitengee katika kituo hicho au zahanati husika. Mara nyingi wanaanza miradi mipywa badala ya kumaliza ile miradi ya zamani.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Sara Ally Msafiri, atauliza lakini kwa niaba yake Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**Migogoro ya Ardhi Kutatuliwa na Mahakama Badala ya Mabaraza ya Ardhi**

**MHE. MUNDE TAMBWE ABDALLAH (K.n.y. MHE. SARA ALLY MSAFIRI)** alilulta:-

Migogoro ya ardhi katika ngazi ya Vijiji hushughulikiwa na Mabaraza ya Vijiji ambayo ufanisi wake umeonekana kuwa hafifu sana:-

Je, kwa nini Serikali isibadilishe mfumo huo kuwa chini ya usikamizi wa Mahakama ili migogoro itatuliwe kwa ufanisi na watu wenye utaalam wa masuala ya ardhi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sara Ally Msafiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yanaundwa chini ya Sheria inayounda Mahakama za kutatua Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216, Toleo la mwaka 2002.

Aidha, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Toleo la mwaka 2002; na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114, Toleo la mwaka 2002 linatambua kuwepo kwa Mabaraza ya Kata na kuyakabidhi majukumu ya kushughulikia rufaa zinazotoka katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Halmashauri nydingi nchini zimeunda Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Hivyo, uzoefu unaonyesha kwamba kumekuwa na mafanikio ya kutosha kutokana na kuwepo kwa Mabaraza haya, kwani yanawezesha kutatuliwa kwa migogoro mingi ya ardhi na mashamba.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA]*

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yaliundwa kwa lengo la kusuluhisha migogoro ya ardhi iliyoletwa mbele yake ili kuleta mapatano kati ya wahusika kwa njia ya usuluhishi. Mabaraza ya Vijiji hayaongozwi wala kufungamana na taratibu za mfumo wa Mahakama, bali huzingatia misingi ya haki za asili (*principles of natural justice*) ili haki itendeke na ioneckanae imetendeka.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina nia ya kuyavunja Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na kuyaunganisha na mfumo wa Mahakama, kwa kuwa kufanya hivyo ni kurudisha mlundikano wa kesi ndogo ndogo Mahakamani kwa sababu ya wingi wa migogoro ya ardhi ikilinganishwa na uchache wa Mahakama, upungufu wa Mahakimu nchini na muda unaotumikia kushughulikia kesi Mahakamani.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. MUNDE TAMBWE ABDALLAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wajumbe wengi wa Mabaraza ya Ardhi Vijijini hawana elimu ya kisheria na kwa kuwa wamekuwa wakitata baadhi ya migogoro na kwa kuwa migogoro mingine imekuwa haitatuliki na kusababisha tafrani kubwa katika vijiji:-

(a) Je, Serikali imepeleka mafunzo mara mangapi katika mabaraza hayo?

(b) Na kama haijapeleka mafunzo hayo, ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha watu wale wanapata mafunzo angalau mara mbili kwa mwaka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA]

Ni kweli naomba nikubaliane naye kwamba Mabaraza ya Vijiji hayana uelewa ambao ni *formal* kisheria, lakini wana ule uelewa wa asili katika maeneo husika. Kwa hiyo, katika maeneo husika kwa kuwa wanafahamiana na wanayafahamu maeneo hayo, mara nyingi wanatenda haki. Pale inapotokea kwamba wameshindwa kabisa kutenda haki, wanaenda kwenye Mahakama ya Ardhi ambayo inashughulikia masuala hayo ya ardhi. Nia ni njema tu kwamba kule vijijini, kesi zote ndogo ndogo za mashamba zikiletwa katika Mahakama, mara nyingi inachukua muda mrefu na wananchi wetu hawawezi kuzifikia hizo Mahakama. Ndiyo maana nia njema hii ya Serikali kwamba Mabaraza haya ya Vijiji yabaki kule, yashughulikie masuala ya ardhi katika sehemu za vijiji. (*Makofii*)

Kuhusu mafunzo, nikubaliane naye kwamba kwa kweli hatujawa na mfumo rasmi wa mafunzo kwa mabaraza yote. Kwa hiyo, kuna baadhi ya mabaraza ambayo yanapata mafunzo, lakini hatujafikia hatua yanchi nzima. Kwa hiyo, baadhi ya sehemu yanafanyika, lakini baadhi ya sehemu bado hatujayafikia. Kwa hiyo, nichukue tu wazo lake zuri la kuhakikisha kwamba watu hao wanapata mafunzo na ni watu muhimu sana katika kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi ya msingi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Katika jibu la msingi, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mabaraza haya hayajengewi uwezo na kwa vile Halmashauri zetu nyingi zimeajiri Wanasheria:-

Je, Serikali iko tayari kuwatumia hawa Wanasheria walau kuwajengea uwezo hao Wajumbe wa Mabaraza? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waziri wa Nchi, majibu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mimi nakubaliana naye kabisa kwamba kule kwenye Halmashauri kuna Wanasheria ambao tukiwatumia vizuri wanaweza wakawajengea uwezo hayo Mabaraza ya Vijiji. Mimi nasema kwamba nachukua mawazo yenu, la Mheshimiwa Munde Tambwe pamoja na wazo lako, tuyafanyie kazi kama Serikali ili tuone kwamba tunawasaidiaje hao viongozi muhimu katika ngazi ya msingi. (Makof)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, kwa niaba yake Mheshimiwa Kange Lugola.

Na. 44

### **Kupeleka Maji Wilaya ya Serengeti**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA (K.n.y. MHE. DKT. KEBWE STEPHEN KEBWE) aliuliza:-**

Mradi wa maji unaojengwa Musoma Mjini utakapokamilika, maji yake yataweza kwenda kwa mtiririko umbali wa km. 50 kufikia Kijiji cha Kitaramanke ambapo ni kama km. 10 tu kufika Wilaya ya Serengeti:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji Wilaya ya Serengeti kuoka Ziwa Victoria?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutumia mradi huo ni fursa ya kupunguza gharama za kuanzisha mradi mwingine mkubwa?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Musoma MJini umesanifiwa kukidhi mahitaji ya wananchi waishio katika Manispaa ya Musoma na Kata zake 14. Eneo hili la Manispaa lina mahitaji ya lita za maji milioni 34 kwa siku. Mradi huu haukufanyiwa usanifu ili kuweza kutiririsha maji kutoka Manispaa ya Musoma hadi Kijiji cha Kitaramanke katika Wilaya ya Butiama na pia kwenda Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo na ili kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Serengeti, Serikali inaendelea na kutekeleza miradi mbalimbali ya maji pamoja na miradi ya Vijiji kuni (10) kama ifuatavyo:-

Kijiji cha Nyagasense, Kebanchabancha, Natta-Mbiso, Natta-Motukeri, Masangura, Nyamitita, Kenyana, Parknyigoti, Mbalimbali, Wagete, Rung'abure na Nyansurumuti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika katika Vijiji vya Natta-Mbiso na Natta-Motukeri. Katika vijiji vingine, ujenzi wa miundombinu ya maji unaendelea na upo katika hatua mbalimbali kuelekea kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Kitaramanke kilichopo Wilaya ya Butiama, kuna ujenzi unaoendelea hivi sasa ambao chanzo chake ni kisima. Mradi huo unaojumuisha uchimbaji kisima, ununuzi na ufungaji wa pampu, ulazaji boma kilometra 23.2, ujenzi wa tanki la lita 100,000 na vituo vya kuchotea maji 15; na utakamilika mwishoni mwa Disemba mwaka huu 2013.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Alphaxard Lugola, maswali ya nyongeza.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa, Mheshimiwa Spika, majibu ya Waziri ni majibu ya swali ambalo Mheshimiwa Kebwe hakuuliza. Mheshimiwa Kebwe ameuliza kwamba Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Wilaya ya Serengeti. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Wanaserengeti tulitarajia atuambie kama maji haya ya Musoma Mjini hayawezekani. Je, wana mpango gani kwa maji hayo hayo? Watuambie mpango walio nao. Yeye anaelezea mlolongo wa vijiji mbalimbali, visima ambavyo Mbunge anavifahamu na hakuviuliza. Kenyana na kule hakuuliza.

Sasa Mheshimiwa Waziri utakaporudi pale kwenye *podiam* tuambie wana Serengeti mna mpango gani kwa mujibu wa swali letu wa kutuletea maji ya ziwa Victoria na kama hayo hamuwezi kuna maji ya mto Mara ambayo yako karibu na Serengeti yako karibu na Tarime na Ranya mnaweza mkatatua tatizo la maji? Kwa hiyo tuambie mna tatizo gani?

(2) Kwa kuwa juzi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji aliliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia mwakanis mwezi wa 6 wana mpango wa kupeleka maji vijiji kati ya 20 - 30, sasa nataka watuambie watapeleka maji ya namna gani kwenye vijiji nchini ambavyo viko karibu na maji ya maziwa? Vijiji hapa nchini ambavyo viko karibu mito. Watapeleka maji haya ambayo tunayoyaona kwa macho au wataendelea kuchimba visima vya maji tusiyoyaona? Tunataka atuambie watapeleka maji ya namna gani? Kule Mwibara kijiji cha mbali kabisa kutoka kwenye maji tunayoyaona ni kilomita 8, tunataka atueleze.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Kwa kweli mchungaji umehutubia. Mheshimiwa Waziri nafikiri ujibu swali, kweli liliulizwa habari ya ziwa na hukujibu swali. Naomba ujibu swali Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu letu la msingi tumeeleza kwamba mradi ulioulizwa wa Musoma Mjini umesanifiwa kwa ajili ya kupeleka maji na kukidhi mahitaji ya mji wa Musoma peke yake, mradi huu haukusaniwiwa kupeleka maji kwenye kijiji cha Kataramke ambacho ndio kimeulizwa kilichoko Butiama.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hatujasanifu mradi wo wote kutoka ziwa victoria ambaeo unakwenda Serengeti, Mheshimiwa Spika nimeyapokea mapendekezo mazuri aliyoyatotoa Mheshimiwa Mbunge ya kuweza kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria na kuyapeleka katika maeneo aliyoyataja. Hata hivyo katika maeneo hayo kuna vyanzo vingine kama mto Gurumeti na mto Mara ambavyo vinaanza kufikiriwa na vyote hivi vinafikiriwa kwa pamoja. Aidha ni muhimu sana tujue kwamba miradi mikubwa ina gharama kubwa za uendeshaji na ujenzi na kama kuna mbadala wa kufanya kupata maji katika maeneo hayo vyanzo hivyo ambavyo ni rahisi zaidi vitatekelezwa na ndio maana nikaeleza juu ya kazi ambayo inafanywa ya kupeleka maji katika eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mpango ambaeo Wizara inaandaa wa Vijiji 20 mpaka 30 katika mwaka huu unaokuja unatayarishwa na kila wakati tutajaribu kutumia maji ambayo ni rahisi zaidi kuwapelekea wananchi na ambayo yana ubora unaostahiki.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo tutaangalia vyanzo vya maji vilivyoko juu ya ardhi na vile vambavyo viko chini ya ardhi hasa kwa sababu vyanzo ambavyo viko chini ya ardhi kama havina madini ya sumu ni vizuri zaidi kuliko vile vya juu kwa sababu ya ubora wa maji yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. JUMA SELEMANI NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, mradi wa maji wa Musoma Mjini unafanana sana na mradi wa maji wa Dodoma Mjini ambako leo Serikali inataka kuchukua maji kutoka katika kijiji cha Farkwa na kulazimisha vijiji viwili kuondoka pale.

1. Je, Serikali iko tayari katika michoro ya awali inaonyesha kwamba maji yale yatatoka pale kuja Dodoma moja kwa moja, lakini makao makuu ya Wilaya ya Chemba ni kilomita 43 kuanzia *Donsee*.

2. Je, Serikali iko tayari kupeleka maji yale hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Chemba, badala ya kuleta Dodoma peke yake.

**SPIKA:** Kwa hiyo, haufanani hata kidogo lakini, Mheshimiwa Waziri kwa sababu unalijua hili swali, endelea kujibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inasanifu mradi wa maji kutoka Bwawa ambalo linatarajia kujengwa eneo la Farkwa na kuleta Mjini Dodoma ili kukidhi mahitaji ya mbele ya mji wa Dodoma unavyoyogeuka kuwa mji Mkuu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maji hayo yatatoa huduma ya maji kwa miji ya Bahi, mji wa Manyoni na hata mji wa Farkwa. Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hakuna tatizo kwamba mji wa Farkwa utaachwa katika utaratibu huu.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, Wanawake wengi wamedhalilika sana, wamedhalilishwa kijinsia kwa tatizo la maji nchini na wengine hata ndoa zao zimeunjika. Serikali imekuwa ikitangaza miradi mikubwa ya maji na kuwashakikishia wananchi vijijini kuwapelekea maji.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MARTHA M. MLATA]

Je, Serikali inaweza ikaja na mpango kama ilivyo REA inavyosambaza umeme vijijini na mafanikio yake sasa yanaonekana ili kuwe na mpango unaofanana na huo kusambaza maji vijijijini ili kuondoa adha kubwa ya wanawake hasa vijijini. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna tatizo kubwa sana la maji katika maeneo yote nchini Tanzania na kwamba watu ambao wanabeba mzigo mzito wa kuyatafuta maji haya popote yalipo kwa ajili ya familia zao ni akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika Serikali inafanya kila iwezalo kuhakikisha kwamba inakabiliana na tatizo hili. Sasa tuko katika maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2014/2015 Mheshimiwa Spika Wizara yangu itapata faraja kubwa kama Bunge hili litatuongezea fedha ili kuongeza uwezo wa kutekeleza miradi mingi zaidi ya maji.

**SPIKA:** Haya tunaendelea na swalii linalofuata.

Na. 45

### **Taratibu za Kutoza Ankara za Maji**

**MHE. REBECCA MICHAEL MNGODO (K.n.y. MHE. JOSHUA SAMWEL NASSARI)** aliuliza:-

Mamlaka ya maji husajiliwa kwa mujibu wa sheria ya maji na usafi wa mazingira ya mwaka 2009 na kupata leseni kutoka *EWURA*.

(1) Je, kwa nini Mamlaka ya Maji Usa River inatoza Ankara wakati haijakamilisha taratibu za usajili kwa mujibu wa Sheria?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. REBECCA MNGODO (K.n.y. MHE. JOSHUA NASSARI)]

(2) Je, ni utaratibu gani unaotumiwa na Mamlaka ya Maji Usa River kutoza ankara za maji, ikiwatoza wengine Tshs. 3,000/= na wengine Tshs. 10,000/= kwa kiasi kile kile cha matumizi?

### **WAZIRI WA MAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma ya maji katika Mji wa Usa River ulikuwa ukisimamiwa na Jumuiya ya Watumia maji wa Usa River iliyoanzishwa mwaka 2009. Jumuiya hiyo ilikuwa ikitambulika kisheria na utozaji wa ankara ulikuwa unatambuliwa chini ya kifungu Na. 32 (e) cha Sheria ya Maji na usafi wa Mazingira Na. 12 mwaka 2009. Kwa sasa usajili wa Mamlaka kamili umekamilika na umetangazwa katika gazeti la Serikali na Mamlaka mpya inajulikana kama Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo Usa River. Bei za maji zilizopendekezwa na Bodi ya Mamlaka hiyo na zitaidhinishwa na EWURA na hizo ndio zitatumika badala ya zinazotumika sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Chombo hiki kinatoza ankara tofauti kwa wateja wake. Wateja wa Majumbani wanatozwa shilingi 3,000/= kwa mwezi na wateja wa maeneo ya biashara shilingi 10,000/= kwa mwezi. Hii inatokana na ukweli kwamba bei za maji hupangwa kutokana na gharama za uzalishaji na matumizi ya makundi tofauti katika eneo husika. Hivyo, ulipaji wa matumizi ya maji katika maeneo ya Biashara kwa kawaida huwa ni kubwa ukilinganisha na majumbani.

Kwa hiyo, sasa, hii inatokana na matumizi katika maeneo ya biashara kuwa makubwa kwa wastani kuliko yale ya majumbani. Aidha, tozo hizi za maji mjini Usa River ziko chini ukilinganisha na miji midogo iliyoko karibu kama Katesh, Magugu na Galapo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mngodo, maswali la nyongeza.

**MHE. REBECCA MICHAEL MNGODO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

1. Mamlaka ya *Usa Riverimekuwa* ikitoza ankara kabla ya usajili, kabla ya taratibu za usajili kukamilika, lakini katika majibu ya Mheshimia Waziri amesema kwamba bei zitawekwa na *EWURA* kwa sababu tayari Mamlaka imekwisha kamilisha utaratibu wake. Ningependa kujua endapo watumiaji wa maji walikuwa wametozwa viwango tofauti na vitakavyowekwa na *EWURA*. Je, itakuwaje?

2. Katika kujibu kipengele (b) Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wafanyabiashara, watu waliopo katika maeneo ya biashara hutozwa shilingi elfu 10,000/= kwa mwezi na ninajua kwamba kuna biashara kubwa na ndogo.

Je, Serikali iko tayari kupunguza kiwango hicho kwa wafanya biashara ndogo ndogo badala ya kulipa Tshs. 10,000 walipe kiwango cha chini zaidi?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Sika, katika jibu letu la msingi tumeeleza kwamba awali kabisa huduma ya maji ilikuwa inatolewa na chama ambacho kiliandikishwa kisheria na ambacho ankara zake pia zinatolewa kisheria na ankara hizo ndio zinatumika sasa. Sasa baada ya Bodi hii kuandikishwa na kutangazwa na gazeti la Serikali. *EWURA* wataangalia gharama ya uzalishaji wa maji katika eneo hilo na kupanga bei kwa ajili ya makundi hayo ambayo nimeyataja. Wakati bei hizo zitakapopatikana wananchi wataendelea kutumia bei hizo mpya badala ya bei zile za zamani.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAJI]*

Aidha, hakuna mabadiliko yoyote ambayo yanaweza kufanywa kwa sababu utozaji unaofanywa sasa ulipangwa kisheria na Jumuiya ambayo ilikuwa inatoa maji na kuandikishwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, suluhu ya kupata bei ambayo ni sahihi anayotumia mteja katika kulipia maji ni kuwafungia mita. Mheshimiwa Spika moja ya maagizo ambayo maagizo ambayo mamlaka hii imepewa ni kwamba iwafungie mita wateja wake ili kila mmoja alipe maji kutokana na matumizi anayofanya. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nina swali moja la nyongeza ambalo Waziri ameligusia. Matatizo ya bili za maji hayapo *USA River* tu bali ni Nchi nzima kama ilivyokuwa matatizo ya bili za umeme. Sasa ili kuepuka hii adha ya kukadiria nani ametumia kiasi kikubwa cha maji au nani ametumia kiasi kidogo cha maji, ni lini sasa utaratibu wa kufunga hizo mita kama ambavyo zile ambazo zimefungwa na *TANESCO* za *LUKU* ili kila mtu mwenye uwezo wa kulipa alipe kadiri anavyotumia. Ni lini sasa utaratibu huo utanza Mheshimiwa Waziri? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, kama utakubalika. (*Makofi/ Kicheko*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna matatizo ya bili za maji katika maeneo mengi nchini. Matatizo haya tunayashughulikia kwa kufunga na kubadilisha mita kadiri inavyowezekana. Mamlaka zetu hizi uwezo wake ni mdogo sana na zinajiendoesa kwa fedha zile ambazo zinazipata kwenye ankara za maji. Kwa hiyo, kadiri fedha zinapopatikana kwa ajili ya kuwekeza wataendelea kuweka mita, kupanua mtandao na kubadilisha mita ambazo zinasoma ankara ambavyo sio vizuri. Mheshimiwa Spika ahsante sana.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini tuko nyuma ya muda.

Na. 46

**Mradi wa Umeme wa Somanga Fungu.**

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO (K.n.y. MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA aliuliza:-**

Mradi wa umeme wa Somanga Fungu una lengo la kuwapatia umeme wananchi wa Wilaya za Kilwa, Rufiji na Mkuranga, kwani umeme huo umeshafika Bungu Rufiji.

Je, ni lini umeme huo utatolewa toka Bungu Kwa Uponda, Njawa, Jaribu Mpakani hadi Kilimahewa ili kuungana na Gridi ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
(K.n.y.WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali kuitia mradi kabambe wa umeme vijijiini awamu ya pili unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijiini (*REA*) kwa kushirikiana na *TANESCO*, imepanga kutekeleza miradi ya upelekaji umeme katika Wilaya ya Rufiji kwa kuhusisha Vijiji

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU (K.n.y.WAZIRI WA NISHATI  
vya Mkola, Mwaseni, Nambujo Sekondari, Chumbi A, B na C,  
Kiwanga, Muhoro, Ngalukula, Kibuga, Jaribu mpakani, Bungu,  
Mtawanya B, Nyamatanga, Ruaruke, Kikale, Mtunda na  
Muyungu. Gharama ya kufikisha umeme katika vijiji hivyo  
inakadiriwa kuwa shilingi Biliioni 9.78.

Mheshimwa Spika, mradi huu utahusisha:-

- (i) Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilomita 174.7;
- (ii) Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilomita 82;
- (iii) Ufungaji wa *transfoma 42*; na
- (iv) Kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 2059.

Kazi ya ujenzi wa mradi inatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2014 na kukamilika ndani ya miezi 24 baada ya mradi kuanza. (*Makofi*)

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimwa Spika, katika swali la msingi mwenye swali alitaka kujua hoja ya kipeleka umeme katika vijiji vya Uponda, Njawa na Kilimahewa. Lakini kwenye majibu ya Serikali Vijihi hivi havitajwi kabisa. Ningetaka kupata maelezo ya Serikali juu ya vijiji hivi ambavyo mwenyewe alivipa kipaumbele?

Miradi mingi inayotekelezwa chini ya mpango wa *REA*, *REA* wanajitahidi sana kwa kweli naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza. Wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana, lakini tuna tatizo la miradi mingi wanaowasainisha au kuingia nao mkataba na *TANESCO*. *TANESCO* hawafanyi kazi sawasawa, utaambiwa kuna tatizo la waya, utaambiwa kuna tatizo la nguzo, utaambiwa kuna tatizo la vikombe na kadhalika.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO]

Ningetaka kupata maelezo ya Serikali hivi imejipangaje kuisaidia *TANESCO* kuhakikisha kazi zinakamilika kwa wakati ili tusiathirike na kelele za wananchi na kwamba nia yetu njema kupeleka huduma ya umeme kwa wananchi iweze kukamilika kwa wakati?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Mheshimiwa Marombwa alikuwa amevitaja hivyo vijiji ili viweze kupatiwa umeme vile vile. Lakini kulingana na mpango wa *REA* Viji vili vyovisoma katika jibu la msingi ndivyo kwa sasa hivi kwa awamu hii vimo katika mpango wa utekelezaji. Na hii haimaanishi kwamba Viji vingine havitapata umeme navyo vitaingizwa katika mipango ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia matatizo ya utekelezaji, matatizo ya Utekelezaji yalikuwepo lakini Serikali imejipanga vizuri na kuititia mpango wa *Big Results Now (BRN)*. Matatizo haya yaliyokuwa yanaonekana yanarekebishwa na tutahakikisha kwamba Miradi hii itatekelezwa kwa kasi inayotakiwa.

**MHE. DAVID Z. KAFULILLA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini awali ya yote nisikitike kwamba Wizara hii ina Waziri na Naibu Mawaziri wawili lakini hapa tunamwuliza Naibu Waziri mwingine ambaye baadhi ya maswali hawezi kuyajua kwa uyakinifu. Huu ni udhaifu mkubwa sana kwa Serikali.

**SPIKA:** Wamepewa ruhusa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika Wilaya ya Kigoma kwa takribani vijiji 14 ambavyo viko kwenye mpango wa kupata umeme kuititia mradi wa *REA* Mpaka sasa ningependa kujua, Serikali imefikia hatua gani kwa sababu tenda ya mradi huu tulipewa taarifa kwamba ilifunguliwa tangu mwezi wa nne, mwaka huu, 2013. Ningependa kujua hatua inayoendelea ni hatua gani?

**SPIKA:** Hapo kwa kweli unategemea Waziri ajibu vizuri, hili ni swali jingine. Ndiyo ni swali jingine kabisa. Wala siyo suala la Kigoma. Lilikuwa ni swali jingine. Ukipenda unaweza kujibu ukipenda unaweza kuacha.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS(K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niabaya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu Swali la Mheshimiwa David Kafulila kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka nimtaarifu Mheshimiwa David Kafulila kwamba inayoulizwa ni Serikali siyo Mawaziri. Sisi sote hapa tupo kwa niaba ya serikali na tuna uwezo wa kujibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri siyo shughuli yako kujibu hayo, ni mimi.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS(K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, vijiji kumi na nne (14) kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi ni kwamba kuna *process* ambayo inatumika. Sasa hivi kuna tenda zimefunguliwa na zimeshafanyiwa *evaluation*. Wakandarasi wamesha-sign mikataba. Baada ya ku-sign mikataba watakwenda kufanya *Evironmental Impact Assessment (EIA)*. Wakishapata *EIA* Wakandarasi watakwenda site na atawaona kuanzia mwezi Januari, 2014. (*Makofii*)

**SPIKA:** Umejibu vizuri. Tunaendelea na swali linalofuata.

## **Wilaya ya Mafia Kupewa Mtambo Wa Kuzalisha Umeme**

**MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MHE. ZAYNAB M. VULLU)** aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 Wilaya ya Mafia iliahidiwa kupatiwa mtambo wa kuzaalisha umme wa *Megawatts 4*:-

### **WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni mwaka 2013 Serikali, kuititia *TANESCO*, ilikuwa imefunga Wilaya ya Mafia mitambo yenye uwezo wa kufua umeme wa *MV 2.13*. Hata hivyo, mahitaji ya umeme (*maximum demand*) ya mji wa Mafia kwa sasa ni *MW 1.3*, hivyo ina umeme wa ziada ambao ni *MW 0.88*.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilipenda kujua japokuwa umesema mahitaji kwa sasa ni *1.3 MW*. Lakini tukijua mji wa Mafia sasa hivi ni mji wa kibiashara unaondelea kutanuka.

Je, Serikali sasa inaonaje badala la kuangalia lengo dogo na sasa hivi tuko katika *Big Results Now* kuhakikisha inaweka mpango uleule uliokusudiwa kuhakikisha kwamba kwa sababu kile ni kisiwa cha mafia kiko kisiwani kuwe na mpango huu sasa kuweza kukusudia kupata *MW 8* kama alivyokusudia hapo awali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS(K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Jafo kama kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU (K.n.y.WAZIRI WA NISHATI]*

Mheshimiwa Spika, Ni kweli mahitaji yataongezeka na Serikali imejipanga mpaka sasa hivi kuna mkandarasi anaitwa *ABByuko* anaendelea kupanua ongezeko la umeme katika mji wa Mafia kutoka msongo wa MW. 11 mpaka MW. 33.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa mpango huu wa kupeleka umeme Mafia uko sambamba na kupeleka *Generator* za umeme Mpanda, mji ambao kwa sasa hivi ninapozungumza una tatizo kubwa, la umeme ambao mashine zilizopo zimechoka na hazifanyi kazi kwa ufanisi. Ni lini sasa Serikali itapeleka zile *Generator* ambazo ilikuwa imeahidi kama ilivyokuwa imeahidi Mafia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka *Generator* katika mji wetu ule bado uko villevile na *Generator* zinaendelea kuelekezwa katika mji huo na zitakopofika Mheshimiwa Mbunge utaona na tutatekeleza kama ambavyo ilivyokuwa imeahidiwa. (*Makofi*)

Na. 48

### **Kupanda kwa Kodi ya Pango**

**MHE. RUKIA HASSIN AHMED (K.n.y. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** aliuliza:-

Hivi karibuni Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) lilipandisha kodi ya pango kwa zaidi ya asilimia mia tatu (300%):-

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha kuwepo kwa mabadiliko hayo?

(b) Je, hali hiyo imeathiri vipi wapangaji wa nyumba hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yaWaziri wa Ardhi Nyumba na Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu a, b na c kama ifuataavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mwezi Agosti 2011, Wizara yangu kupitia Shirika la Nyumba la Taifa lilipandisha kodi za pango. Kwa muda mrefu viwango hivyo vilikuwa chini ikilinganishwa na viwango vya kodi vya soko la nyumba nchini wakati Shirika la nyumba linaanza zoezi hilo la kuhuisha kodi ya pango wastani viwango vya kodi za nyumba za makazi ulikuwa takribani asilimia 25 ya kodi za soko wakati kodi ya nyumba za wafanya biashara binafsi ikiwa ni asilimia 40 ya kodi halisi ya soko.

Mheshimiwa Spika, sababu zilizopelekea kupanda kwa kodi ni utekelezaji wa maelekezo ya Sheria Na. 11 ya Mwaka 2005 iliyorekebisha Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa Na. 2 ya Mwaka 1990 ambayo iliipa Shirika la Nyumba la Taifa mamlaka ya kufanya marekebisco ya viwango vya kodi. Kifungu cha 25 cha Sheria hii, kinaitaka Shirika kujidesha kibashara kadhalika kifungu cha 26 kinaainisha vigezo vya kuzingatiwa na Shirika wakati wa kufanya marekebisco ya viwango vya kodi. Vigezo hivi ni pamoja na ukubwa wa nyumba, matumizi ya nyumba, thamani ya nyumba ikilinganishwa na kiasi cha pango, eneo ilipo, mahali ilipo nyumba na hali ya nyumba. Vigezo vingine vilivyoanishwa kaika kifungu hiki ni pamoja na kodi ya kiwanja, gharama za bima kodi ya majengo, kodi nyinginezo pamoja na matengenzo ambayo Shirika ilitakiwa kuyafanya kulingana na mikataba ya upangaji.

Mheshimiwa Spika, marekebisco ya viwango vya kodi za pango uliyofanyika uliendana na matakwa ya Sheria utekelezaji wa mpango mkakati wa Shirika pamoja na dhamira ya kuboresha nyumba zake ili kuondoa malalamiko ya muda mrefu ya wapangaji wake.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MA. YA MAKAZI ]

(b) Mheshimiwa Spika, ongezeko la kodi ya pango humaanisha kuwa wapangaji wanalipa zaidi kuliko walivyozoea. Kwa hali ya kawaida hii ina maana kuwa mpangaji atalazimika kupunguza matumizi kwenye maeneo mengine ili amudu kulipa kiasi cha kodi kilichoongezeka. Hivyo ndio athari ambayo tunaweza kuelezea kutokea. Pamoja na marekebisho hayo ya kodi ya pango kwenye nyumba ya Shirika ambayo bado yanaendelea, viwango vya kodi ya pango bado viko chini ikilinganishwa na viwango vya kodi ya nyumba za wamiliki binafsi.

Mfano, wapangaji wa nyumba za Shirika zilizoko Dar es Salaam maeneo ya Masaki, Upanga, Kurasini, Chang'ombe, Msasani na *Oysterbay* wamekuwa wakilipa viwango vya chini sana kuliko wapangaji wa nyumba binafsi maeneo ya Sinza, Ilala, Magomeni, Tandika na Mwananyamala. (*Makofî*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu dhaifu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhamira ya Serikali ya kujenga nyumba hizi ni kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa dhamira hii imebadilika na imekuwa nyumba hizi kwa ajili ya matajiri na watu wa kipato cha juu?

(b) Kwa kuwa Serikali hii hii iliwauzia baadhi ya wakubwa wa Serikali nyumba kwa bei ya chee ya kimjomba.

Je, hawaoni sasa wafanyakazi hao, watu hao wanaoishi katika nyumba hizi ambao wengi wao ni wastaafu walikwisha itumikia nchi hii kwa muda mrefu na ni wanyonge wakawauzia nyumba hizi nao vile vile kwa bei ya chini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nyumba Maendeleo na Makazi, napenda kujibu swalil la nyongeza la Mheshimiwa Rukia Ahmed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalil la kwanza dhamira ya kuhudumia watu wa kipato cha chini imebadilika na kwamba sasa nia imekuwa ni kuwahudumia watu wa kipato cha juu, siyo ya kweli. Kwa sababu kama ambavyo nimeeleza. Kwa mfano, kodi inayolipwa na mpangaji alioko katika magorofa ya llala, ukilinganisha na mtu alieko mtaa wa Arusha pale pale llala kwenye nyumba ya mtu binafsi ni kifo na usingizi. Kwa hivyo, siyo kweli kwamba dhamira ya Serikali imebadilika kwamba tunahudumia watu wa kipato cha juu.

Mheshimiwa Spika, Swalil la pili. Kuhusu suala la kuuza nyumba za Shirika. Mheshimiwa Spika, suala hili tumelijibu mara nyingi sana hapa Bungeni na maelezo tunayatoa ya kina kwamba Shirika limeelekezwa na Serikali kujenga nyumba na kuwauzia wananchi. Nyumba ambazo zimekuwa zikizungumziwa muda mrefu kwamba tuwauzie wapangaji baadhi ya nyumba zilitaifishwa kutoka kwa wamiliki wa zamani, tukasema kwa kumwuzia mtu huyo mpangaji aliekuwepo sasa wakatika tulitaifisha kwa mtu binafsi ile dhamira ya kutaifisha itakuwa haipo. Hiyo moja la pili kwamba baadhi ya nyumba hizi ambazo wanaishi wapangaji ziko kwenye maeneo ambayo kwa dhamani ya ardhi, thamani yake ni kubwa sana na kwa hiyo badala ya kumwuzia mtu mmoja nyumba ni bora kuvunja na kujenga jengo kubwa ambalo tutawenza kuwauzia watu wengi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, na kama ambavyo tunaelewa na ambavyo tutaona wiki ijayo tutazindua baadhi ya nyumba ambazo tumejenga kwa gharama nafuu na kuwauzia wananchi. Kwa hivyo nirudie kusema kwamba zile nyumba ambazo tulishazungumza huko nyuma hazitauzwa zitabaki kuwa chini ya Shirika. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Naomba tuendelee. Kama kawaida Wizara hii majibu yake yanakuwa ni marefu.

Na. 49

### **Kujenga Majengo ya Mahakama Mpanda**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Mji wa Mpanda ni Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi, lakini una uhaba mkubwa wa majengo ya Mahakama.

Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Arfi kwa ukomavu wake wa Kisiasa na kwa namna anavyofuatilia matatizo ya wananchi wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Mpanda ni Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi, lakini ina uhaba mkubwa wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo, Mhakama za Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uhaba huo uliopo katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 Serikali itajenga Jengo kwa ajili ya Mahakama ya Mwanzo Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kupitia mfuko wa Mahakama itaendelea kuongeza Bajeti ya Mahakama ili kujenga majengo hayo na sio kwa Mkoa wa Katavi pekee bali pia katika maeneo mengine ambayo hayana majengo ya Mahakama. (*Makofii*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa napenda kujuu kwamba ujenzi huo wa Mahakama ya Mwanzo Mpanda Mjini, unaanza lini?

Mheshimiwa Spika, Swali la pili, kwa kuwa nilikuwa nikiuliza juu ya ujenzi wa majengo ya Mahakama ya Wilaya na Mkoa ambayo kwa sasa hayapo na Jengo linalotumika halina hadhi hata kidogo ya kuendesha vikao vya Mahakama Kuu.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga badala ya majibu ya jumla fedha zitakapopatikana hata kama ikiwa 2020/2025 waambie watu wa Mpanda wajue kwamba mtajenga 2020/2025.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuhusiana na ujenzi wa Mahakama hii ya Mpanda Mjini itaanza lini nimeeleza kwamba katika mwaka huu wa fedha (2013/2014) hivi sasa tayari tumeshapata mshauri mwelekezi ambaye atapitia michoro iliopo pamoja na kufanya usimamizi katika ujenzi wa Mahakama hizo.

Lakini tunatarajia itakapofikia mwisho wa mwezi huu Desemba, 2013 tutakuwa tumeshampata mkandarasi atakaefanya shughuli hiyo. Kwa hiyo itshe kusema kwamba ifikapo Juni, 2014 Mahakama hii itakuwa imejengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili, anataka kupata kabisa muda mahsus ni lini Mahakama za Wilaya katika Mkoa wa Katavi za Mahakama za Hakimu Mkazi zitajengwa. Bajeti yetu ndiyo inayotuongoza kwa Mahakama za Mwanzo Nchi nzima. Tuna upungufu wa Mahakama za mwanzo 751 nchi nzima. Kwa Mahakama za Wilaya tuna upungufu wa Mahakama za Wilaya 62.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

Kwa hiyo, itoshe tu kusema kwamba tunajenga hatua kwa hatua na tunatambua nia yetu ya kusogeza huduma karibu na wananchi na tunajitahidi kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali wa maendeleo, lakini vilevile Serikali imekuwa ikijitahidi kuongeza fedha. Ukiangalia mwaka jana 2012/2013, mwaka jana wa fedha za Bajeti yetu ya maendeleo ilikuwa takribani bilioni ishirini (20) mwaka huu wa fedha Serikali imetenga bilioni 42.7.

Mheshimishwa Spika, ukiangalia katika fedha za uendeshaji mwaka jana tulikuwa na bilioni 57 mwaka huu imetenda bilioni 88 tunajitahidi kuuwezesha mfuko wa Mahakama kuwa na fedha za kutosha na tutajitahidi. Lakini vilevile nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kupitia Bunge lako Tukufu, tujitahidi pia tushirikiane na Mahakama kujenga kupitia nguvu za wananchi ili kupunguza mzigo kwa Serikali. (*Makof*)

**MHE. MARIAM KASSEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mahakama ya Mwanzo ilioko mijini Masasi ilichomwa moto mapema mwaka huu na hivyo wananchi kukosa huduma hii na sasa hivi huduma hiyo imekuwa ikipatikana katika chumba kidogo sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kukarabari Mahakama ile na kujenga ofisi ambazo zilitketezwa kwa moto kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niwape pole sana wananchi wa Masasi kwa kuchomewa moto Mahakama ile. Lakini tuhakikishe kwamba vyombo vya Sheria vitahakikisha watu wote waliohusika na tukio hili ambao wanarudisha nyumba juhudhi za Serikali watachukuliwa hatua. Lakini kwenye eneo la pili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]*

kwamba tunatenga fedha za ukarabati na kuhakikisha kwamba Mahakama hii inakarabatiwa haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

Na. 50

### **Tatizo la Ucheleweshaji wa Kesi Mahakamani**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Tarehe 30 Mei, 2013 wakati akijibu Swal Namba 315 Bungeni, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, alisema moja ya sababu za ucheleweshaji wa kesi mahakamani ni idadi ndogo ya watumishi waliopo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri watumishi wa kutosha ili kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba mnamo tarehe 31 Mei, 2013 wakati najibu swal Na. 315 lilitolizwa na Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, nilieleza kwamba mojawapo ya sababu za ucheleweshaji wa kesi Mahakamani ni idadi ndogo ya watumishi wa Mahakama waliopo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu huu Serikali kwa Mwaka 2012/2013 Serikali ilitoa kibali cha kuajiri jumla ya watumishi wapya 260 wa kada za Katibu Mahsus, Wasaidizi wa Kumbukumbu, Wasaidizi wa Ofisi, Walinzi, Madereva na Wahasibu. Mchakato wa kukamilisha ajira bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mahakama ya Tanzania inatarajia kuomba kibali cha kuajiri watumishi wapya wapatao 984 (ikihusisha Mahakakimu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]*

Wakazi Daraja la Pili wapatao 300 na watumishi wasio Mahakimu 684).

Mheshimiwa Spika, vilevile, utaratibu wa kutoa ajira ya mkataba kwa wastaafu utendelea kutumika kwa kada ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanza ambayo inakabiliwa na uhaba mkubwa wa watumishi. (*Makof*)

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswala mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba nimwulize.

Mheshimiwa Spika, ajira ambazo ziliombewa kibali mwaka 2012/2013 ni 260 ambayo ni idadi ndogo sana ukillinganisha na Mahakama zetu, jambo ambalo hadi sasa huo mchakato wa kutoa ajira hizo toka kwa Watumishi wa Mahakama haujakamilika, unaendelea kwa mujibu wa majibu yake, naomba niulize.

Je, ni mahakama ngapi na zipi ambazo zitafaidika na ajira hizo ambazo zitatolewa kwa kipindi hicho?

Kwa kuwa Mahakama ya Tanzania inategemea kuomba kibali cha kuajiri watumishi 984 mwaka 2013/2014, ajira zilizoombwa 260 hadi leo mwaka unakaribia kwisha tena hazijapatikana, hazijakamilika.

Je, kweli Serikali yetu ina nia ya dhati ya kuondoa tazizo hili la ucheleweshaji wa kesi mahakamani hasa ukizingatia Tanzania ni mionganoni mwa nchi zinazotathmini Utawala bora (*African Fair Review Mechanism*)?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

1. Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ajira 260 tunazozitarajia ni ndogo sana. Serikali yetu muundo wake ni mkubwa na nchi nzima katika Taasisi mbalimbali za Serikali zinahitaji Watumishi. Kwa hiyo, sisi tumeomba na tumeona kwa kipindi hicho zimetutosha na tutazitumia vizuri pindi mchakato utakapokamilika.

Lakini vile vile mwaka bado haujaisha, tumhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba si mara ya kwanza tumekuwa tukiomba vibali na tumekuwa tukipata mwaka 2011/2012 tuliomba kibali cha mahakimu 300 na tayari wameshaajiriwa na wanafanya kazi vizuri sana. (*Makofii*)

2. Katika swalii la pili kwamba kama kweli tuna nia ya dhati ya kupunguza mlundikano wa mashauri. Mhehimiwa Spika nia ya dhati ipo na mikakati mbalimbali tunayo, na hivi sasa nipende tu kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshapunguza mashauri kwa kiasi kikubwa. Ukiangalia tu kwa Mahakama kuu peke yake katika mwaka jana mwezi Desemba, 2012 kulikuwa kuna mashauri takribani 16,103 lakini mpaka kufikia hivi sasa tumeshapunguza mashauri 11,000.

Kwa hiyo, utaona pamoja na kwamba tunasubiri vibali vya ajira lakini bado kazi inafanyika. Lakini vile vile tunao mpango mahsus na mpango endelevu katika mahakama zetu ambapo tumewashirikisha Majaji wetu Wafawidhi wa Kanda na wamefanya vikao na Mahakimu na wameshawapangia viwango vinavyokubalika (*Standard Case Red Disposal*) na tayari kila Hakimu ameshapangiwa kutokana na eneo husika na kutokana na ugumu wa kesi mbalimbali na wanajua ni mashauri mangapi wanatakiwa kuyapunguza. Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tuendelee muda umezidi kuwa mbali na jana tuna kiporo. Waziri wa Fedha, tunaingia Ofisi ya Wizara ya Fedha Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid.

**Wizara Kutopewa Fedha Zilizokwisha Idhinishwa**

**MHE. NEEMA M. HAMID** aliuliza:-

Pamoja na kuwa Wizara zote hupitishiwa fedha wakati wa Bajeti lakini inapofika mwisho wa mwaka wa fedha huwa kuna malalamiko kuwa fedha hizo huwa hazipelekwi kulingana na Bajeti hasa fedha zile za Maendeleo.

(a) Je, tatizo hasa ni nini?

(b) Je, tatizo hilo litamalizwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANETH Z. MBENE):-**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge Iako Tukufu hupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi yenye uwiano sawa, yaani Makadirio ya Mapato sawa sawa na Makadirio ya Matumizi. Kwa kawaida, muundo wa Bajeti yetu una vyanzo viwili vyaa mapato, mapato ya ndani na nje. Wakati wa utekelezaji wa Bajeti, kiwango cha mgao (*disbursement*) hutegemea zaidi makusanyo halisi (*Actual Collection*) kutoka vyanzo vyote viwili. Hivyo basi, makusanyo pungufu au chini ya malengo yanaathiri mgao wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Serikali, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimwa Spika, kwa muda mrefu, Miradi ya Maendeleo yameendelea kutegemea zaidi fedha kutoka kwa Washirika wetu wa Maendeleo. Kuna wakati fedha za Washirika wa Maendeleo huchelewa kutolewa kutokana na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANETH Z. MBENE)]  
sababu mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa masharti ya awali ya mikataba kabla ya fedha kutolewa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutoa fedha pungufu ya Makadirio litaisha pale tu tutakapoweza kutimiza malengo ya kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyote kama yaliviyokadiriwa na kuimarisha vyanzo vyetu vya ndani vya mapato na kupunguza utegemezi na kuwa na ziada ya kukabiliana na matumizi ya dharura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Rita Kabati swali la nyongeza.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake na naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

1. Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa kuanzisha utaratibu wa *Capita Budget* badala ya mfumo wa sasa wa *Cash Budget* ili kupata fedha za maendeleo kwa wakati kuliko hivi hivi sasa?

2. Sasa tunafikia karibu nusu mwaka toka tunapitisha Bajeti humu Bungeni nikiri wazi Mheshimiwa Spika kwamba pesa hizi katika Mkoa wetu wa Iringa ikiwepi Wilaya ya Kilolo, Mufindi na Iringa Manispaa bado hatujapatiwa hizo pesa za Maendeleo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni asilimia ngapi labda anieleze ni asilimia ngapi ya fedha za maendeleo ambazo sasa wameshapeleka katika miradi mbalimbali toka tumepitisha hapa Bungeni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANETH Z. MBENE):-**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rita Kabati, kama ifuatavyo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANETH Z. MBENE)]

1. Kuhusiana na kutumia *Capital Budget* badala ya kutumia *Cash Budget* ambayo tunaitumia sasa hivi ni wazo zuri na ni jambo zuri kama Bajeti yetu isingekuwa tegemezi na kwa sababu sasa hivi kutumia *Capital Budget* na wakati bado Bajeti yetu inategemea wafadhili au Wahisani wa Maendeleo itakuwa vigumu kwa sababu mahitaji ya *Capital Budget* yanataka kuwa una pesa yako mwenyewe, unaitawanya kwa muda wa miaka kadhaa katika miradi yako mbalimbali ambayo umejiwekea na hususan miradi ya maendeleo. Lakini kwa jiinsi tulivyo sasa hivi *Cash Budget* inatufaa zaidi kwa sababu kubwa mbili:-

Kwanza inatuwezesha kuwa na nidhamu ya kusimamia Mapato pamoja na Matumizi. Lakini vile vile inaonyesha uwazi zaidi na kwa kweli kama tungekuwa tuna nidhamu nzuri zaidi *Cash Budget* ingetufaa kwa sasa hivi mpaka hapo tutakapokuwa na vipato ambavyo vina uhakika.

*Capital Budget* vile vile inazingatia zaidi masuala ya Maendeleo. Kwa hiyo, Miradi ya Maendeleo kwa sababu ni ya miaka mingi unakuta sasa *Capital Budget* inafaa zaidi kwa sababu unapanga yale matumizi kila mwaka kidogo kidogo kwa hiyo inakupa ule uhuru wa kuweza kubajeti vizuri zaidi. Lakini sisi tunategemea zaidi Wafadhili, na nidhamu sio kubwa sana kwa sasa hivi bado. Kwa hiyo, inatubidi tujiveke hivi tujibane ili tuweze kuwa na nidhamu nzuri zaidi kwa kuangalia vipaumbele na pesa tunazozi-*allocate*.

2. Kuhusiana na kiwango gani cha pesa ambayo imekwenda kwenye Bajeti ya Maendeleo sina takwimu sahihi sasa hivi kamili kwa sababu siwezi kuziweka kichwani zote lakini nitazifanyia kazi na nitatoa jibu kipindi kifupi tu baada ya sasa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Spika moja ya tatizo la Serikali ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HAMAD R. MOHAMED]

pamoja na ubunifu mdogo wa vyanzo vipyta ya mapato. Lakini kubwa zaidi ni hili alilosema Mheshimiwa Waziri kwamba bado nidhamu ya matumizi katika Serikali bado haijakuwa nzuri. Kwa mfano Bajeti ya safari za viongozi ilikuwa ni bilioni 15 sasa hivi wameshatumia bilioni 28.

Je, huoni kwamba hii nidhamu ya matumizi nayo ni tatizo kubwa sana ambalo Wizara imeahidi kulikabili lakini bado mmeshindwa kulisimamia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu,

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimia Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Ni kweli bado tunahitaji kuwa na nidhamu zaidi na hilo nikiri kuwa ni tatizo la Serikali. Sasa hivi na ni kazi ambayo tunafanya. Lakini kuhusiana na safari za Viongozi au Safari za watu Serikali, kuna safari ambazo wakati mwingine zinajitokeza bila kuzipangia na kwa hali hiyo inabidi pesa itafutwe kwa ajili hiyo.

Lakini ni jambo ambalo kwa kweli tunakiri na tutaendelea kulifanya kazi ili kuhakikisha kuwa mipango tulioipanga, Bajeti zilizopitishwa na matumizi yake vinaenda sambamba. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana naomba tuendelee muda wenyewe kama ulivyo, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, swalii linalofuata. Kwa niaba yake Mheshimiwa Aliko Kibona.

Na. 52

**Msongamano Uliopo Kituo cha Mpakana-Tunduma**

**MHE. ALIKO N. KIBONA (K.n.y. MHE. DKT. MARY M.MWANJELWA)** aliuliza:-

Kituo cha Mpakani Tunduma kina msongamano mkubwa ambao huchukua muda mrefu sana hali inayosababisha kufungua mianya ya rushwa.

Je, nini mkakati wa Serikali wa kupambana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe maelezo kuhusiana na swali hili, nasikitika kuwa hatukuweza kupata muda wa kumtafuta Mheshimiwa kufafanua. Lakini swali ni kuwa Kituo cha mpakani (lakini hatukuambiwa ni kituo kipi) Tunduma, kina msongamano (hatukuambiwa ni msongamano wa kitu gani). Kwa hiyo, tume *assume* katika kujibu kuwa anazungumzia kituo cha Forodha kwa sababu imekuja Wizara ya Forodha, kwa sababu imekuja Wizara ya Fedha nimechukua *assumption* hiyo na msongamano kwa maana ya magari ya usafirishaji.

Kwa hiyo, nitalijibu swali hilo kutokana na hilo Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika kituo cha Forodha cha Tunduma unasababishwa na ufinyu wa miundombinu kwa upande wa Zambia. Ufinyu huo wa miundombinu unaisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

kutoruhusu magari mengi toka upande wa Tanzania kuingia Zambia. Utaratibu huu wa kuruhusu magari kidogo kidogo kuingia upande wa pili wa Zambia husababisha mlundikano mkubwa wa magari kwa upande wa Tanzania.

Mheshimwa Spika, Serikali zote mbili zimechukua hatua za makusudi ya kuondokana na tatizo hili kwa kuweka mkakati sasa wa kujenga kituo kimoja cha ushuru wa forodha yaani (*One Stop Border Post*) kwa ajili ya kuharakisha shughuli za forodha katika kituo hicho. Usanifu wa awali unaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu wa Desemba, 2013 chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*).

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kuwa, kukamilika kwa ujenzi wa kituo kimoja cha forodha cha Tunduma na kuanza kutumika kutaondoa msongamano wa magari ikiwa ni pamoja na matatizo mengine yanayotokana na msongamano huo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Aliko Kibona, swali la nyongeza.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

1. Mheshimwa Spika tumezowea kuona miradi mingi ya Serikali ikichukua muda mrefu sana kukamilika. Sasa kwa sababu wananchi wa Tunduma wana kero kubwa ya msongamano wa magari ningependa sasa kujua.

Ni lini, Serikali imeweka ukomo kuwa kituo hiki kitakuwa kimekamilika ili kuwapunguzia bughudha Wananchi wa Tunduma?

2. Ni kutaka kujua kwa kuwa upo mpango wa kujenga kituo kimoja cha ushuru kwa Nchi zote mbili Tanzania na Zambia.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ALIKO N. KIBONA]

Je, isingekuwa vema kituo hicho kikajengwa pembeni au nje ya mji wa Tunduma badala ya kujenga pale Tunduma ambapo pana msongamano pia wa nyumba za Wananchi na hivyo kuleta msongamano ambao utakuwa ni endelevu?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aliko Kibona, kama ifuatavyo:-

1. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, sasa hivi kituo kiko tayari kuanza kujengwa, tumezungumzia kuanza kujengwa mwishoni mwa mwezi wa Desemba, yaani mwezi huu tulioko sasa hivi.

Naamini katika muda mfupi sana kituo hiki kitakuwa kimekwisha malizika kwa sababu pesa ya kukijenga ipo, sitaki kujikomiti ni lini kitaisha lakini najua kuwa kitaanza Desemba hii na naamini kwa umuhimu wake na uharaka wake kitachukua muda mfupi kujengwa. Lakini nitafuutilia kwa Wizara husika kusudi njue ni lini na nitamweleza Mheshimiwa Aliko Kibona, ili na Waheshimiwa Wabunge wengine waweze kupata taarifa hiyo.

2. Kuhusu kujenga kituo cha ushuru mbali kidogo kwa ajili ya kuzuia msongamano, aah, sina hakika sasa hivi kutokana na kuwa tayari mipango imeshaanza ya kujenga itakuwaje lakini naamini kuwa wataalam walizingatia yote hayo wakati wakifikiria kujenga kituo hicho.

**SPIKA:** Tuendele na swali lilitobaki Wizara ya Mambo ya Nchi, Mheshimiwa Zabein Mhita, atauliza swali hilo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alifika jana na akaona hilo Gereza, naomba kufuta hilo swali.

*(Swali Namba 53 lilitutwa na Muuliza swalii)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kunipunguzia muda, sijui mliona nini maswali yamekwisha, na muda pia umeisha. Waheshimiwa Wabunge niwatambue baadhi ya wageni walipo.

Waheshimiwa Wabunge, niwatambue pia baadhi ya wageni waliko hapa Bungeni. Ninao Wanafunzi 20 wa Shule ya Sekondari ya Pemba Mnazi, kutoka Wilaya ya Temeke Mkoani Dar es salaam wakiongozwa na Mwalimu wao Mkuu Ndugu Halifa Yongo. Naomba wasimame walipo. Ahsante sana, mnatakiwa msome kwa bidii, ahsanteni sana pamoja na mwalimu. *(Makofii)*

Tunao wageni wawili kutoka Asasi ya Tanzania *Rehabilitation Organisation* kutoka Dar es salaam, ambao ni Ndugu Athman Mohamed Mlimasungu (Mkurugenzi) sijui yuko wapi asimame alipo, ahaa ahsante na yuko Ndugu Bernard David Masamu, Mkurugenzi wa Mipango, Masamu asimame, ahsanteni sana.

Nina wageni wengine pale, nitawaambia baadaye sikupewa majina yao.

Shughuli za kazi eeh! Kaimu Mwenyekiti wa Huduma za Jamii Ofisi ya Bunge anatangaza kwamba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuwa leo Ijumaa tarehe 6 Desemba, 2013 Saa 7.00 mchana mara baada ya Kuahirisha Kikao hiki kutakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 219.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Halafu, bado lile swalii la Kamati ya Maadili tunaendelea kuwatangazia mliokuwa na fomuzenu rudisheni hapa, kuna *tendency* ya watu kusahau na mkisahau mnapelekwa kwenye Baraza la Maadili ni kama Mahakama kabisa, kwa hiyo wako hapa rudisheni fomu tarehe 30 ni kesho tu kwa hiyo fanyeni hivyo msisahau. Tunaendelea, Katibu tuendelee.

Kuna tangazo lingine. Siku moja tuliwatambulisha vijana fulani hapa wanaohusika na kitu kinaitwa *Uhuru Marathon* sasa *Uhuru Marathon* bahati mbaya inafanyika Dar es salaam tarehe 8 Desemba, 2013 na ina kilometra nyingi nyingi tu. Kwa hiyo, ni kitu cha hiari, mnakaribishwa wanaotaka kwenda. (Makof)

Tunaendelea Katibu. Msianzishe mchezo wa kila baada ya maswali Mwongozo, Mwongozo! Mheshimiwa David Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ndio wajibu.

**SPIKA:** Mnapenda majibu nimeshasema nawe endelea na kitu unachotaka kukisema.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 64 (7), Mheshimiwa Spika leo pamoja na siku zingine pamekuwa na mwenendo wa baadhi ya Wizara, Mawaziri wake, Manaibu Waziri kutokuwepo siku ambapo maswali yao yanapashwa kupatiwa majibu hapa Bungeni. Unakuta Mbunge ana swalii lake amepewa majibu tangu siku 3, na Serikali inayajua majibu hayo kwa muda mrefu lakini siku ambayo Serikali inapaswa kutoa majibu Waziri hayupo, Manaibu hawapo, matokeo yake Wabunge tunapewa majibu na Manaibu Waziri au Mawaziri wa Wizara zingine, hii ni moja ya sababu ya majibu ambayo yako chini ya viwango katika Bunge hili. (Makof)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DAVID Z. KAFULILA]

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, ni kwa nini usitumie mamlaka yako kikanuni kuhakikisha kwamba mwenendo huu unakoma ili kusudi Wabunge wapate majibu yenye viwango ambavyo vinastahili. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ee, uzuri Mawaziri wote ambao hawapo hapa na mimi najua hawapo, kwa sababu utaratibu wanaofanya sasa hivi wanapoomba ruhusa kwa Waziri Mkuu na mimi naambiwa. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Serikali hii Mawaziri wapo ee! Sasa lakini nilichokinote kwa mfano swali ulilouliza Mheshimiwa siyo swali lile la msingi hata angekuwa Waziri mwenyewe asingeweza kujibu, ni swali nje ya lile la msingi.

Kwa hiyo, kuwepo au kutokuwepo Mawaziri utaratibu upo, wameniaga wote na wasiokuwepo nawajua kwa nini hawapo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, siyo *why*. Tumesema ndivyo ilivyo, Serikali ni moja. Umetoa mfano, ameniandikia na kibarua hapa anasema Kenya. Kenya ni Kenya wenyewe. Sasa sisi tunachokifanya.

Lakini ninachokisema si kwamba Mawaziri wasijibu vizuri. Hiyo siyo sababu. Kujibu vizuri, mtajibu vizuri kwa sababu ni Serikali. Wakati wote mnapoahidi vitu fulani, yejote anayeahidi hata kama siyo Wizara, mjue mmeshaahidi kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo lazima mijibu baadaye.

Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naumwa sana. Jana nilishindwa kabisa kuja Bungeni. Leo nimeugua usiku kucha, nilikuwa na homa na bado haijaisha.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Mheshimiwa Spika, lakini nimekuja. Nimejikongoja hivyo hivyo kwa sababu nimeshangaa kidogo, msiba wa Bara zima ambao tumeupata usiku. Afrika hajatoa mtoto kama Mzee Nelson Mandela. Nilitegemea kwamba kwa uzito wa msiba huu, Bunge lako Tukufu lingeahirishwa angalau kwa leo. Lakini naona Bunge linaendelea kama kawaida, ndiyo maana nimekuja. Vinginevyo, nisingekuja.

**SPIKA:** Ahsante sana, tumeku-*miss* sana jana. Pole.  
(*Makofii/Kicheko*)

Lakini ngoja tuseme *serious note*. Mambo ya nchi yanakwenda kwa utaratibu wa nchi. Siyo kila mtu anaweza kufanya maamuzi yake. Sisi kanuni zetu za Bunge zinaposema ni nani akifariki tuwe tunaahirisha, zipo. Sasa sisi wenzio tumesimama hapa tumemkumbuka, kwa utaratibu tu wa kibunge, kesho tunatoa Azimio la Kumsifu na Kumpongeza. Mengine ni maamuzi ya nchi, hatuwezi kufanya tunavyotaka.

Kwa hiyo, tunaendelea. Katibu tuendelee.

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka 2013**  
(The Referendum Bill, 2013)

(*Majadiliano yanaendelea*)

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka  
2013(The Referendum Bill, 2013)**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jana tulikuwa na Mheshimiwa Wenje's hoja, sasa umeme ukazimika. Sijui alikuwa nani anayejibu pale, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tulikuwa tunashughulika na kifungu cha 5, maelezo yalitoka pande zote, nadhani mmejiandaa vizuri kwa leo.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza na Mheshimiwa Wenje, sasa sijui kama atakubaliana na ushauri wangu au .....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG, endelea kama mlivyokubaliana. Kwa sababu tungependa kusikiliza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la Mheshimiwa Wenje, *effect* yake ni kwamba kila anayeomba kufanya ile kazi ya kutoa elimu ya uhamasishaji, basi Tume ilazimike kumpa hiyo ruhusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yetu ni kwamba kazi ya msingi ya Tume hii inayosimamia *referendum* kwa mujibu wa *paragraph* ya 5, kifungu kidogo cha 3 ni kazi ya msingi ya Tume. Hii ya kuruhusu Vyama vya Kiraia na Vyama visivyo vya Kiserikali kutoa elimu na uhamasishaji kwenye Kura ya Maoni ni ya ziada. Makubaliano na Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba mapendekezo yalivyo pamoja na marekebisho tulioleta yabaki kama yalivyo na Tume itakapokuwa inakataa kuruhusu hivyo vyama, itoe sababu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani kwamba hiyo ni *safe guard* ya kutosha kama ambavyo inaonekana kwenye *schedule of amendment* ukurasa ule wa 2, *paragraph* ya (c), sehemu ya 6 ambako tunasema “*Where the Commission refuses a civil society or non governmental Commission to carry out civic education or awareness programme, the Commission shall state the reasons thereof*”.

Maana ya kifungu hicho, Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mahali ambako Mamlaka zinaambiwa zitoe sababu, maana yake ni kwamba mtu ambaye ana-*challenge* au anapinga uamuzi huo anaweza kuomba Mahakama Kuu ikaingilia kuona kama uamuzi huo ni wa busara au ni uamuzi unaozingatia misingi mikubwa ya sheria. Kwa hiyo, tunadhani kwamba inatosheleza na namshauri ndugu yangu, Mheshimiwa Wenje akubali kusudi tuendelee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje, tumalize hili suala.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya AG, nakubaliana na mapendekezo ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kuna nani mwingine alikuwa, Mheshimiwa John Mnyika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE SECOND  
READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

**D:** In Clause 6 by-

(a) deleting article “The” appearing at the beginning of subclause (1) and substituting for it the following phrase:

“Save as otherwise provided for under this Act, the”;

(b) renumbering subclauses (2) as subclause (3) and vice versa; and

(c) deleting the renumbered subclause (2) and substituting for it the following:

“(2) The Commission shall organize and supervise the conduct of poll during the referendum.”

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE SECOND  
READING OF A BILL ENTITLED  
"THE REFERENDUM ACT, 2013"

---

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled "The Referendum Act, 2013" is amended:-

E: In Clause 7 by-

- (a) inserting the words "upon consultation with the Commission" between the words "shall" and "appoint" appearing in subclause (2);
- (b) inserting immediately after subclause (2) the following subclauses:

"(3) The Commission shall issue guidelines providing for the appointment referendum returning officers and management of objections against such appointments.

(4) The guidelines issued under subsection (3) shall be binding upon the referendum returning officers

- (c) renumbering subclauses (3), (4) and (5) as subclauses (5), (6), and (7) respectively.

(d) adding immediately after the renumbered subclause (7) the following:

"(8) Any officer appointed under this Act shall, before assuming office, take an oath or affirmation in the manner to be prescribed by the Commission and be impartial, in performing his duties.

" Dodoma,  
.....2013

M.K.P.P.  
WM

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN  
JOHN MNYIKA MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO  
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL  
ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013

*Made under standing order 86(11) and 88(2)*

A bill entitled “**THE REFERENDUM ACT, 2013**” is amended as follows:

C: In Clause 7 in sub clause (2) between the word “shall” and the word “appoint” add comma and words “in consultation with the Commission” and comma.

Also after sub clause (5); add new sub clause 6 to read “Provided that every appointment of a referendum returning officer and referendum deputy returning officer under this section shall not be from among serving civil servants or public officials”.

.....  
**JOHN JOHN MNYIKA (MP)  
UBUNGO CONSTITUENCY**  
**4.12.2013**

**MWENYEKITI:** Nimepewa barua na Mheshimiwa John Mnyika, ambaye amepata dharura na nimeruhusu kumweka mwingine amwakilishie marekebisho ambayo alikuwa ameyaleta na mtu mwenyewe ni Mheshimiwa Wenje. Kwa hiyo, panapokuwa Mnyika nitamwita Wenje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo *clause 7*, tulikubaliana na Serikali na marekebisho tulioleta kwenye Jedwali la Serikali limezingatiwa. Kwa hiyo, haina tatizo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Kifungu cha 8

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE SECOND  
READING OF A BILL ENTITLED  
"THE REFERENDUM ACT, 2013"

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

The Bill entitled "The Referendum Act, 2013" is amended:-  
**F:** In Clause 8 by deleting subclauses (3) and (4).

Dodoma,  
....., 2013

M.K.P.P.  
WM

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN  
JOHN MNYIKA MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO  
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL  
ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013

*Made understanding order 86(11) and 88(2)*

A bill entitled '' **THE REFERENDUM ACT, 2013**'' is  
amended as follows:

**D:** In Clause 8 sub clause (1); remove the words "by office  
or" without replacement.

.....  
JOHN JOHN MNYIKA (MP)  
UBUNGO CONSTITUENCY  
04.12.2013

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 8 tunapendekeza kutoa neno moja la "office" ili *appointment* iwe "by name", yaani libaki ile *by name* peke yake. Tulikubaliana na Serikali tulipokuwa kwenye kikao cha *consultation* cha Kamati na walikubali kwamba watatoa neno "by office" ili libaki neno "by name". Lakini katika Jedwali la marekebisho ya Serikali, hawajafanya jinsi tulivyokubaliana. Kwa hiyo, napenda nipate *response* yao kwa nini hawajafamya tulivyokubaliana?

**MWENYEKITI:** Enhe upande wa Serikali, Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali ni kweli kwenye Kamati kama anavyosema Mheshimiwa Wenje, tulikubaliana. Lakini baada ya kushauriana, tunaona ugumu wa kuondoa ile "office".

Naomba Waheshimiwa Wabunge mtuelewe kwamba tunachosema hapa ni kwamba Afisa anayehusika, aidha ateuliwe kwa ofisi yake au ateuliwe kwa jina lake. Sasa akiteuliwa kwa ofisi yake ina maana kwamba itakuwa rahisi kwa Tume kutumia *facilities* za ofisi hiyo.

Tulikuwa tunafikiri kwamba hiyo ina tija zaidi kuliko ukiondoa tu hiyo "by name". Kama tunavyofanya kwenye Uchaguzi kwamba *DED* au Wakurugenzi wale wanateuliwa kwa ofisi zao. Kwa hiyo, inarahisisha zaidi pia kupunguza gharama zingine za kuendesha zoezi hili.

Kwa hiyo, tunashauri Mheshimiwa Wenje, pamoja na kwamba tulikubali kwenye Kamati; lakini baada ya kushauriana, Serikali imeona kwamba kwa kweli kuna tija zaidi kuweka yote mawili. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sababu za "by name" only, zilikuwa nini? Mheshimiwa Wenje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kupendekeza kutolewa "by office" ibaki "by name"

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

pale ilikuwa ni kwamba unapomteua kwa mfano *RAS* au Mkuu wa Wilaya, tuseme “*by office*” kuwa *Coordinator* wa *referendum*; kuna wakati mtu anaweza akafanya makosa au kuna kosa likatokea, lakini *simply because he was acting at the capacity “by office”*, ni ngumu kwa mfano labda kuchukua hatua.

Sasa ndiyo maana tulikuwa tunapendekeza kwamba mtu anapokuwa *appointed “by name”*, inafanya huyu mtu anakuwa *more responsible*; lakini pia yale mamlaka yake yanatoka, yaani yanabaki “*by name*” kama yeche *specifically for referendum*. Hii *argument* ya Serikali wanaposema kwamba unapo-*appoint “by name”*, itasaidia *Commission* kutumia vifaa vya huyu mtu unayemu-*appoint*, siyo *valid argument*. Kwa sababu hii sheria yenye inasema kwamba Tume itaruhusiwa kutumia maeneo yote ya Serikali au vifaa vya Serikali.

Kwa mfano, unapomteua Mkuu wa Wilaya “*by name*”, magari ambayo yapo kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya au Ofisi ya *RAS*, siyo magari ya baba yake, ni magari ya Serikali. Hata wakiamua kuchukua *lets say*, jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuna ofisi zingine wanaweza wakatumia, ile siyo mali ya Mkuu wa Wilaya *personally*, ni mali ya Serikali. Kwa hiyo, *argument* ya kutumia rasilimali za hawa watu ukiwateua “*by office*” siyo *valid* hata kidogo. Ndiyo maana tunaona kuna umuhimu, tulikubaliana kwenye Kamati na tulijadili sana kwa upana wake. Ndiyo maana tulikubaliana kwamba tukiweka “*by name*” inakua *more safe*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa wote na Mheshimiwa Wenje, ni kweli. Lakini baadaye tulipokwenda kutafakari vizuri na wenzetu wa Tume, tukagundua kwamba ukiweka “*by name*” ni ngumu.

Kwa sababu Tume ile ya Taifa ndiyo inayopewa fedha na Serikali na Bunge. Lakini baadaye zile fedha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, SERA, URATIBU NA BUNGE]

zinagawanywa kwenye Ofisi zile za Usimamizi za Wilaya na Mikoa. Ukimteua Wenje *by name*, unapeleka fedha kwenye akaunti ya Wenje *by name*, za kusimamia uchaguzi au kura ya maoni katika mkoa mzima; nalo halikubaliki. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tukafikiri *facility* nini pamoja na kutumia *facility* za majengo, magari na akaunti. Kwa sababu *operation* za akaunti za Serikali zinasimamiwa na Serikali. Serikali haiwezi kutoa fedha kupeleka kwa mtu binafsi kwenye akaunti yake kwa kusimamia kazi za Serikali. Tofauti hii anayoisema kwamba sheria inasema vifaa vyta Serikali, ni wakati wa kupiga kura - *poling stations*. Kwamba vituo vyta upigaji wa kura vitatumika vyovyyote, vyta Serikali au Watu binafsi.

Mfano uliotolewa mle ndani tukiwa kwenye Kamati, hofu yao ni kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa maana yake anaweza akateullwa Mkuu wa Mkoa. Wakuu wa Mkoa huwa hawajihusishi na mambo ya uchaguzi. Tume ya Uchaguzi hata mara moja hajjawahi kumtumia Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya. Kwa hiyo, tunatumia tu kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, lakini tunawalenga wale watendaji. Pale ndani ya utendaji, kuna mtu atatajwa. Tume huwa inamtaja mtu, nani *Supervisor* wa Mkoa na nani *Supervisor* wa ile Wilaya kama ni Mkurugenzi. Kwa hiyo, tunachukua ofisi. Hofu nilliona, walitaja Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa. Wakuu wa Mkoa nataka niwatoe hofu na Wakuu wa Wilaya, huwa hawahusiki na *process* hiyo, na hawatajwi. Ofisi katika wilaya inayohusika ni ya Mkurugenzi kwa sababu ana watendaji na ofisi, atasaidia katika kupunguza gharama na uendeshaji wa ofisi ulio *smooth* wa uendeshaji wa ofisi. Kule ni katika Ofisi ya RAS na watendaji wake.

Kwa hiyo, hivyo vifaa tunavyokuwa na hofu na utendaji ni pamoja na *financing*. Kwa sababu mtandao wetu wa Serikali ulivyo ndio unao-determine fedha ziende wapi, hata za Tume ya Uchaguzi. Kwa hiyo, nilifikiri Mheshimiwa Wenje turidhike tu kwamba Tume hivi sasa inavyofanya kazi ndivyo itakavyofanya kazi, lakini hakutakuwa na *abuse*. Kama yatatokea, nafikiri Tume inaweza ikashughulikia. Aamini tu kwamba Ofisi hizi za Serikali zinaweza kusimamia kwa ngazi

za Wilaya ili tupate nafasi ya kuweza kutumia *facility* badala ya kumteua mtu peke yake bila kuhusisha ofisi. Kwa hiyo, tungeomba tu kwamba vyote viwili viwepo.

**MWENYEKITI:** Sheria ya Uchaguzi baada ya mwaka 2005 ilifanyiwa *amendment* kwamba yule atakayekuwa ametajwa ataapishwa na anawajibishwa kama yeye. Iko sheria kabisa, iko sheria. Mheshimiwa Wenje, tumalize hili.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hoja ya pesa angalau ina mashiko. Kwa hiyo, nakubali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE SECOND  
READING OF A BILL ENTITLED  
"THE REFERENDUM ACT, 2013"

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

The Bill entitled "The Referendum Act, 2013" is amended:

**G:** In Clause 9 by deleting subclause (4) and substituting for it the following:

"(4) Where a person is a registered voter and his particulars are available in the voters' register but has lost the voter's card, the referendum officer shall, before allowing that person to vote, require that person to produce any identity which identifies him and fill a declaration form prescribed by the Commission."

Dodoma,  
....., 2013

M.K.P.P.  
WM

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON CECILIA  
DANIEL PARESSO MEMBER OF PARLIAMENT FOR SPECIAL  
EAT AT THE SECOND READING FOR THE BILL ENTITLED THE  
REFERENDUM ACT, 2013**

*Made under standing order 86(11) and 88(2)*

A bill entitled “**THE REFERENDUM ACT, 2013**” is amended as follows:

A: In Clause 9 (4); By deleting the words which appears between the words “to and fill”, also delete the word “before” appears between the words “form and allowing” and substitute with the word “and”

.....  
**CECILIA DANIEL PARESSO (MP)  
SPECIAL SEAT  
04.12.2013**

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Nimeleta marekebisho ya kufuta baadhi ya maneno katika kifungu hiki kidogo cha 4, kwa nini. Kwa sababu kwa matakwa ya kifungu hiki, kinamtaka mtu ye yote ambaye taarifa zake ziko kwenye Daftari la Kupigia Kura na amepoteza kitambulisho, basi Ofisa wa Tume atamtaka mtu huyu awasilishe kitambulisho kingine, ajaze kiapo ndipo apige kura.

Katika marekebisho ya Serikali, bado wameleta suala hilo hilo la kumtaka huyu mpiga kura alete kitambulisho kingine. Hoja hapa ni kwamba tunaelewa Watazania walio wengi, ukimwambia alete kitambulisho kingine kama amepoteza kitambulisho cha kupigia kura, Watanzania wengi walioko vijjini hawana vitambulisho vingine. Ni wachache sana wa Mijini ndio wanaweza kuleta. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa yasomeke kwa kuondoa maneno pale, na yasomeke ifuatavyo:- Kwamba “*where a person is a registered voter and his particulars are available in he voters' register but has lost the voter's card, the referendum officer*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*shall require that person to fill on the affidavit form and allowing such person to vote".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Tunaomba maelezo, Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Cecilia Paresso. Lakini nilikuwa namshawishi kwamba kwenye *schedule of amendment* ya kwetu tulio nayo. Tufute maneno yale maneno matatu ya mwisho "*produce any identity*", tuyafute hayo; tufute na maneno manne "*which identifies him and*". Kwa hiyo, itasomeka sasa na nitaeleza athari zake ni nini. "*Where a person is a registered voter and his particulars are available in the voters' register but has lost the voter's card, the referendum officer shall, before allowing that person to vote, require that person to fill a declaration form prescribed by the Commission*". Itakuwa ime-capture hiyo ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, na namshukuru sana, ametumia mawazo mazuri. Sasa athari yake ambayo siyo athari *negative* ni *positive*.

**MWENYEKITI:** Athari ya kwamba mkibadilisha mlivyo sema?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Tukifanya hivyo sasa, ina maana kwamba ile *obligation* ya ku-*fill form* siyo ya *referendum officer*, isipokuwa ni ya mpiga kura; ambacho ni kitu kizuri pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Huo ndiyo uelewa wangu na ninafikiri ndiyo uelewa ambaao watu wote wenye nia njema na ambaao hawataki kupotosha mambo, ndiyo uelewa wao pia. Hii ya kusema kwamba kuna watu wanafanya njama, kutisha; kwa kweli Mheshimiwa Wenje baba yako alikuwa Mwalimu wangu, siyo kweli. Siyo kweli kabisa! Nafikiri ungekuwa unazungumza kama Mzee Dibogo, mambo yangetuwa vizuri zaidi. Lakini sasa ukizungumza kwa sauti, sisi wengine tunakuwa na hofu, lakini hofu hii siyo ya msingi kwa sababu *process* hii inakuwa guided by two things, "yes" and "no". Lakini kinacho-guide zaidi kufikia muafaka ni ile akidi. Ile akidi ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba pendekezo hili pamoja na kwamba kuna *energy* imetumika, lakini tunappreciate energy na nimesikia *common sense*, lakini hili siyo suala la *common sense* kwa sababu *common sense it not common*. Kwa hiyo, tunashauri kwamba ibaki kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** Hapa ukiangalia hoja ya Mheshimiwa Wenje ina sehemu mbili; ina sehemu ya 35(3) halafu kuna ile ya tano ya ku-delete. Nafikiri ya ku-delete hapa mimi sioni sababu, kama ukiacha inakuwa nini halafu? Lakini hii ya tatu naomba nilelewe vizuri.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, with due respect, mantiki hapa ni kwamba tukienda kupiga kura, watu wakisema "yes" maana yake ni kwamba tunapata Katiba.

**MWENYEKITI:** Watu wa kutosha!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Tuseme “yes”, hiyo ya kutosha sasa, tutapata Katiba. Watu wakisema “no”, kwamba no ika-*prevail*, maana yake ni kwamba hatupati Katiba, lakini pia kutakuwepo na sababu za msingi za watu kusema “no.”

Ndiyo maana nasema, *is just a common sense* kwamba watu wanaposema “no” na sababu watakuwa nazo, *is just a common sense* kwamba hizi sababu ziwe *revealed* kuliko kurudi kwenye *process* upya au kuliko kuendelea na Katiba ambayo tuna-*feel/leo* kwamba haikidhi matakwa ya maisha ya leo. *It is just a common sense* kwamba watu wanaposema “no” na “no” ika-*prevail* watakuwa na sababu. Kwa hiyo, kuna haja tu ya hizo sababu kuwa *revealed* halafu Tume ikapewa mamlaka ya kuitisha tena siku ya kupiga kura baada ya hayo matatizo au hizo changamoto kuwa *addressed*.

**MWENYEKITI:** Hiyo itakuwa ni mara ya tatu!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** *The thing is...*

**MWENYEKITI:** Kwa sababu kuna mara ya kwanza hamjafikia *fifty fifty*.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Yes!

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, wanapewa *six days*; tena wakapiga baada ya *six days* ikawa kama vile zamani, ndiyo wanasema kwamba tutaendelea na hii Katiba ya sasa. *Subject* ya kuangalia hayo unayoyasema, lakini huwezi kuyalundika hapa, maana yake itabidi kwanza mtulie na bila shaka hilo suala litakuwa ni refu na kama litakuwa ni refu hakiwezi kuwa ni kitu cha kubadilisha tu mkato au nini, *that is what I understand* kwamba mtatumia hiyo wakati mnaangalia tena huu utaratibu mwингine na ku-*consider* hayo yanayoweza kuwepo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWANYEKITI]

Nilifikiri ndivyo inavyotazamika kwamba tunapiga mara mbili, lakini hii ya tatu itabidi turudie ya zamani lakini sasa tuangalie upya, *what was the contention?* Nadhani ndivyo inavyosomeka hivyo.

Mheshimiwa Wenje, ndivyo tunaelewana hivyo, au mimi nasema vinginevyo?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa. *Logic* yangu ilikuwa ni kwamba watu wakisema “no” watakuwa na sababu, inawezekana hizo sababu siyo nyingi sana kiasi kwamba kuzi-*address* inaweza kuwa ni rahisi sana na tukarudi tena kupiga kura, *that was my concept.*

Vilevile, inaweza ika *serve* Taifa, kwa mfano usipotumia gharama nyingi ya kurudi tena kuanza mchakato upya. Hiyo ndiyo ilikuwa ni *logic* yangu. Lakini...

**MWENYEKITI:** Nafikiri unayo, lakini mimi nilikuwa nafikiri kuingia *second time* ni lazima mu-*address* vitu walivyolalamika, *otherwise how would you change the outlook?*

Sasa ya pili mmepeiga, wamesema “no”, si ndiyo mnarudi kwenye ile ya zamani ili mwendelee kuangalia mchakato upya.

Hebu mtusaidie, Mama Anna Kilango niliona umesimama.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi kwenye hiki kifungu cha tano nakubaliana na Serikali na naisihi isije ikakubali kuingia kwenye mtego kwamba watu wakisema “no” yenyewe imeandika vizuri kwamba watu wakisema “no”, tuendelee na ile Katiba ya zamani.

Hiki kifungu Serikali msije mkaingia kwenye mtego mkakiacha, kwa sababu tutakapoacha tuseme watu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANNE K. MALECELÀ]*

wakisema "no" and then tusiandike kwamba tuendelee kutumia Katiba ya zamani, hawa hawa wanaweza wakaja wakatugeuka kwamba kwenye sheria hamkuweka kwamba tuendelee kutumia Katiba ya zamani.

Kwa hiyo, mimi narudi hapa kwamba hii iendelee kuwa hivi hivi kwamba watu wakisema "no" basi tuendelee kutumia Katiba ya zamani. Iwe hivi hivi kama ilivyo. Ahsante. (Makofî)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Abdallah!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka na mimi nizungumze kama alivyo sema Mheshimiwa Anne Malecela. Lakini naomba niseme tu kwamba mchakato wa Katiba hata huu tunaoendelea nao sasa umechukua muda mwiningi sana, sasa tutakwenda mara ya tatu watu wamesema "no", maswali haya tunayowauliza ni "ndiyo" au "hapana," hatuwaulizi kwa nini mmesema "ndiyo" wala hatuwaulizi kwa nini mmesema "hapana". Wakisema "hapana," mimi nafikiri tunarudi tulikotoka. Sasa hao watakaokuwa madarakani, wataanzisha mchakato mpya mwininge wa Katiba, lakini vinginevyo tutakuwa tunaendelea na Katiba kila siku, hatutafanya kazi katika nchi hii na tuna mambo mengi ya kufanya kuwaendeleza wananchi.

Mimi nashauri kwamba hivi ilivyo ni sawasawa kabisa. (Makofî)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge!

**MHE. ANDREW J. CHENGÈ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ni eneo la msingi sana katika Muswada huu na sisi kama wanasiasa ni vema tukatambua kwamba katika hatua ya kwanza mmejaribu, hamkupata akidi inayotakiwa; mwaniasiasa yejote, kwa sababu ninyi ndio mmeshiriki katika majadiliano ya Katiba na vifungu ambavyo vimeingizwa katika rasimu hiyo ambavyo mnasema ni *contention*, yaani zina mabishano; sasa wanasiasa katika hatua ya kwanza ambapo hamkupata, mnasubiri zile siku 60, ndiyo *political*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE]*

league work inaanza, vyama vyaa siasa na wadau wengine wote wenye nia njema na mapenzi kwa nchi hii watasema.

Natoa mfano tu, kwamba sisi tunachukia rasimu hii ya Katiba kuingiza vifungu ambavyo vinakiuka imani yangu ya dini, mnaruhusu; mfano tu nasema, U-Cameroon. (*Makofi*)

Eeh! Inazua mijadala mikubwa sana na wanasiasa mtalijua hilo kwamba jamani turudi tena tukayanyooshe haya na ndio yote haya yamewekwa kwa namna hiyo, unapata *a breathing point*, mpumue vizuri halafu mnatulizana, joto linapungua mnakuja kukutana ili kwenda mbele, mnapiga tena kura. Lakini mtakuwa mnatembea nchi nzima kuelezea kwa nini tunataka ibaki kama ilivyo au isiwe hivyo.

Mimi nataka kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili liliwyowekwa na Muswada wa Serikali limekaa vizuri sana na ninaomba tuliunge mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 36

### **SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED “THE REFERENDUM ACT, 2013”**

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

- T:**      In Clause 36 by-
- (a) adding the following marginal notes “Procedure for conduct of referendum”

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

- (b) deleting the word “Part” appearing at the end of this clause  
and substituting for it the word “Act.”

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 37

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

- U:** In Clause 37 by-
- (a) redesignating clause 37(1) as clause 37;
  - (b) deleting the words “who are outside the United Republic or”  
appearing in the redesignated clause;
  - (c) deleting subclause (2).

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kidogo. Kwenye kifungu cha 37 pamoja na marekebisho tuliyofanya, naomba kwenye mstari wa pili yapo pia maneno yanatamka "*the citizens of Tanzania*," naomba hayo maneno yafutwe na badala yake liwe neno moja tu "*voters*". Kwa hiyo, isomeke *the Commission may make special provisions for voting a referendum for voters who will not be able to vote*, yaendelee sawasawa.

Pia mstari wa pili, maneno "*the citizens of Tanzania*" yafutwe na badala yake liwekwe neno moja tu, "*voters*".

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 38

Kifungu cha 39

Kifungu cha 40

Kifungu cha 41

Kifungu cha 42

*(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

**V:** In Clause 43 by deleting subclause (2) and substituting for it the following-

“(2) A referendum committee shall only be allowed to file a petition to the High Court challenging referendum results if-

- (a) it is the referendum committee at the national level; and
- (b) it obtains not less than ten percent signatures of the total number of the registered voters from each part of the Union of at least five constituencies.”

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 44

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

---

*(Made under S.O. 86(10)(b)*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

**W:** In Clause 44 by adding the words “as may be determined by the Registrar” after the word “shilling” appearing at the end of subclause (1).

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 45

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

---

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

- X:** In Clause 45 by deleting the word “fourteen” appearing in subclause (2) and substituting for it the word “twenty one”.

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
WM

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 46

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

---

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

**Y:** In Clause 46 by deleting the word “seven” appearing in subclause (3) and substituting for it the word “fourteen”.

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 47

Kifungu cha 48

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49 kipyta

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT  
THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

**Z:** By-

(a) adding after clause 48 the following new clause:

“Rules of procedure **49.** The Chief Justice may, after consultation with the Chief Justice of Zanzibar, make Rules of procedure for referendum petitions and appeals under this Act.”

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

- (b) renumbering clause 49, 50, 51 and 52 as clause 50, 51, 52 and 53.

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

*(Kifungu Kipywa cha 49 kilipitishwa na  
Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu 50 – ambacho kilikuwa kifungu cha 49

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51 – kipywa

**MWENYEKITI:** Tunaposema kifungu kipywa ni  
*renumbering* jamani, siyo kipywa cha *substance*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52 - kipywa

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 53 - kipywa

**SCHEDE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

---

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

AA: Adding immediately after Part V the following:

“PART VI

CONSEQUENTIAL AMENDMENTS

Construction**53.** This Part shall be read as one with the Constitutional Cap.<sup>83</sup> Review Act hereinafter referred to as the “principal Act”.

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 54 – kipyta

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

---

*(Made under S.O. 86(10)(b)*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

Addition of  
sections  
28A and  
28B

**54.** The principal Act is amended by adding immediately after section 28 the following:

Publication      **28A.-**(1) Upon the passing of the proposed and submission Constitution by the Constituent Assembly, the Chairman of the Constituent Assembly shall, within seven days submit the proposed Constitution to the President.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

(2) The President shall, within seven days after receiving the proposed Constitution and upon consultation and agreement with the President of Zanzibar, publish the proposed Constitution in the *Gazette* and other local newspapers.

Validation of      **28B.** The referendum Act shall apply in respect of  
proposed               validation of the provisions of the proposed Constitution.”  
Constitution

Dodoma,  
....., 2013

**M.K.P.P**  
*WM*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na *thrust* ya mapendekezo ya Serikali kwenye kifungu cha 54 kile kifungu kipycha (28)(a), lakini nauliza kwa upande wa Serikali, maneno tuliyotumia “*upon the passing,*” hatuwezi tukawa wakweli tu katika hatua hii ambapo Bunge Maalum la Katiba limepitisha rasimu, tukasema “*upon enactment*” kwa sababu ndiyo kazi ya Bunge la Katiba. Tunajua tunakwenda kwenye *referendum* lakini kule ndiyo ku-validate au kuthibitisha ama kuidhinisha. Naomba tu kama Serikali itakubali, twende na lugha ya kisheria ya kikatiba kwamba badala ya “*passing*” tuseme “*enactment.*”

La mwisho, kwenye kifungu kidogo cha (2), tumempa Rais ile kazi kwamba atafanya hicho, atakifanya na atakifanya baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar, Rais achapishe. Tunajua kwamba yeche huwa hachapishi. Hivyo basi, nashawishi tuone kwamba afanye hivyo or course to be published maana ndivyo itakavyotokea. Sijui kama Mwanasheria Mkuu ataelewa hoja yangu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Kwanza naomba nипитише hiki kifungu kipyä cha 54, lakini hiki anachokizungumzia ni kifungu kipyä cha 55. Kwa hiyo, tupitishe kwanza hiyo cha 54 kipyä.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge sasa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mtemi Chenge, *monitor* wangu. Kwenye mapendekezo ya *enactment* katika *stage* ya Bunge la Katiba kwa kweli halienact, hili lina *adopt*. Labda tukubali tuseme "*upon the adoption*." Kwa sababu hii kazi ya "*enact*" ni kazi yetu, *we the people*. Wale wakishapigia kura, sasa wale ndio wanenact. Hiki ni kitu ambacho tunatakiwa tukifahamu kabisa kwamba Bunge la Katiba halina mamlaka ya mwisho kwenye utungaji wa Katiba. Wenye mamlaka ya mwisho ni sisi wananchi wa Watanzania kwa umoja wetu na kwa rangi zetu wote.

Kwa hiyo, nilikuwa nakubaliana na Mheshimiwa Chenge kwamba badala ya kusema *upon the passing*, tutumie tu *adoption* kama ambavyo Sheria ya Marekebisho ya Katiba yanavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii ya pili, kifungu cha 28(a) ya pili nakubaliana naye kwamba *the President shall within the seven days after receiving the proposal Constitutional and upon the consultation of agreement of president of the Zanzibar cause to be published the proposal Constitutional in the Gazette to be enacted Constitutional. sorry no proposal to Constitutional. Cause to be published the proposal Constitutional in the Gazette and other local newspaper.* Nafikiri atakubaliana na mimi Mheshimiwa change.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Tupo wote au arudie tena? Tupo wote. Kwa hiyo, hii itakuwa 55. Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria kwa ufanuzi mzuri tu. Sina tatizo na neno "*adopt*", hayo ndiyo maneno ya Katiba kwa sababu anasema "*we the people*" tunajipatia Katiba hii. "*We adopt and enact the Constitutional.*"

Kwa hiyo, mimi sitegemee kwamba tutakapoenda kwenye Kura ya Maoni kwa wananchi, wananchi wenye Katiba yao kwamba tutakuwa na nafasi kuongeza maneno. Kwa sababu maneno yale yatakuwa kwenye ile *preamble* inapofika mwisho; *Now therefore*, sisi wananchi wa Tanzania, kama Katiba ya Tanzania ya Jamhuri ya Muungano inavyosema sasa hivi, maneno hayo utayakuta. Ndiyo yatakayopelekwa katika ujumla wake wa Rasimu hiyo ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi ninsingependa kwa sababu najua Bunge la Katiba litashughulika na masuala haya. Nisingependa nichukue muda wa Kamati yako kwa hili. Lakini mimi nadhani tungeliweza tukalinyosha tu hapa. Lakini sina tatizo na maneno ya Mwanasheria Mkuu.

**MWENYEKITI:** Ulifikiri tulinyoshe namna gani?

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme "*adopt*" badala ya kusema "*passed*."

**MWENYEKITI:** Nafikiri ndivyo tulivyokubaliana kwamba "*upon adoption of the proposed Constitutional*" ndiyo kilivyo sasa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Jedwali

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE  
SECOND READING OF A BILL ENTITLED  
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

---

*(Made under S.O. 86(10)(b)*

---

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

**BB:** In the Schedule by deleting the word “FIRST” appearing in that Schedule.

Dodoma,

**M.K.P.P**

....., 2013

*WM*

*(Jedwalli lilitotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

*(Bunge lilitrudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa mwaka 2013, sasa ukubalike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*(Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka 2013  
(The Referendum Bill, 2013) uliridhiwa na Bunge  
na Kusomwa kwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, mimi binafsi nadhani hilo nililokuwa nasema *political maturity* nadhani ipo. Wale walioleta *Amendments* wamekuwa *very considerate*, wametoa maoni yao, wametoa *arguments* zao na wote tumeku-*consider* jambo ambalo ndilo naliomba liendelee hivyo. Sisi wenzeni tuliookaa humu ndani ndivyo tulikuwa tunafanya hivyo. (*Makofi*)

Kwa mfano, nilisema nimempa ruhusa Mheshimiwa John Mnyika aandike barua kumteua mtu mwingine. Kama Mheshimiwa Ezekia Wenje angekuwa haku-*network* na Mheshimiwa John Mnyika hapa, ingekuwaje? Sasa maana yake hapa Mheshimiwa Ezekia Wenje inaonekana anafahamu kile ambacho alikuwa anataka kuleta Mheshimiwa John Mnyika ndiyo maana amekuwa *confident enough* kuweza ku-*present* kwa niaba ya Mheshimiwa John Mnyika. Kwa hiyo, kuna dalili ya *networking*. (*Makofi*)

Sasa tuiongeze *network* katika kutunga Sheria mwende kwa Vyama vyote *across*. Mki-*network* huko nje hakutakuwa na kusema niunge mkono kwa sababu kasema huyu, hakuna. Tuki-*network* katika *amendment* pamoja *all part cross* yaani tu-*network* tu; najaribu ku-*buy* wazo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba labda tutengeneze kitu ambacho kinakuwa cha Vyama vyote kujadiliana hivi nje ya hapa mahali, nadhani tunaweza kwenda vizuri. Mimi leo nimefurahi. Maana Mheshimiwa Ezekia Wenj asingekuwa ame-*network* na Mheshimiwa John Mnyika asingeweza. Mheshimiwa John Mnyika kwa dharura alinipigia simu usiku kwamba hatakuwepo.

Kwa hiyo, mimi nashukuru, tuendelee na mtindo huu huu ndugu zangu kwa sababu ni lazima tutoe heshima yetu kwa watu wetu kwamba tumeletwa hapa *very responsibly* kufanya kazi hii. Mimi nawashukuruni sana kwa hatua zetu za kwetu katika mchakato wa Katiba tumemaliza hapa. Sasa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*(WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE))*  
hatua iliyobaki ya Bunge la Katiba siyo letu sisi ni la watu wote wale mia sita na kitu. Kwa hiyo, sisi kwa *referendum* hii tumemaliza na *I hope* hakuna kingine kitakachotokea zaidi ya hapo, kwa sababu tumetoa uhuru wa kutosha kabisa.

Kwa hiyo, nawashukuruni sana wote, Vyama vyote na tuendelee na *spirit ya kujenga nchi yetu*. Hakuna mwingine atakayejenga nchi hii, ni sisi wenyewe. (*Makof!*)

Leo atakuwepo fulani anatawala, kesho anatawala na mwingine, naye pia awe huru kwa Katiba tunayotunga sisi. Siyo kwamba Katiba impende mmoja halafu imchukie mwingine, haiwezekani, hiyo siyo Katiba. Kwa hiyo, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, chukueni hili kama ni suala zito katika miyo yetu na kumwogopa Mwenyezi Mungu. Katibu!

### **HOJA ZA KAMATI**

#### **Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Bajeti**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilitoa taarifa kwamba Kamati *PAC* itawasilisha taarifa yake kesho, kwa sababu haiko tayari. Kwa hiyo, nitamwita Mwenyeekiti, wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa atatumia nusu. Tutaona tutakavyoendelea. (*Makof!*)

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali naomba kwamba taarifa yangu yote iingizwe kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge, 2013, naomba kuwasilisha Bungeni Taarifa yenye Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kama yalivyooneshwa katika taarifa ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge (2013), Muundo wa Taarifa hii upo katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Utangulizi inayowatambulisha Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati, Majukumu ya Kamati (Hadidu za rejea), na namna majukumu ya Kamati yalivyotekelizwa.

Sehemu ya Pili inatoa maelezo kuhusu vyanzo vyamapato katika Serikali za Mitaa, mwenendo wa upatikanaji wa ruzuku ya Serikali Kuu katika Serikali za Mitaa, uwezo wa Serikali za Mitaa kujitegemea kimapato, matokeo ya Ziara na Mahojiano ya Kamati wakati Sehemu ya Tatu inahusu Hoja ama Mapendekezo ya Kamati kuhusu masuala yaliyobainika.

Katika Sehemu ya Tatu, Mapendekezo yamewasilishwa kama Hoja za Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 54 (2) ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuijadili na kuiasili (*adopt*) Taarifa; hivyo kuyafanya Mapendekezo kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali. Kwa msingi huo, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali itawasilisha Bungeni majibu ya kina kuhusu Hoja za Taarifa hii na Taarifa nyingine kwa kuzingatia utaratibu wa Kibunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ina Wajumbe Kumi na Tisa wafuataao: Mheshimiwa Rajab M. Mohammed - Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani J. Zedi - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Alphaxard K. Lugola, Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Munde T. Abdallah, Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa Tauhida C. G. Nyimbo, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Yusuph Abdallah.

***Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)***  
*[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAAJ]*

Mheshimiwa Spika, huduma ya mawasiliano na ushauri kuhusu shughuli na taratibu za kibunge, uandishi wa taarifa na mihtasari, utafiti na uchambuzi wa masuala mbalimbali ilitolewa na Katibu wa Kamati Ndg. Dickson M. Bisile akisaidiwa na Ndg. Chilemeji C. Nyamwaja na Ndg. Waziri Kizingiti.

Mheshimiwa Spika, Hadidu za Rejea za Msingi kwa ajili ya Kamati hii ni majukumu yake ya Kikanuni ambayo yameainishwa katika Nyongeza ya Nane, fasili Ndogo ya 13 ya Kanuni za Bunge (2013) kuwa ni:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba tatizo la matumizi mabaya ya fedha linapungua katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati imeweza kukagua Hesabu za Halmashari mbalimbali nchini na kufanya ukaguzi wa thamani (*value for money*) na Ukaguzi wa ufanisi (*performance audit*) katika Halmashauri hizo. Kamati ilibaini Udhifu mkubwa katika maeneo makuu matatu:-

(a) Uwajibikaji Usioridhisha katika Halmashauri zetu nchini;

(b) Utekelezaji duni wa miradi mingi ya maendeleo, kwani miradi mingi hailingani na thamani ya pesa iliyotumia; na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

(c) Uwezo mdogo wa Wataalam katika kusimamia fedha za Umma zinazopelekwa kutekeleza miradi mbalimbali katika Halmashauri nchini.

Aidha, ili kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, maafisa kutoka Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Hazina na TAMISEMI huunda Kamati Ndogo ya Wataalam kwa ajili ya kuwashauri Wajumbe wa Kamati mwenendo wa kitaalam kuhusu namna ya kushughulikia hoja za Ukaguzi. Kamati hupima majibu ya hoja za ukaguzi kwa njia ya mahojiano (mezani) na ziara za ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kwa njia ya mahojiano, majibu ya Hoja za Ukaguzi kutoka katika Halmashauri hujadiliwa na kutathminiwa na Kamati kwa nia ya kubaini ukweli ama mantiki ya matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri husika.

Aidha, katika Ziara, Kamati hujielekeza katika kuangalia ubora na thamani ya miradi iliyotekelizwa. Ziara za Kamati zimekuwa zikifadhiliwa na Mradi wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma [*Public Finance Management Reform Programme (PFMRP)*] kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yaliyoorodheshe hapo awali, na wewe unayo mamlaka ya kuipatia Kamati hii jukumu lingine kwa kadri utakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili inahusu matatizo sugu katika mapato na matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kuhusiana na Ruzuku ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, 90% ya fedha za Serikali za Mitaa ni ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa utaratibu uliowekwa katika Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977). Chini ya Utaratibu huu, Bunge huidhinisha maombi ya fedha yanayowasilishwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

kawaida na matumizi ya maendeleo Serikalini zikiwemo Serikali za Mitaa.

Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 ruzuku ya Serikali Kuu katika Serikali za Mitaa ilikuwa ni jumla ya Sh. 557,606,455,000/= ambapo Sh. 291,669,791,000/= ilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za kawaida wakati Sh. 265,936,664,000/= ilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Tatizo kubwa katika ruzuku ya Serikali ni ukweli usiyopingika kwamba ruzuku hii haipelekwi kwa wakati kwenye Halmashauri husika. Hivyo, kutokupeleka fedha kwa wakati kunachochaea udhaifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati muafaka. Kamati imebaini kuwa Halmashauri hazikupokea fedha kulingana na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado kuna ubadhirifu, ujisadi na utovu wa nidhamu wa hali ya juu wa matumizi ya fedha za umma na hii inatokana na Wizara husika (*TAMISEMI*) kutosimamia kwa karibu au yenye kuhusika moja kwa moja na ujisadi huu. Ukosefu wa nidhamu ya matumizi ya fedha pia unajidhishirisha katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, mwaka 2011/2012 jumla ya kiasi cha Sh. 1,688,848,579 katika Halmashauri 38 kilitumika nje ya Bajeti iliyoidhinishwa bila kibali kutoka mamlaka husika kinyume na kifungu 10(3)cha Sheria ya fedha Na. 9 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 iliyorekebishwa 2001. Pia jumla ya Sh. 2,673,964,170/= zilizohamishwa kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine na hazikuweza kurejeshwa katika Akaunti husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Halmashauri Kujiendesha kwa kutumia fedha za ndani. Pamoja na kwamba Serikali za Mitaa ni mamlaka zenyе mipaka kamili, rasilimali, uongozi na watu, uwezo wao wa kujitegemea hauna dalili zozote za kuisaidia Serikali Kuu kujinasua kutoka katika makucha ya utegemezi kwa Wahisani.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umebaini kuwa ni Halmashauri chache sana zinazokusanya mapato yake ya ndani kwa kiwango cha uwezo wake wa ukusanyaji. Mfano, Halmashauri ya jiji la Tanga ambao walijipangia kukusanya Shilingi bilioni sita kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo na badala yake wakakusanya sh bilioni tatu tu.

Aidha, hakuna Halmashauri hata moja inayokusanya mapato yake ya ndani kwa kiwango cha kujiwezesha kujitegemea.

Baada ya Ukaguzi, katika eneo hili Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(a) Halmashauri zitengeneze mipango mahususi ya uwekezaji/kuongeza uwezo wa kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali;

(b) Watumie fursa za kisheria kutengeneza Sheria ndogo za Halmashauri kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato na kuongeza *property tax, service levy*, minara ya simu, viwanda, migodi, mabango ya matangazo, na Maeneo yenye vyanzo vya uzalishaji wa umeme;

(c) Wizara iharakishe kuitisha haraka sheria ndogo zinapopelekwa kwake na Halmashauri husika; na

(d) Pawepo na mkakati wa udhibiti wa makusanyo ya fedha za Halmashauri kutoka kwa Mawakala ili Kuongeza Uwezo wa Halmashauri Kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, hakuna Halmashauri hata moja yenye uwezo wa kujitegemea unaozidi 10% ya jumla ya mapato yake yote ya mwaka. Hii ina maana kuwa kiasi cha utegemezi wa kifedha wa Serikali za Mitaa kwa Serikali kuu ni zaidi ya 90%. Mfano makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yalikuwa Shilingi bilioni 236.7 wakati matumizi halisi ya Halmashauri hizo yalikuwa Shilingi trillioni 2.277. Hiki ni kiwango kikubwa cha utegemezi.

***Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)***  
*[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAAJ]*

Rejea ya nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja matokeo ya mahojiano baina ya Kamati na Halmashauri mbalimbali vinaonesha kuwa sababu kubwa za udhaifu huu ziko mikononi mwa Serikali yenyewe. Kikubwa ni udhaifu wa Serikali za Mitaa katika kukusanya mapato na kudhibiti upotevu wa mapato hayo. Kwa mfano:-

(a) Idadi ya Vitabu vya kukusanya mapato ambavyo Mawakala wa ukusanyaji wa mapato hawakuvirejesha/ hawavirejeshi katika Halmashauri husika na imekuwa ikiongezeka. Hii inaweza kutafsiriwa kwamba upotevu wa mapato yanayokusanya unazidi kukua ambapo katika mwaka 2011/2012 vitabu 2,990 vya makusanyo kutoka jumla ya Halmashauri 36 tu hapa nchini havikuwasilishwa kwa Ukaguzi, kama inavyoonekana katika Kiambatisho ambacho kiko hapo chini.

**Jedwali Na 1. Mwelekeo unaoonesha vitabu ambavyo  
havikuwasilishwa kwa ukaguzi**

Mwaka	Idadi ya vitabu vivilyo kosekana	Idadi ya Halmashauri
2007/2008	860	43
2008/2009	1341	50
2009/2010	948	48
2010/2011	682	36
2011/2012	2990	36

**Chanzo:** Uchambuzi wa LAAC katika Taarifa za NAOT kwa Miaka iliyooneshwa.

(b) Kiasi cha maduhuli yasiyowasilishwa na Mawakala wa Ukusanyaji wa mapato kinazidi kuongezeka. Hii ikiwa na maana kuwa mapato yapo na yanakusanya ila kwa kiasi fulani yanaishia mifukoni mwa wajanja wachache. Kwa mfano, ukaguzi uliofanywa 2011/2012 katika jumla ya Halmashauri 56 kama zinavyoonyeshwa katika kiambatisho ambacho nimeoneshwa hapo chini, ulibaini kuwa, kiasi cha Sh. 4,466,028,478/= hakikuwasilishwa kwa watunza fedha japo kilikusanya. Rejea Jedwali lifuatalo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

### **Jedwali Na 2. Muhtasari wa Maduhuli ambayo hayajawasilishwa na mawakala**

Mwaka	Maduhuli yasiyowasilishwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri Husika
2007/08	421,213,641	22
2008/09	1,095,113,399	43
2009/10	2,756,763,702	43
2010/11	4,360,299,618	48
2011/12	4,466,028,478	56

**Chanzo:** Uchambuzi wa LAAC katika Taarifa Mbalimbali za NAOTkwa Miaka iliooneshwa.

### **Jedwali Na 3. Mwelekeo wa masurufu ambayo hayakurejeshwa**

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri husika
2007/2008	214,489,665	18
2008/2009	14,983,300	4
2009/2010	1,574,632,616	72
2010/2011	984,955,534	34
2011/2012	1,999,406,423	70

**Chanzo:** Uchambuzi wa LAAC katika Taarifa Mbalimbali za NAOTkwa Miaka iliooneshwa.

(c) Kusuasua na uwajibikaji usiyordhisha wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya TAMISEMI katika kupitisha Sheria Ndogo za Halmashauri hususan Sheria Ndogo zinazohusu uibuaji wa vyanzo vipyta vya mapato. Yapo Malalamiko ya Halmashauri kadha wa kadha kwamba zimepeleka kwa muda mrefu TAMISEMI rasimu za Sheria Ndogo lakini mpaka sasa hazijapata majawabu. Aidha, sheria nyingi zinazotumika Halmashauri zimepitwa na wakati. Mfano, sheria zilizotungwa mwaka 1988 hazijaboreshwaa kulingana

***Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)***  
[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]  
na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi yaliopo sasa.  
(Makofii)

Maoni ya Kamati ni kwamba kusuasua kwa aina hii bila sababu za msingi kunazikwamisha Halmashauri katika kutekeleza mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mishahara kwa Watumishi hewa ni tatizo sugu. Mwenendo wa kitakwimu hauoneshi kama tatizo hili linaelekea kupungua. Matumizi mabaya ya fedha za umma kwa njia hii yanapaswa kudhibitiwa na kutokomeza kabisa kwani Waajiri wanao maafisa utumishi wanaoshughulika na taarifa za Waajiriwa wao. Takwimu zifuatazo kama zilivyooneeshwa katika nyaraka mbalimbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinathibitisha kuendelea kuwepo kwa ubadhirifu huu:-

Kamati inashauri kuwa malipo ya mishahara ya watumishi yafanyike kwa umakini mkubwa na Mfumo wa *Lawson* uharakishwe mara moja ili kuondoa tatizo hili sugu la Mishahara hewa.

Aidha, Kamati inaielekeza Serikali kwamba watumishi waliolipa na wale waliolipwa wakiwa wamestaafu wachukuliwe hatua stahiki.

Katikamwaka 2011/2012 jumla ya Sh. 693,132,772/= katika Halmashauri ya Wilaya tatu ilikuwa ni hewa.

**Jedwali Na 4. Mwenendo wa mishahara iliyolipwa kwa watumishi walitoroka, waliostaafu na waliofariki**

Mwaka	Mishahara iliyolipwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri Zilizohusika
2009/10	583,221,297	38
2010/11	961,394,959	36
2011/12	693,132,772	43

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, manunuzi yasiyo na nyaraka ya malipo yanaendelea kuongezeka kwa kasi ya kutisha na kuifanya Kamati iamini kwamba manunuzi haya ni ya udanganyifu au ubadhirifu katika matumizi ya fedha za umma.

Katika mwaka 2011/12 zaidi ya Shilingi bilioni 1.5 yalikuwa ni matumizi yasiyokuwa na hati za malipo.

### **Jedwali Na 5. Mwenendo wa Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa miaka mitano mfululizo**

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2007/08	1,370,245,729	45
2008/09	2,526,117,587	33
2009/10	2,830,338,208	34
2010/11	1,080,519,637	32
2011/12	1,509,529,810	22

Kumekuwepo na ongezeko la kiasi cha masurufu yasiyorejeshwa ambako pia kunaashiria uvujaji wa mapato. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Masurufu yenyeye thamani ya Sh 1,999,406,423/= yanayohusisha Halmashauri 70 yalikuwa hayajarejeshwa, kama inavyooneshwa katika kiambatisho C katika Taarifa hii.

Meshimiwa Spika, matatizo mengine sugu yenyeye kuchangia matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Halmashauri. Serikali kutuma fedha zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwenye mafungu ya Halmashauri (*excess vote*).

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na shughuli nyingine za kawaida katika Halmashauri, Kamati imebaini kwamba upo mtindo wa Serikali kutuma katika Halmashauri kiasi kikubwa cha fedha kuliko kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge katika fungu. Kwa mfano, jumla ya Sh. 2,016,312,633/=,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAAJ]*

zilitumiwa katika Halmashauri ya Jiji la Tanga Fungu 86 na Sh. 500,000,000/= zilitumiwa katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe, zaidi ya kiasi kilichokuwa kimeidhinishwa. Matokeo yake ni kwamba Halmashauri ilizitumia fedha hizo katika matumizi mengineyo bila kuzirejesha Hazina.

Kamati imebaini kuwa ni vitendo vya makusudi vyenye dhamira ovu kwa Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla. Kitendo hiki ambacho kinafanyika kwa ushirikiano wa hali ya juu baina ya Hazina, TAMISEMI na Halmashauri husika kunaashiria kuwepo kwa mtandao wa kutisha wa kifisadi baina ya Mamlaka hizo za Serikali. Aidha, fedha zinazopelekwa katika Halmashauri siyo halali, kwani hazijaidhinishwa na Bunge lako Tukufu ambalo hupitisha mafungu ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa yapo malalamiko yenye ushahidi na athari dhahiri kuhusu Serikali kutokupeleka fedha za maendeleo kwa wakati katika Halmashauri mbalimbali nchini. Yawezekana tatizo hili likawa linachangiwa na utegemezi wa Serikali yetu kwa Wahisani hasa pale Wahisani wanapochelewesha kutoa fedha. Hoja ni kwamba tatizo hili litaendelea mpaka lini kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini?

Mheshimiwa Spika, hapo awali taarifa imebainisha tatizo la kuzipelekea baadhi ya Halmashauri kiasi kikubwa cha fedha tofauti na kiasi halisi kilichoombwa. Lipo tatizo lingine la kuzipelekea Halmashauri kiasi kidogo cha fedha ikilinganishwa na kiasi halisi kilichoombwa ama kuidhinishwa. Madhara yake ni kwamba miradi husika hutekelezwa nusu nusu, chini ya viwango na nje na ratiba za utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba mwenendo wa utoaji wa fedha kwa utaratibu huu huchangia matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri kwani fedha zinapotolewa nusu nusu hufanya utekelezaji wa miradi kuwa wa kusuasua na chini ya viwango.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, Serikali kupeleka taarifa ya fedha isiyo ya kweli katika halmashauri. (*exchequer notifications*), Kamati imebaini kuibuka kwa tabia nyingine yenyе kutia shaka hasa katika miradi mingi ya barabara ambapo *Exchequer Notifications* hupelekewa Ofisi za Mikoa zikionesha kwamba fedha za barabara tayari zimekwisha kutumwa katika Halmashauri husika. Halmashauri hujianaa kwa ajili ya kuzitumia fedha hizo, lakini kiuhalisia ni kwamba fedha hizo hazifiki Halmashauri husika. Kwa uchache, Halmashauri zilizokumbwa na kadhia hii ni zifuatazo:-

Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, Karagwe, Pangani, Kilindi, na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watuhumiwa wa ufisadi kuhamishwa vituo vya kazi. Suala la Watumishi wanaotuhumiwa kufanya ubadhirifu katika Halmashauri moja kisha kuhamishwa haraka vituo vyengine na baadhi yao TAMISEMI kuthubutu kuwapandisha vyeo limeendelea kuwa sugu na linaitia shaka Kamati. Pamoja na Wizara kujitetea mara kadhaa kwamba jambo hili halifanyiki, hali ni tofauti sana na ilivyo, kitu kinachoifanya Kamati iamini kwamba Wizara husika kwa maana ya TAMISEMI inalegalega na ulegevu huu unajidhihirisha katika Halmashauri chache zifuatazo: Kwa mfano, Mwanza, Mvomero, Kishapu, Kilindi, Bagamoyo, Same na Masasi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Serikali (TAMISEMI) imekuwa ikitumia mtindo huu kuwalinda Watumishi mafisadi ndani ya Halmashauri na kuifanya Kamati iamini kuwa TAMISEMI ni sehemu ya ufisadi huu na kwa makusudi mazima, imekuwa ikieneza saratani hiyo kwenye Halmashauri nyingi iwezekanavyo. Kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali kuachana na mtindo huu wa kuwahamisha Watumishi hao wanaotuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, kutopelekwa kwa 20% ya ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa na 10% ya mfuko wa akina mama na vikundi vya vijana. Baada ya ukaguzi wa hesabu na miradi ya maendeleo katika Halmashauri

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAAJ]

mbalimbali zilizotembelewa na kukaguliwa, Kamati imebaini kuwa fedha hizi ambazo zinatakiwa kupelekwa kwa mujibu wa sheria na taratibu, hazipelekwi Vijijiini, kwa akina mama na vijana, hivyo kukwamisha maendeleo katika vijiji na kwa makundi haya.

Mheshimiwa Spika, pesa za mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo (*CDCF*) upo kwa mujibu wa Sheria Na.16 ya mwaka 2009 kwa ajili ya miradi ya Maendeleo Majimboni. Kamati imebaini kuwa kwa mwaka 2011/2012, kiasi cha Sh. 2,561,822,820/= hazikutumika na zilibaki katika akaunti za Halmashauri ambazo jumla yake ni 69. Hii inasababishwa na usimamizi hafifu wa Menejimenti unaofanywa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo.

Aidha, kushindwa kutumia fedha hizo, kunachelewesha jamii kunufalka na mfuko na hivyo malengo yaliyokusudiwa kutotimia.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu kwamba mara baada ya Kamati kuwasilisha maoni na mapendekezo yake Bungeni, Serikali hupaswa kujibu hoja hizo kwa maandishi (*Treasury Notes*). Inasikitisha kuona kwamba utaratibu huu hautekelezwi na Serikali. Mnamo tarehe 14 Aprili, 2012, LAAC iliwasilisha Bungeni Taarifa yenye Mapendekezo 14. Mapendekezo yote haya hayajawahi kupata majibu ya Serikali hadi leo hii.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba, matatizo sugu yote yaliyoibuliwa na Kamati katika Taarifa hiyo ni kweli kabisa na Serikali haina cha kujibu zaidi ya kukaa kimya kukiri udhaifu wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kuwasilisha mambo muhimu yaliyotokana na matokeo ya ukaguzi wa Kamati wa Hesabu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2011/2012 kwa hesabu za mamlaka ya Serikali za Mitaa katika sura zilizotangulia, sasa Kamati inakuja na mapendekezo ambayo kama yatakelezwa, yataimarisha usimamizi wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

fedha katika uendeshaji wa Halmashauri nchini ambako ndiko fedha nyingi za Umma hupelekwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini kuwa miradi mingi ya maendeleo hususan ile ya maendeleo inayopatiwa fedha kutoka *LGCDG, Road found, RWSSP, MMAM, MMES* na *DADPs* inatekelezwa chini ya viwango na baadhi haileti tija kusudiwa. Kamati inapendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika usimamiaji na utekelezaji wa Sheria za Manunuzi ya Umma; zipo sheria nyingi na nzuri zinazotoa mwongozo katika manunuzi ya Umma, lakini sheria hizi zimekuwa hazifuatwi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Kamati ni kwamba, Sheria za Manunuzi ya Umma na kanuni zake zifuatwe na zizingatiwe ili kuwezesha Manunuzi yanayofanyika kuwa na tija kwa Watanzania. Kamati ya Ukaguzi ziimarishwe na ziwe zinawasilisha taarifa zake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika Usimamizi wa Miradi ya Kamati imebaini kuwa baadhi ya Wataalam hususan wahandisi, wameonekana kuwa mbali na miradi wanayoisimamia, hivyo kuifanya miradi mingi wanayoisimamia kutekelezwa chini ya kiwango na wakati mwingine kuwepo kwa miradi hewa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Kamati ni kwamba Wataalam hawa (wanaohusika na usimamizi wa miradi mabalimbali) wawe zaidi kwenye maeneo ya miradi inakotekelezwa na kuepukana na tabia ya kubaki maofisini tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa miradi mingi haiibuliwi na wananchi wenyewe hali inayosababisha miradi mingi kukwama wakati wa uendelezaji wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Kamati ni kwamba Miradi yote inayowahusu wananchi ni vyema washirikishwe

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Kiasi cha kutotia shaka ili iweze kuitunzwa na kuendelezwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na hali ya kutothaminiwa kwa michango inatolewa na wananchi wakati wa utekelezaji na Miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba ni muhimu michango inayotolewa na wananchi ioneshwe katika hesabu za Halmashuri husika. Kwa kufanya hivyo, kutawatia moyo wananchi, kuona michango yao inathaminiwa na hii itawatia moyo kuiona miradi hiyo ni ya kwao pia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo yaliyotolewa na *OWM-TAMISEMI* yaliyowataka Maafisa Masuuli wote kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa kufuata mfumo wa Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) na kuziwasilisha pamoja na hesabu za mwisho kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa madhumuni ya ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha, Halmashauri nyingi hazikutii maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika pendekezo la Kamati ni kwamba Maafisa Masuuli wote wanapaswa kuzingatia maelekezo yatakayowawezesha wakaguzi kukagua utendaji na utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa kipindi kinachokaguliwa na kuoanisha na taarifa nyngine za fedha; na kufanya ziara kwenye miradi husika ili kutathimini hali halisi ya miradi na mafanikio yaliyofikiwa. Hii itawasaidia Wakaguzi katika kutathimini uwepo wa thamani ya fedha katika miradi iliyotekelizwa na Halmashauri husika na kutoa taarifa juu ya matokeo ya tathmini hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu weledi wa Madiwani juu ya Usimamizi wa Shughuli mbalimbali katika Halmashauri. Kwa kuwa Halmashauri inatekeleza shughuli mbalimbali ambazo zinahusiana na taaluma tofauti tofauti, Kamati inapendekeza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

(a) Madiwani wajengewe uwezo ili wawe na weledi juu ya yale wanayoyasimamia katika Halmashauri zao;

(b) Maslahi na mazingira ya kazi yaboreshwe ili waweze kusimamia vyema fedha za Umma katika Halmashauri zao; na

(c) Pawepo na mpango mkakati wa kuwajengea uzalendi kwa Waheshimiwa Madiwani ambao ndio wasimamizi wakuu wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini udhaifu mwingi katika ukusanyaji wa mapato hasa kwa kutumia Mawakala. Kamati inapendekeza yafuatayo:-

Moja, mikataba kati ya Mawakala na Halmashauri iandaliwe kisheria kwa kumshirikisha Mwanasheria wa Halmashauri, sambamba na kulinda maslahi ya Halmashauri husika.

Pili, mipango sahihi na thabiti ifanywe kabla ya kufikia uamuzi juu ya kuvibinafsisha vyanzo vyta mapato kwa Mawakala pamoja na kuzingatia taratibu za kuwapata Mawakala wenye sifa.

Tatu, Waheshimiwa Mameya, Wenyekiti, Madiwani, na Watendaji wa Halmashauri wasiwe wenye kumiliki kampuni za kiwakala na ambazo huchukua kazi za Uwakala au Ukandarasi katika Halmashauri husika ili waweze kufuatilia na kusimamia vema utendaji wa Mawakala au Wakandarasi hao.

Nne, Halmashauri zifanye utafiti wa kina wa hali ya soko kwa ajili ya shughuli iliyotarajiwa sambamba na kufanya upembuzi yakinifu kwa kila chanzo cha mapato kama msingi wa kubinafisisha.

Tano, Halmashauri zianze taratibu za kutumia mashine za kieletroniki (*EFD*) zitolewazo na *TRA* kwa ajili ya kutoa risiti

***Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)***  
[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]  
za mapokezi ya fedha (hii itaondoa tatizo la upotevu wa  
vitabu vya risiti).

Sita, Halmashauri kupitia Maofisa Mipango wawe na mipango kabambe na endelevu kuibua vyanzo vipya ya mapato ikiwa ni pamoja na kodi za majengo, mabango, matangazo ya biashara, mirahaba na kodi za huduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usiri katika utowaji wa taarifa kwa Umma; kwa mujibu wa Sheria Na. 9 kifungu 49 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 na Sheria ya *Memorandum* ya fedha za Serikali za Mitaa (90), Halmashauri zinatakiwa kutangaza mapato na matumizi yake ya mwaka katika magazeti yanayosomwa nchini.

Kamati inapendekeza Taarifa hizo zitangazwe katika magazeti yanayopatikana eneo husika. Taarifa hizi ziwe katika lugha ya Kiswahili, pia ziambatanishwe na mambo ya msisitizo (*Emphasis of matters*).

Mheshimiwa Spika, kuna udhaifu mkubwa katika mfumo wa udhibiti wa ndani. Pamoja na juhudini zinazochukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), hata hivyo Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(a) Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kiimarishe na kiwe kinajitengemea;

(b) Kamati za Ukaguzi (*Audit committees*) zifanye Shughuli zake ipasavyo;

(c) Mifumo ya kubainisha viashiria vya wizi na ubadhilifu viimarishe ikiwa ni pamoja na kuimarishe mfumo Fungani wa Usimamizi wa Fedha (*IFMS*) *Epicor 9.05*, Lawson na Mfumo wa Usimamizi wa Mapato (*Revenue Management System*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya Halmashauri na kesi zilizoko mahakamani; kutopteka na kuongezeka kwa ukubwa wa madeni yanayodaiwa Halmashauri zetu ambayo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

kwa mwaka 2011/2012 yamefikia Sh. 62,192,991,408/= ukilinganisha na wadaiwa wa Halmashauri ambayo ni Sh. 48,443,176,126/= ambapo Halmashauri ya Manispaa ya llala ndiyo inayoongoza kwa kuwa na deni kubwa la Sh. 7,649,250,988/=.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Kamati ni kwamba madai yafanyiwe tathmini na yalipwe haraka iwezekanavyo, sambamba na wadaiwa kulipa ili kuepusha Halmashauri zetu kuwa na kesi nydingi Mahakamani. Kwa mfano, Halmashauri 18 za katи ya Halmashauri 134 zilizokaguliwa zimegubikwa na wimbi zito la kesi zilizoko Mahakamani zenye thamani ya Sh. 8,698,124,431/=.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu kwako kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa milongozo mbalimbali ya kusaldia ufanisi katika utendaji wa Kamati. Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa kutekeleza majukumu yao kwa ustadi mkubwa na kwa namna ambavyo wamenipa msaada moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndг. Theonest Ruhilabake ni Wasaidizi wao Ndг. Dickson M. Bisile, Ndigwako Mwaigaga, Chilemji Chipanda, Waziri Kizingiti na Evaristi Mtende kwa ufanuzi wa mambo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za kibunge kila tulipowahitaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watumishi wake kwa Taarifa za Ukaguzi zinazoisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Shukrani zaidi kwa nchi Wahisani wa Mfuko wa Maboresho katika matumizi ya fedha za Umma (PFMRP) kwa kutuwezesha kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri mbalimbali na kuifanya Kamati ione uhalisia wa kinachotendeka katika Halmashauri hizo, shukrani kwa Ofisi ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED - MWENYEKITI WA  
KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAAJ]*

Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Fedha (Hazina) kwa ushirikiano wao wakati wote wa Vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Taarifa hii imebainisha matatizo sugu yaliyobainika katika matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012. Dhidi ya matatizo hayo, mapendekezo kadhaa yametolewa kama suluhisho kwani Kanuni za Bunge zinaitaka Kamati kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa matatizo hayo. Ni vyema Serikali ikajipanga vyema kwa ajili ya kutekeleza ushauri huo bila ya kuhitaji msukumo wa kibunge. Kutowana na uchambuzi uliofanyika, ni vyema pia Halmashauri zikaitambua nafasi yao katika ujenzi wa uchumi na maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa heshimima na taadhima nakushukuru na naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kamati ya Bunge la Bajeti, kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge la bajeti pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kama inavyofahamika, Kamati hii ni mpya. Kamati hii ilianzishwa rasmi mwezi March, 2013 yaani mwaka huu, na kuanza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge. Katika kutekeleza majukumu yake katika kipindi hicho, Kamati imekutana na changamoto mbalimbali ambazo licha ya kuwepo kwake, hazikuzuia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, tofauti na ilivyo katika Mabunge mengine yaliyopo duniani ambayo yana utaratibu huu, Kamati hii imeanzishwa bila ya kuwepo kwa Ofisi ya Bajeti ya Bunge inayojitegemea kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Bajeti. Hivyo, ipo haja ya kuwa na Ofisi ya bajeti ambayo inajitegemea ambayo itakuwa na watumishi wa kada mbalimbali wenye ujuzi,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

weledi na uzoefu mpana katika masuala ya Bajeti, watakaoisaidia Kamati katika kufanya uchambuzi wa kina juu ya Bajeti ya Serikali. Ni matumaini ya Kamati hii kuwa Bunge litafanya kila lililo ndani ya uwezo wake ili kukamilisha mapema mchakato wa kuanzisha Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Shughuli za Kamati kipindi cha mwezi Februari hadi Desemba, 2013. Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Kanuni za Bunge pamoja na Sheria, kanuni na taratibu mbalimbali yazilizowekwa kupitia Sheria za Fedha na hivyo kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya fedha, kodi na mengine ambayo kwa ujumla yalilenga kusaidia Serikali kukusanya mapato yake yenze tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni baadhi ya kazi zilizotekeliza na Kamati ya Bajeti kwa kipindi cha kuanzia mwezi Februari hadi sasa:-

(a) Kutathimini na kuchambua makadiriao ya mapato ya matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;

(b) Kupitia na kujadili mpango wa maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2013/2014;

(c) Kupitia na kujadili mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa wa kipindi cha mwaka 2014/2015;

(d) Kufuatilia na kusimamia Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa vipindi mbalimbali vya robo ya mwaka;

(e) Kuchambua na kushauri kuhusu Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2013/2014 uliyowasilishwa Bungeni;

(f) Kuhudhuria mafunzo mbalimbali yenze lengo la kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kuwajengea uwezo na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

ujuzi wa kuchambua Sera ya Kodi na Sera za Fedha zilizopendekezwa na Serikali;

(g) Kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kukusanya mapato;

(h) Kujadili na kupitia mwongozo wa kutayarisha mpango wa Bajeti ya Serikali 2015/2014 na hatimaye kutoa maoni na ushauri; na

(i) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa shukrani kwa wadau wote waliotoa ushauri na maoni mbalimbali yaliyowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la taarifa hii ni kulitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya utekelezaji wa shughuli za Kamati katika kipindi hicho, naomba kuelezea shughuli za Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee kuhusu tathmini na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bajeti kumeliwezesha Bunge lako kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali pamoja na kulijengea Bunge lako uwezo wa kuchambua Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 na hivyo kujikita zaidi katika kuangalia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kutekeleza jukumu lake la kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, imefanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa ikiwa pamoja na kukutana na Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Bunge za kisekta ambao waliwasilisha mbele ya Kamati hoja zao za msingi zilizojitokeza wakati wa kupitisha bajeti za Wizara husika. Aidha, Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta zilizokuwa na hoja, walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa ufanuzi kuhusu hoja hizo. Kamati ilipata maoni yao kuhusu hoja hizo na kushauriana na Serikali na hatimaye kuoneza fedha kwenye baadhi ya mafungu kwa upande wa matumizi ya kawaida na matumizi ya Maendeleo katika Bajeti husika.

Mheshimiwa Spika, katika kila hatua, Kamati iliona busara kumshirikisha Waziri wa Fedha pamoja na wataalamu wake na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango katika kujadili na kushaurina kuhusu masuala mbalimbali yaliyohusu ugawaji wa fedha kwenye mafungu mbalimbali, hatua ambayo iliisaidia Kamati kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zinaonesha kuwa kazi hii ilifanyika kwa muda wa miezi miwili kuanzia tarehe 8 Aprili, 2013 hadi tarehe 26 Juni, 2013 na kuweza kupokea takribani hoja 71 kutoka katika Kamati za Kisekta 10. Kati ya hoja hizo, hoja 32 zilihusu maombi ya fedha za nyongeza kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha na hoja 39 zilihusu masuala mengine, kwa mfano maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013, maombi ya kubakiza yaani (*retention*) na malimbikizo ya madeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua hoja hizo na kupendekeza nyongeza ya fedha katika hoja za mafungu 13 na mafungu mawili yaliongezewa fedha na Bunge lako Tukufu bila maombi hayo kupitia katika Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya kuongeza fedha katika baadhi ya mafungu yalifikiwa baada ya uchambuzi, mijadala na mashauriano marefu kati ya Kamati ya Bajeti, Wenyeviti wa Kamati za Kisekta, Mawaziri pamoja na maoni na ushauri uliotolewa katika kipindi hicho na wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango. Takwimu zinaonesha kuwa, jumla ya fedha za nyongeza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

zilizoombwa wakati wa kupitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka huu ilikuwa ni Shilingi bilioni 654.21 na Bunge iliidhinisha rasmi fedha za nyongeza kwa mafungu sita kwa mchanganuo ufuatao:-

- (i) Fungu 49 - Wizara ya Maji Shilingi bilioni 184.5;
- (ii) Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi Shilingi bilioni 30;
- (iii) Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara Shilingi bilioni 30; na
- (iv) Fungu 96 - Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, Shilingi bilioni 9.

Aidha, mafungu yafuatayo yalidhinishiwa fedha na Bunge bila kupitia kwenye Kamati ya Bajeti, yaani Fungu 35 - Idara ya Kurugenzi ya Mashtaka, yaani Shilingi bilioni 10 na Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama Shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Spika, mbali ya fedha hizo za nyongeza ambazo zilitolewa taarifa Bungeni, yapo maombi mengine ya fedha za nyongeza kiasi cha Shilingi bilioni 370.71 yaliyordhiwa na Kamati na kuwasilishwa Serikalini kwa mashauriano na hatimaye Serikali ilikubali kutoa kiasi cha Shilingi bilioni 229.5 kwa mchanganuo ufuatao:-

- (1) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi Shilingi milioni 350;
- (2) Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika (ruzuku ya mbolea na mbegu bora) Shilingi bilioni 21.15;
- (3) Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake) Shilingi bilioni 2;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

- (4) Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini (Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini - REA) Shilingi bilioni 186; na
- (5) Fungu 99 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, kiasi cha fedha kilichoongezwa kilikuwa ni asilimia 78.42 ya fedha yote iliyopendekezwa kuongezwa. Mafanikio haya ni kielelezo kimojawapo cha umuhimu wa kuanzishwa kwa Kamati hii ya Bajeti na kuwa na utaratibu mpya wa kujadili na kuidhinisha bajeti ya Serikali kwa kuzingatia mzunguko mpya wa Bajeti ya Serikali, yaani (*New Budget Cycle*).

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba utaraibu huu ulikuwa mgeni kwa Kamati lakini kwa kupitia mlongozo mbalimbali kutoka kwako na busara za Kamati yenyewe, Kamati ilifanikiwa kutekeleza jukumu hili. Aidha, pamoja na kuwepo kwa changamoto mbalimbali wakati wa kutekeleza jukumu hili, changamoto hizo zimechukuliwa kama chachu katika kutekeleza jukumu hili wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2014/2015; mwezi Oktoba 2013, Kamati ya Bajeti ilikutana na Ofisi ya Rais - Tume ya Mpango na kupata fursa ya kupokea na kuchambua Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015 na hatimaye Bunge lako Tukufu lilijadili na kuidhinisha mapendekezo hayo. Ikumbukwe kwamba Mpango wa Maendeleo wa kila Mwaka ni mwendelezo wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012-2015/2016) ikiwa ni awamu ya kwanza ya Mpango Elekezi (*Roadmap*) wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025 kwa kipindi cha miaka 15 iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuwasilishwa kwa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo mbele ya Bunge

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Iako Tukufu ilikuwa ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa maoni na ushauri utakaosaidia Serikali kuboresha mapendelekezo hayo kabla ya kuandaa Mpango wenyewe wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Maoni ya Waheshimiwa Wabunge yatasaidia kuboresha mapendelekezo ya Mpango wa Maendeleo kabla ya kufanyiwa kazi na kuletwala tena Bungeni kuititia Kamati ya Bajeti mwezi Machi/Aprili mwaka ujao 2014 na hatimaye kuwasilishwa Bungeni rasmi asubuhi siku ya Bajeti ya Serikali itakaposomwa.

Hivyo, Kamati inawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kujadili na kutafakari kwa kina mapendelekezo yaliyowasilishwa na hatimaye kutoa ushauri kwa Serikali nini kifanyike katika maandalizi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji makini na kwa wakati wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, utafungua fursa za ukuaji wa uchumi na hivyo kuelekeza nguvu za kitaifa katika maeneo ambayo yatakuza viwango vyajumla na vya kisekta, kiuchumi na hatimaye kuendelea kupambana na changamoto kubwa za kupunguza umaskini wa mahitaji muhimu na ule wa kipato.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha hili, Kamati ilitoa maoni yake ya msingi takribani 17 na kuyawasilisha Serikalini kuititia Taarifa yake iliyosomwa hapa Bungeni tarehe 30 Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2013/2014; itakumbukwa kwamba tarehe 13 Juni, mwaka huu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwasilisha Bungeni Mapendelekezo ya Serikali kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/2014, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kuipa uwezo wa kupata mapato ya kugharamia bajeti yake kwa mwaka huu wa fedha.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha hili, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013/2014 pamoja na marekebisho yake kama ilivyobainishwa katika Jedwali la marekebisho, lengo lake likiwa ni kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, Sheria zilizofanyiwa marekebisho na maelezo ya ufanuzi yalitolewa kwenye Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 27 Juni, 2013.

- Marekebisho ya Sheria mbalimbali zilizoanzisha Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma sura 348 vinavyoweka sharti kwa mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye mfuko mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka.

- Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (Sura 147) iliyofanya marekebisho kadhaa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 katika kifungu namba 124 na Jedwali la Nne kwa kubadili tafsiri ya maneno "*telecommunication services*" ndani ya Sheria hii kwa lengo la kupanua wigo wa huduma za simu zitakazotozwa ushuru wa bidhaa.

- Marekebisho ya Viwango vya Kodi katika Mafuta iliyofanya marekebisho yafuatayo:-

- (i) Mafuta ya taa kutoka Sh. 400/= kwa lita hadi Sh. 475/= kwa lita;
- (ii) Mafuta ya Dizeli kutoka Sh. 530/= kwa lita hadi Sh. 490/= kwa lita; na
- (iii) Mafuta ya Petroli hayana ongezeko, hivyo inabakia kiasi cha Sh. 713/= kwa lita.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

- Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura 332) iliyoweka adhabu kwa wafanyabiashara na walipa kodi watakaokiuka kifungu cha 80A kilichoweka sharti la kutumia mashine za kielektroniki katika kutoa stakabadhi na kuhifadhi kumbukumbu za mauzo ya kila siku.

- Sheria ya Ubia Bainya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, (Sura ya 103) na Sheria ya Ununuzi wa Umma. (Namba 7 ya mwaka 2011), iliyofanyia marekebisho katika kifungu cha 15 kwenye Sheria ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili kuondoa sharti la ushindani kwa zabuni za miradi yote ya ubia iliyoibuliwa na Wazabuni wenyewe (*Unsolicited PPP Proposals*).

- Sheria ya Uwekezaji Tanzania (Sura ya 38) iliyofanyia marekebisho vifungu vya 19 na 20 vya Sheria ya Uwekezaji Tanzania (Sura 38).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo yake juu ya marekebisho yaliyofanyika katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka wa fedha 2013/2014 na yaliwasilishwa katika Bunge lako Tukufu kuititia taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu la utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kipindi cha robo mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2013 Kamati ya Bajeti ilipokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu kuhusu mapato na matumizi ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa. Bajeti ya mwaka 2013/2014 imekuwa bajeti ya kwanza kutekelezwa kwa kuzingatia mapendekezo ya Bunge ya kuwa na mzunguko mpya wa bajeti.

Nia ya mzunguko huu mpya wa bajeti ya Serikali ni kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa miradi ya maenddeleo, zinatolewa na zinaanza kutumika kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

kuzingatia mpango wa utekelezaji wa miradi husika. Aidha, nia ni kutoa fursa ya kushirikisha wadau wengi zaidi ili kutoa michango ya kuandaa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha robo mwaka; robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, inaonesha kuwa lengo la makusanyo ya fedha vyanzo mbalimbali halikufikiwa kwa kiasi cha asilimia 14.3. Kamati ilijulishwa kwamba katika robo hiyo ya kwanza ya mwaka 2013, jumla ya mapato yote yalifikia Shilingi bilioni 3,082.2, sawa na asilimia 85.7 ya makadirio ya Shilingi bilioni 3,998.5. Mapato yatokanayo na kodi yalikuwa Shilingi bilioni 2,082.5 ikilishwa na makisio ya Shilingi 2,492.3 sawa na upungufu wa asilimia 14.6. Kwa upande wa misaada na mikopo, Serikali ilipokea misaada ya jumla Shilingi bilioni 94.1 sawa na asilimia 32.4 ya makadirio ya Shilingi bilioni 291 yaliyotarajjiwa katika robo ya kwanza. Kati ya misaada hiyo, Shilingi bilioni 43.4 zilipokelewa kama misaada ya kibajeti na Shilingi bilioni 50.7 ni za miradi ya maendeleo. Mikopo ya masharti ya kibiashara katika kipindi hiki ilifikia Shilingi bilioni 118.6 kutoka Benki na Taasisi za kifedha kati ya ukomo, yaani *ceiling* ya Dola za Kimarekani milioni 700 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizi, ni wazi kwamba katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2013/2014 malengo ya makusanyo ya mapato kutoka vyanzo vyote hayakuweza kufikiwa kikamilifu.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, jumla ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo katika kipindi hiki kwa miradi inayosimamiwa na Serikali Kuu ilifikia kiasi cha Sh. 581,611,667,769/= sawa na asilimia 11 ya fedha zote za maendeleo katika mwaka huu. Kwa upande wa fedha za Mikoa, kiasi cha Sh. 115,196,413,727/= sawa na asilimia 17 tu ndizo zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upatinaji wa fedha katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha unatoa taswira ya hali ya bajeti ya Serikali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*  
itakavyokuwa. Hivyo, ipo changamoto kubwa katika utekelezaji wa malengo tuliojiwekea katika bajeti hususan kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi imetajwa kwenye Taarifa, sitaisoma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hali ya uchumi, taarifa za awali kuhusu Ukuaji wa Pato la Taifa zinonyesha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2013, Pato halisi la Taifa ilikuwa kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2012. Sekta zilizokuwa zilizokuwa na viwango vikubwa vyaa uakaji wa uchumi ni pamoja na usafiri na mawasiliano (18.4%); fedha (14.6%); na ujenzi (8.7%). Aidha kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2013/14, Maoteo yanaonyesha kwamba Pato la Taifa litafikia asilimia 7.0.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwenendo wa bei unaonyesha kwamba mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 13.5 Septemba, 2012 hadi kufikia wastani wa asilimia 6.1 Septemba 2013. Wastani wa mfumuko wa bei wa chakula ulishuka na kufikia asilimia 6.5 Septemba 2013 kutoka asilimia 16.8 Septemba 2012 kutohana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha jukumu la ufuatailiaji wa matumizi ya Serikali hasa kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa nyakati tofauti, wakati wa Vikao vya Kamati, Kamati ya Bajeti ilikutana na viongozi wa Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Nishati na Madini na kujadiliana nao kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha nusu ya mwaka huu wa fedha 2013/2014. Matokeo ya majadiliano hayo ni kama yafuatayo:-

(a) Wizara ya Maji (Fungu 69).

Mheshimiwa Spika, bado Wizara ya Maji inakabiliwa na changamoto kubwa katika kutekeleza miradi ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

maendeleo licha ya kuwa mojawapo ya Wizara iliyoombewa fedha za nyongeza kiasi cha Shilingi bilioni 184.5. Changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati. Mfano, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2013 Wizara ilipanga kutumia kiasi cha Shilingi bilioni 155.9 kwenye miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 86.4 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 69.5 ni fedha za nje.

Aidha, fedha kwa ajili ya robo ya kwanza ya mwaka zimepatikana robo yapili ya mwaka huu wa fedha 2013/2014, ambapo kiasi cha fedha kilichopatikana ni Shilingi bilioni 161.7, kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 86 ni fedha za ndani; na Shilingi bilioni 75.7 sawa na milioni 46.7 *USD* ni fedha za nje. Aidha, kwa upande wa fedha za matumizi mengineyo (*OC*), kiasi kilichopaswa kutolewa ni Shilingi bilioni 5.2 katika kipindi cha Julai-Oktoba 2013. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa ni Shilingi bilioni 2.6 sawa na asilimia 50 ya kiasi kilichopangwa kutumika.

(b) Wizara ya Kilimo (Fungu 24).

**SPIKA:** Naomba kidogo Mheshimiwa.

Naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) niongeze muda, kusudi msomaji huyu aweze kumaliza zile dakika zake 30. Nadhani tutaongeza kama dakika 10. Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGU YA BAJETI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya kilimo Chakula na Ushirika katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 ilitengewa jumla ya Sh. 394,502,630,000/= . Kati ya fedha hizo, Sh. 268,462,342,000/= ni fedha za matumizi ya kawaida na Sh. 81,040,288,000/= ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa kutoka Hazina hadi tarehe 15 Novemba, 2013 zilikuwa Sh. 127,958,147,640/= sawa na asilimia 48 ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yalikuwa Sh. 127,533,856,570/=

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

sawa na asilimia 99 ya fedha zilizotolewa. Kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizopokelewa hadi kufika tarehe 15 Novemba, 2013 ni Sh. 23,689,089,120/= sawa na asilimia 29.2 ya fedha iliyoidhinishwa. Matumizi yamekuwa madogo kutokana na fedha hizo kutolewa mwanzoni mwa mwezi wa Kumi na Moja.

(C) Wizara ya kwa upande wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, hali ni hiyo hiyo, lakini kwa upande wa fedha za maendeleo taarifa zinaonesha kuwa hadi Oktoba, 2013 jumla ya Sh. 37,223,289,194/= zilipokelewa toka Hazina hii ikiwa ni sawa na asilimia 34 ya bajeti ya matumizi ya kawaida yaani mishahara (Sh.5,988,979,470) na matumizi mengineyo (OC) (Sh. 31,234,309,724/=). Aidha, kwa upande wa fedha zilizopokelewa ni Sh. 311,732,745,000/= ikiwa ni fedha za ndani sawa na asilimia 42 ya bajeti ya fedha za ndani na asilimia 26 ya fedha yote ya maendeleo kwa bajeti ya mwaka huu. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. 97,350,000,000/= sawa na asilimia 31 ya fedha yote ya ndani ilipelekwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme vijijini na Sh. 63,000,000,000/= kwa mradi wa bomba la gesi la kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai - Novemba, 2013 Wizara imepokea Jumla ya Sh. 367,961,034,194/= sawa na asilimia 29 ya Bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Wizara hizi chache, hali inaonesha kuwa kwa ujumla hali halisi ya utoaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo kwa kuzingatia ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo, siyo ya kuridhisha. Aidha, kuongezeka kwa kasi ya matumizi ya kawaida ya Serikali kumekuwa ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti kwa upande wa miradi ya maendeleo ukizingatia kuwa fedha za makusanyo hugawanywa kulingana na matumizi ya wakati husika, hivyo hakuna uwiano sawia kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, Kamati imehudhuria katika mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujinoa na tutaendelea kufanya hivyo, ili kuiongezea uwezo wake wa kiutendaji, hasa ukizingatia kwamba ni Kamati mpya ambayo imepewa majukumu makubwa na Bunge lako Tukufu katika kushiriki katika mchakato wa bajeti kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Utaratibu wa kuwa na Kamati mahsus i kwa ajili ya Bajeti kama hii, siyo utaratibu mpya duniani, nia ni kulijengea Bunge uwezo wa kujadili masuala yanayohusu Bajeti ya Serikali na hivyo kuishauri Serikali ipasavyo.

Mabunge kadhaa yamekuwa na utaratibu huu na yamefanikiwa sana katika kuongeza ushirikishwaji katika mchakato wa bajeti lakini pia uwajibikaji katika utekelezaji wa Bajeti. Hivyo Bunge letu limebahatiika kuanzisha Kamati ya Bajeti wakati tunayo mifano mingi ya mabunge mengine ambayo yamefanikiwa sana katika kutumia utaratibu huu, na hivyo kuwa ni mifano ya kuigwa. Mfano mzuri ni kama Bunge la Uganda na Kenya yameweza kuwa na utaratibu kama huu na hivyo kuwa na Ofisi ya Bajeti ya Bunge ambayo inaratibu shughuli zote za sekretariati ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika nyakati tofauti, Kamati yako ya Bajeti imeshiriki katika semina na warsha mbalimbali kuweza kujinoa ndani na nje ya nchi, na tutaendelea kufanya hivyo, tunayaeleza hayo, ambazo zilitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati kuweza kupata elimu ya masuala ya utekelezaji wa shughuli za Kamati za Bajeti ikiwa pamoja na kupata uzoefu wa Mabunge ya kiafrika ambayo yanazo Kamati za Bajeti ama Kamati zenye majukumu yanayofanana na ya Kamati za Bajeti. Kwa mfano, Kamati imeweza kujifunza kutoka uzoefu wa nchi za Kenya na Uganda ambazo ambazo zimepiga hatua kubwa sana katika usimamizi wa bajeti ya Serikali kuititia Kamati ya Bajeti. Nchi nyingine ambazo zimebadilishana uzoefu na Bunge lako ni Zambia na Ghana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba katika semina na warsha hizo, ilionekana kwamba Kamati ya Bajeti ya Tanzania pamoja na upya wake imeanza vizuri katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

kutekeleza majukumu yake ukilinganisha na nchi ambazo tumezitembeala kama Ghana na Zambia. Aidha, kutokuwepo kwa Sheria mabsusi ya kusimamia masula ya bajeti (*Budget Act*) ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii pamoja na kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Aidha, ni muhimu kwa Kamati ya bajeti ikaongezewa wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kuwasaidia waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii iingizwe kwenye Hansard katika sura yake yote, kwa sababu ya muda. Nijielekeze sasa katika maeneo ambayo ni changamoto katika muda ambao umebakie.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ya kuanzisha Kamati ya bajeti ni kuongeza ushirikishwaji (*participation*) ya waheshimiwa wabunge na wadau wengine katika mchakato wa mzima wa bajeti ya Serikali. Kamati ya Bajeti imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa inashirikiana na wadau mbalimbali nchini na nje ya nchi katika kuhakikisha kuwa nchi inapata mapato ya kutosha bila kuathiri kipato cha walipa kodi hao. Katika kutekeleza hili, katika kipindi cha kuanzia Machi hadi Novemba, 2013 Kamati imefanya vikao na wadau mbalimbali kujadiliana kuhusu masuala la mbalimbali yaliyohusu bajeti, hasa katika upande wa mapato na matumizi ya Serikali. Kamati inapenda kuwatambua baadhi ya wadau hao katika makundi yao kama ifuatavyo:-

(1) Sekta binafsi chini ya umoja wao (*Tanzania Private sector Foundation*) ambao Kamati ilikutana nao mara kadhaa kupata maoni na ushauri wa sekta binafsi kuhusu hatua na utekelezaji wa kodi nchini;

(2) Umoja wa wamiliki wa malori nchini (*Tanzania Truck Owners Association*) ambao walishauriana na Kamati ni kwa namna gani Sekta ya Uchukuzi wa mizigo inaweza kuboreshwa ili kuiingizia nchi mapato zaidi ya haya yanayopatikana hivi sasa;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

(3) Shirikisho la watoa huduma za utalii nchini (*Tourism Confederation of Tanzania*) ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia Sekta ya Utalii;

(4) Umoja wa watoa huduma za simu nchini (*Mobile Operators Association of Tanzania*) ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia Sekta ya Mawasiliano;

(5) Umoja wa wenyewe mabenki nchini (*Bankers Association of Tanzania*) ambao walijadiliana na Kamati masuala kadhaa ya kibenki na namna bora ya Serikali kupata mapato ya Serikali kupitia njia mbalimbali za kibenki;

(6) Umoja wa watoa huduma za Bima nchini (*Tanzania Insurers Association*) ambao walishauriana na Kamati uwezekano wa kupanua huduma za Bima hususan katika shughuli za Bima ya uchimbaji wa gesi na madini; na

(7) (*Tanzania Chamber of Minerals and Energy*) ambao walishauriana na Kamati kuhusu kodi mbalimbali zinazotozwa kwa Kamapuni za Madini nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa nyakati tofauti, Kamati iliweza kukutana na wataalamu mbalimbali kwa lengo la kupata ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala mbalimbali ya kibajeti yanayohusu sekta mbalimbali.

Kutokana na ushauri wa wataalam hao Kamati imeweza kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi wa kuridhisha. Wataalam hao ni kutoka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango, Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato, Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*), Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Taasisi za Elimu ya Juu hususan Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na sekta binafsi. Kamati itaendelea kuwatumia wadau hawa na wengine wengi kwa lengo kuongeza uelewa na kupanua ushirikishwaji katika bajeti na kupelekea maamuzi yenye tija kwa Taifa kwa ujumla. Kwa namna ya pekee, Kamati itashirikisha pia Asasi za Kiraia (*Civil*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]  
Societies) kwa kuwa wamekuwa mstari wa mbele katika  
kufanya tathmini mbalimbali za kibajeti na maisha ya  
wananchi kwa ujumla.*

Mheshimiwa Spika, katika vikao nya Kamati Mwezi Novemba 2013 vilivyo fanyika Dar es Salaam, Kamati iliweza kupitia na Kujadili taarifa ya Serikali kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa mujibu wa taarifa, uandaaji wa mwongozo huu uliwashirikisha wadau wengi na maoni yao yamezingatiwa ipasavyo.

Aidha, mwongozo umezingatia pia vipaumbele nya mapendekozo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2014/2015 ambao ulijadiliwa kwa kina na Kamati hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge na kuhitimishwa tarehe 4 Novemba, 2013. Hivyo basi, maoni na ushauri ultiotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika mwongozo huu yana nafasi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mwongozo ujao pamoja na uandaaji wa bajeti za Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari mwongozo huu unatoa majukumu ya msingi ya kuzingatia katika kuandaa mipango na bajeti, ukusanyaji wa mapato ya Serikali, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, na mikakati ya kudhibiti ongezeko la madeni. Aidha, mwongozo huo umeelekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Waakala wa Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mfumo madhubuti ya ufuatilaji na tathmini ya matumizi ya fedha za umma na kuibua miradi itakayotekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP).

Vilevile mwongozo umebainisha malengo ya utekelezaji katika kipindi cha muda wa kati pamoja na maeneo ya kipaumbele yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa uandaaji wa mpango na bajeti ikiwa ni hatua mahsus ya utekelezaji wa FYDP I na MKUKUTA II kupitia mfumo wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]  
usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili kupata  
matokeo makubwa sasa (BRN).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuitia na kuujadili mwongozo huu, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo yake kwa kina hasa katika upande wa kuongeza wigo wa kukusanya kodi kwa kuzingatia ubunifu wa vyanzo vipyta vyta mapato, udhibiti wa matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima na ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufanya utafiti na uchambuzi wa Sera za Kodi, Sera za Fedha na Sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali, Kamati imejitahidi kutekeleza jukumu hili kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali wa masuala ya fedha na kodi ambao wameisaidia Kamati katika kutoa uelewa kuhusiana na masuala haya.

Mheshimiwa Spika, suala la kufanya utafiti na uchambuzi ni pana na linahitaji wataalam (*man power*) wa kutosha wenye taaluma na weledi wa masuala haya. Kama nilivytangulia kueleza hapo awali kuhusu changamoto zilizopo kwenye Kamati hii ni katika eneo hili pia. Hata hivyo utekelezaji wa jukumu hili ni endelevu na hauna budi kuwekewa mkazo ili kuiwezesha Kamati kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusiana na masuala ya fedha na kodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilifanya tathmini kadhaa ya kodi mbalimbali zilizopitishwa na Bunge lako katika mwaka huu wa fedha baada ya kupata maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Maeneo ambayo yalitolewa maoni na wadau wengi ni hasa katika eneo la kodi ya laini ya simu (*SIM Card Tax*) na ushuru katika hamisho la fedha kwa huduma za kibenki (*Excise Duty on Money Transfer*).

Kamati ilikutana na wadau husika kwa madhumuni ya kuwasikiliza. Kimsingi, Kamati ilielewa hoja zilizotolewa na wadau hao. Kwa kushirikiana na Serikali, Kamati iliangalia na kuishauri Serikali namna bora ya kuboresha ukusanyaji wa kodi hizo ikiwa ni pamoa na kukutana na wadau husika na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

kukubaliana namna bora ya kukusanya kodi hizo bila kuathiri mapato yaliyokadiriwa katika mwaka huu wa fedha. Pindi mashauriano yatakapokamiliwa, suala hili litaletwa katika Bunge lako kwa ajili ya maamuzi.

Aidha, Kamati imeendelea kushauriana na Serikali kuhusu maeneo mapya ya mapato ikiwa pamoja na kuangalia maeneo mapya yaliyopendekezwa kwenye Taarifa ya vyanzo vipyta vya mapato ya Serikali iliyofanyiwa utafiti chini ya Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Spika chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Andrew Chenge. Ni matumaini ya Kamati kwamba katika Muswada wa fedha wa mwaka ujao, Serikali itajumuisha vyanzo vingi vipyta vya mapato ili kupunguza utegemezi na pia kuwapunguzia mzigo wananchi wa kuongezewa viwango vya kodi mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2013/2014. Katika tathmini hiyo Kamati ilibaini masuala na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Ucheleweshaji wa kutolewa fedha na Hazina pamoja na upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, mfano mzuri ni kwa Wizara ya Maji na Kilimo.

(ii) Matumizi ya fedha zaidi ya ilivyoidhinishwa na Bunge kwenye baadhi ya vifungu hali inayopelekea vifungu vingine kukosa fedha za kutosha. Hali kadhalika utoaji wa fedha katika mafungu mbalimbali ultofautiana, mafungu mengine yakipata fedha zaidi ya zilizopangwa wakati mengine yakipata pungufu.

(iii) Kutozingatiwa kwa Sheria na Kanuni za fedha na hivyo baadhi ya vyanzo vya mapato havijaweza kukusanya kwa wakati. Mfano, kushindwa kwa Makampuni ya Simu na Taasisi za kifedha zikiwemo Benki kukusanya ushuru wa bidhaa kwa kadi ya simu (*SIM card levy*) na uhawilisho wa fedha (*money transfer*) kuwasilisha Serikalini. Kodi hizi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

zilitarajiwa kuingizia Serikali takribani mapato ya Shilingi bilioni 178 kwa kadi za simu na Shilingi bilioni 150 kwa huduma za kibenki. (*Money transfer*). Suala hili lipo Mahakamani. Hata hivyo, Kamati, Serikali pamoja na wadau wa mawasiliano walishaanza mazungumzo kuhusu namna ya kuboresha kodi hiyo.

(iv) Kuongezeka kwa Deni la Taifa na hivyo kutokuwa na uhalisia na Pato la Taifa. Kwa sasa Deni hili limeongezeka kwa asilimia 10 kutoka Dola za Marekani bilioni 13.9 mwezi Desemba, 2012 hadi Dola bilioni 15.29 mwezi Juni, 2013.

(v) Upungufu wa fedha zilizotengwa na Serikali pamoja na washirika wa maendeleo kwa utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mkakati wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa, utekelezaji wa miradi hilo unakadiriwa kugharimu kiasi cha Shilingi trilioni 17.3 katika kipindi cha miaka mitatu itakayofikia ukomo mwaka 2015/2016.

(vi) Urasimu mkubwa katika taratibu za manunuzi na uwezo mdogo wa wakandarasi wa ndani na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati. Mfano mzuri ni utekelezaji wa miradi ya maji kwa kila vijiji kumi kwa kila Halmashauri.

(vii) Serikali kutokuwa bunifu zaidi kwa vyanzo vypya vyta mapato na pia kutochukua uamuzi wa haraka kutumia vyanzo vypya vyta mapato vinavyopendekezwa na wadau wa masuala ya kodi.

(viii) Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Serikali kwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali.

(ix) Kutotolewa kwa wakati kitabu cha kwanza cha Bajeti kinachoonesha makadirio ya mapato ya Serikali (*Revenues estimates*) na hivyo kupelekea Waheshimiwa Wabunge kutotambua mapema vyanzo vypya vyta mapato.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

(x) Kutokuwepo kwa Ofisi ya Bajeti na Sheria ya Bajeti (*Budget Act*).

Mheshimiwa Spika, sasa nielezee maoni na ushauri wa jumla wa Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa bajeti ya Serikali unazingatia makusanyo ya siku kwa siku (*cash budget*), hata hivyo, bado kuna tatizo la kuongezeka kwa kasi matumizi ya kawaida ya Serikali na hivyo kuathiri ugharamiaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika utaratibu wa sasa, hakuna uwiano sawia kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupunguza matumizi yake na kuongeza ukusanyaji wa mapato ili tuweze kugharamia miradi ya maendeleo katika kiwango cha asilimia 35 ya bajeti ya Serikali kama mpango wa miaka mitano wa maendeleo unavyoolekeza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ili kuboresha shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti, Bunge lako lianzishe Ofisi mahsus ya Bajeti itakayokuwa na wataalamu wa kutosha pamoja na Sekretariati iliyopo kuweza kuisaidia Kamati kufanya chambuzi mbalimbali za kibajeti.

Aidha, Kamati inapendekeza Serikali iwasilishe Bungeni mapema iwezekanavyo Muswada wa Sheria itakayosimamia masuala ya Bajeti yaani (*The Buget Act*) ili kuweza kulipa Bunge lako Tukufu nguvu za kisheria katika kusimamia matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na ushiriki wa Bunge katika mchakato wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza na kuwashukuru wadau na Taasisi zote zilizokubali wito wa Kamati, ama zilizoomba kukutana na Kamati kwa madhumuni ya kujadiliana masuala mbalimbali ya kibajeti yenye lengo la kuijenga nchi yetu. Kamati inatoa wito kwa wadau wengi na wenyewe wajitokeze katika kufanikisha shughuli hii kukutana na Kamati ili kuweza kushauriana nao kuhusu masuala ya kibajeti. Hata hivyo, Kamati inatoa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

angalizo kuwa haitajishughulisha na maoni yenyе mlengo wa mtu binafsi ama Taasisi moja moja, bali yale ya makundi yenyе maslahi ya Taifa tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya mapato, Kamati inashauri Serikali iendele kuyafanyia kazi mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na Bunge lako Tukufu kuhusu vyanzo vipyा vya mapato. Ni vyema Serikali ikafanyia kazi taarifa za Kamati zinatolewa hapa Bungeni ambazo zimesheheni maoni na mapendekezo mahsusи ya vyanzo vipyा vya mapato yenyе lengo la kuhakikisha Serikali inapata mapato iliyojpangia. Aidha, kwa kutumia uwezo wake wa kitaalam, Serikali iendelée kutafuta na kuchambua vyanzo vipyा vya mapato ili kuongeza wigo wa kodi na hatimaye iweze kugharamia miradi yake ya maendeleo na kuweza kuikwamua nchi yetu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto ya ukomo wa ukopaji mikopo ya nje ya masharti ya kibiashara inayopelekea nchi kushindwa kukopa mikopo mikubwa ya kibiashara (*non-concessional loans*) kutokana na makubaliano yaliyopo kati ya Serikali yetu na Taasisi ya Kimataifa ya fedha, *IMF* pamoja Benki ya Dunia. Kwa sasa kiwango cha mikopo ya nje kinachoruhusiwa kwa mwaka ni kiasi kisichozidi Dola za Marekani milioni 700 (Shilingi bilioni 1,120) kwa *exchange rate* ya *jana*.

Kamati inapendekeza ukomo huu uangaliwe upya kwa lengo la kupandishwa ili Serikali iweze kukopa na kuwezesha kushughulikia eneo hili kwa kuipeleka mikopo hiyo katika miradi mikubwa ya maendeleo ya kimkakati kama vile ujenzi wa Reli ya Kati, Bandari ya Dar es Salaam na maeneo ya Tanga, Bandari ya Tanga na kadhalika. Kamati inashangazwa na kitendo cha Serikali kusit akukopa ndani ya ukomo huu kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi ambayo kwa sasa utekelezaji wake hasa kwenye miradi ya maendeleo imekuwa ikiongezea Serikali gharama kubwa ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

manunuzi ikilinganishwa na hali halisi ya soko. Hivyo, Serikali haipati thamani halisi kwa bidhaa na huduma kama inavyokusudiwa. Aidha, sheria hii imekuwa ni kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na huduma kwa vile mchakato wake una mlolongo mrefu.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa deni la Taifa siyo wa kuridhisha kutokana na kuongezeka kwa mikopo ya masharti ya kibiashara na malikimbikizo ya riba. Kamati inaishauri Serikali kutafuta namna bora ya kukabiliana na mwenendo wa madeni. Aidha, Kamati itapenda Bunge lako Tukufu kupewa takwimu zenyne mchanganuo unaoonesha kiasi tunachodaiwa, nani anadai kiasi gani, na fedha iliyokopwa ilitumika katika kugharamia nini. Hii itasaidia kupata ufahamu wa mwenendo wa deni hili.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli kwa Wizara na Idara ambazo zipo kwenye mfumo wa kubakiza (*Retention Scheme*) bado haujawa wa kuridhisha. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na baadhi ya Wizara zenyne maduhuli mengi kutokusanya kikamilifu, mfano Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Nishati na Madini, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina. Kamati inapendekeza Serikali kuhakikisha suala hili linatafutiwa ufumbuzi ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata mapato yake iliyojipangia.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) - Mheshimiwa Stephen Wasira kwa kushirikiana vyema na Kamati.

Namshukuru pia Waziri wa Fedha - Mheshimiwa William Mgimwa kwa ushirikiano anaoutoa kwa Kamati. Tunawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Tume ya Mipango pamoja na Taasisi mbalimbali za Fedha ambazo wamefanya kazi na Kamati hii katika kipindi hiki. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

napenda kuwashukuru wadau mbalimbali wa masuala ya biashara na kodi ambao walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni na ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge – Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Christina M. Lissu, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu; Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Mheshimiwa Ritha Mlaki, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa John Cheyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua pia nafasi hii kumshukuru pia Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa D. Mbise na Makatibu wa Kamati Ndugu Michael Kadebe, Ndugu Michael Chikokoto, Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Elihaika Mtui kwa kuihudumia vyema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tulikuwa tuisome na ile Kamati ya Tatu. Naona hawapo, wataisoma kesho. Turudipo kipindi cha jioni mtakuwa mnajadili hizi taarifa kwa pamoja. Upande wa Serikali kila Wizara ita-take note

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

katika maeneo yanayowahusu, kwa sababu tutatoa muda na nyinyi ku-react.

Waheshimiwa Wabunge, mnaweza kujadili pale mnapotaka. Wenyewe watajua ni nani anayehusika na suala hilo.

Hata hivyo, pale kwenye *Speakers Gallery*kuna Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - Ndugu Benjamin Mashauri akiwa na Wasaidizi wake. Karibuni sana, tunajua hii kazi tunayoifanya hapa kwa msingi mkubwa inatoka na kazi mnazozifanya nyinyi. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge sina tangazo linguine, nasitisha shughuli mpaka Saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.08 Mchana Bunge ilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, mmaruhusiwa kuchangia mahali popote mnapotaka na sasa nitamwita Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa mara ya kwanza katika taarifa za Kamati hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kusimama na kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Hama tu hapo!

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba mimi ni Mjumbe katika Kamati ya LAAC na taarifa ambayo imesomwa na Mwenyekiti wetu mimi nimeshiriki na nimeshiriki katika majadiliano mbalimbali na Halmashauri zetu hapa nchini. Katika kukagua mapato na matumizi ya Halmashauri katika nchi yetu, tumegundua mambo kadha wa kadha ambayo yanafanya maendeleo yasifike kwa haraka kwa wananchi aidha, kutokana na ufujaji wa fedha za Halmashauri au fedha kutofika kwa wakati katika Halmashauri zetu au watumishi kutowajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tulipotembelea Halmashauri mbalimbali, tulikuta miradi mingi imesimama kwa ajili ya ukosefu wa fedha na tukakuta kwamba fedha nyingi zinakwenda kwenye Halmashauri mwisho wa mwaka, mwezi wa Sita au mwezi wa Tano mwishoni na hii husababisha Halmashauri nyingi kutotekeleza miradi yake ipasavyo. Lakini kama alivyosema Mwenyekiti wetu, Maafisa Mipango hawapo karibu na miradi hiyo husika.

Utaona katika taarifa ya CAG, ruzuku ya miradi ya maedeleo iliyopelekwa katika Halmashauri zetu ni Shilingi bilioni 535.017 lakini fedha zilizotumika ni 65% tu na 35% ya fedha hizo hazikutumika. Hazikutumika kwa sababu gani? Wengine walituambia kwamba fedha zimechelewa kupelekwa, wengine walikuwa hawana utaratibu mzuri wa kutumia hizo fedha, kwa hiyo, wananchi wakakosa huduma kutokana na fedha hizo kutotumika lakini faida ya miradi hiyo pia haionekani kwa haraka.

Tulikwenda Tabora tukakuta Zahanati imesimama pale, imejengwa chini ya kiwango, lakini tukaona kwamba ni Watumishi wa Halmashauri hawawajibiki ipasavyo, hawatembelei miradi kwa wakati. Miradi ile imeachwa mikononi mwa wananchi katika vijiji ili wao ndio wazisimamie. Wale wananchi hawana utaalamu wowote wa kusimamia miradi, kwa hiyo miradi inakwenda kwa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya CAG kuna fedha za MMAMShilingi bilioini 2.586, hizi fedha hazijatumika.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. FELISTER A. BURA]

Lakini hizi fedha zingejenga Zahanati, wanawake na watoto wakabitibwa jirani kuliko wanavyokwenda mbali. Hizi fedha hazikutumika mpaka mwaka unakwisha. Hakuna thamani ya fedha kama fedha hazitumiki kwa wakati. Pia tuliona kuna maduhuli ambayo yanakusanywa na mawakala katika Halmashauri zetu, lakini maduhuri haya hayapelekwi kwenye Halmashauri zetu. Shilingi bilioni 4.466 zilikusanywa na mawakala, fedha ambazo ni karibu bajeti ya Wizara moja katika Serikali yetu, lakini fedha hizi zimeliwa na wajanja.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano tu, katika Jiji la Dar es Salaam, Shilingi bilioni 1.548 zilikusanywa lakini hazikufika Halmashauri. Kule Meatu Shilingi bilioni 1.313 zilikusanywa na mawakala lakini hazikufika Halmashauri. Twende Mbarali, Sh.150,900,000/= zilikusanywa lakini hazikufika kwenye Halmashauri. Sengerema Shilingi milioni 158, Halmashauri 56 mawakala walikusanya fedha lakini fedha hizi hazikufika Halmashauri.

Hebu fikiria, Shilingi bilioni 4.4 zingekwenda kuwashudumia wananchi, ni wananchi wangapi wangefaidika na hizi fedha? Lakini kwa sababu baadhi ya watumishi wa Halmashauri zetu wanaingia mikataba isiyoeleweka na mawakala na hata mawakala wanapoacha kutimiza wajibu wao, hawashtakiwi, hakuna hatua za kisheria zinazochukuliwa dhidi yao. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Halmashauri wanachofanya ni kusitisha mkataba na kutafuta wakala mwingine ili aendeleee na ukusanyaji. Matokeo yake Serikali inapoteza fedha nyingi mno na kutokana na taarifa ya CAG Serikali yetu ni tajiri sana! Kama kweli Shilingi bilioni 4.4 hazikusanywi na bado tunasema Serikali haina fedha, siyo kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulipotembelea Halmashauri hizi, tulikuwa Maafisa Wakuu wa Idara mbalimbali wengi wanakaimu na wengine wameshakaimu miaka mitatu, miwili na hata mitano na hawana maamuzi na nafasi wanazokaimu, hawajui kama watapata nafasi hizo wala hawajui kama wataondolewa. Kwa hiyo, hii inaondoa *morale*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. FELISTER A. BURA]*

ya watumishi katika maeneo yao. Kama hawafai, basi watolewe wapelekwe wengine, kama hawana sifa, basi watolewe wawekwe wengine.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda Tabora, tukakuta *DT* ana matatizo na Afisa Mipango lakini wakasimamishwa na Baraza la Madiwani na baada ya kusimamishwa na Baraza la Madiwani *wali-appeal* kule Utumishi. *Walipo-appeal* Utumishi wakawarudisha Tabora. Wakati wanarudishwa Tabora, TAMISEMI walishampeleka *DT*na Afisa Mipango. Sasa nani acae ofisini? Wale waliokataliwa na Madiwani au hawa waliopelekwa na TAMISEMI? Mkanganyiko huo unafanya utendaji kazi usiwe mzuri.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kingine ambacho tumekikuta TAMISEMI, kwamba wanaofanya ubadhirifu katika maeneo fulani katika Halmashauri, wanahamishwa. Kule Mbarali tulikuta kesi ya Shilingi milioni 800. Katika zile Shilingi milioni 800 *cheque* 20 ziliandikwa kwa siku na zile Shilingi milioni 28 zikatoka, lakini yule bwana hakusimamishwa kazi, aliondolewa tu akapelekwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda pia Mvomero, tukakuta nyumba moja ya Mkurugenzi ilijengwa kwa Shilingi milioni 400. Tulipowauliza maafisa wa *National Housing* wanaojenga Mvomero nyumba za watumishi wakasema kwamba Shilingi milioni 400 kwa nyumba moja, wao wangejenga nyumba 10. Sasa tuone ubadhirifu huo unavyodidimiza Serikali yetu na unavyodidimiza maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Lakini huyo aliyefanya hivyo Mvomero tunaambiwa alihamishwa na Mhasibu aliyekuwa pale alihamishwa, mpaka sasa hatujui ni hatua zippi zilizochukuliwa dhidi ya hao wanaotenda ubadhirifu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mishahara inayolipwa kwa watu ambao hawapo kazini na mishahara ile hairejeshwi. Halmashauri kuna Wahasibu, kuna Maafisa Utumishi, lakini kuna watu ambao wanalipwa mishahara wengine walishakufa, wengine walishaacha kazi na wengine walishastaifu na wengine hawajulikani walipo, lakini fedha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. FELISTER A. BURA]

zao zinalipwa na ukiangalia Halmashauri 43 zilipatikana na hatia hiyo ya kutorejesha mishahara isiyo na wenyewe Hazina na Shilingi bilioni 1.5; ndiyo maana nasema Serikali yetu ina pesa lakini kwa sababu hizi fedha hazitumiki inavyotakiwa ndiyo maana tunaonekana kwamba hatuna fedha za miradi na kadhalika. Lakini, hivi Shilingi bilioni 1.5 zingekwenda kwenye miradi ya maendeleo si zingefanya kazi nzuri tu? Kuna udhaifu sana katika udhibiti wa fedha za Serikali.

Pia tulikuta kuna tatizo kubwa la raslimaliwatu. Ukitaka utendaji wa ufanisi katika Halmashauri zetu, ni lazima tuwe na watumishi wa kutosha, lakini Halmashauri 15 ambazo zimetolewa mfano hakuna watumishi 14,663. Nitoe mfano kwa Halmashauri yangu ya Kondoa; Kondoa ina upungufu wa watumishi 1,032, tunategemea wananchi watahudumiwa na nani? Tunategemea huduma nzuri kutoka kwa nani? Wakati watu 1,032 hawapo na nafasi zipo tupu. Mpwapwa watu 590, Sikonge watu 710, Namtumbo 945, nimetoa mfano tu! Raslimali watu katika Halmashauri zetu ni tatizo, lakini hasa Watendaji wa Vijiji ambao Halmashauri hawana namna ya kuwaajiri, ajira mpaka itoke Tume ya Utumishi, ni lini hawa watakapoajiriwa jamani ili nafasi hizi zizibwe watu wafanye kazi?

Nzungumzie tatizo la Mfuko wa Wanawake na Vijana. Serikali inapeleka fedha nyangi katika Halmashauri zetu kwa ajili ya kuwakopesha wanawake na vijana ili waweze kuwa wajasiriamali, lakini nikwambie fedha hizi haziendi. Tumekagua Halmashauri nyangi, kama Halmashauri 10 unaweza ukakuta ni Halmashauri mbili tu zinazopeleka fedha kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Watoto. Lakini kuna 20% ya ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato. Asilimia hii 20 pia haiendi. Ni tatizo kubwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri zetu pia kuna matatizo makubwa ya malipo ya nyaraka pungufu, wewe umemlipa mtumishi CAG akija kukagua hakuna nyaraka. Ni kauli ambayo haieleweki, kwa sababu tunaamini wanaofanya kazi katika Halmashauri zetu ni watu waliosoma na ni watu wenye uelewa mkubwa. Katika Halmashauri zetu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. FELISTER A. BURAJ]

zilizokaguliwa Halmashauri 74 walikuwa na nyaraka pungufu za malipo zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.367, fedha hizi zingetumika vizuri tungefika mbali.

Nitoe mfano wa Wilaya chache, Kigoma kuna fedha Shilingi milioni 425 nyaraka hazikuonekana kwa CAG. Rungwe Shilingi milioni 335 nyaraka hazikuonekana kwa CAG. Ilala Shilingi 304 milioni nyaraka hazikuonekana kwa CAG. Kama wametumia ipasavyo nyaraka wamepeleka wapi? Lakini kuna malipo ya nyaraka yasiyo na hati za malipo, watu wamelipwa, lakini hati za malipo hakuna.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono taarifa hii. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nami nitamke au ni-*declare interest* kwamba na mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC na nilishiriki kikiamilifu katika kuandaa taarifa ya Kamati. Kwa nafasi yangu kama Mjumbe wa Kamati na kama Mwenyekiti wa Kamati nilipata fursa pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati kupita kwenye Halmashauri kadhaa kufanya ukaguzi uliotokana na taarifa ya CAG. Mengi tumeyaona na kuyabaini lakini cha msingi mimi kwa mtazamo wangu, la muhimu zaidi ni kwamba tumebainisha changamoto kadhaa. Sasa nini kifanyike ili iwe suluhisho la changamoto hizo na tuweze kusonga mbele? Kwa hiyo, mchango wangu kwa kiasi kikubwa utajikita katika mapendekezo ya mambo gani ambayo nayaona yatakuwa kama suluhisho ili kupata ufumbuzi wa changamoto tulizoziona na hatimaye tuweze kusonga mbele katika eneo hilo la Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza, baada ya kuzunguka katika Halmashauri kadhaa, nimebaini kwamba kuna tatizo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SELEMANI J. ZEDIJ]

kubwa la Mabaraza ya Madiwani, aidha kutojua mamlaka yao au kama mamlaka yao yanajulikana, basi kutoweza kuyatekeleza kwa mujibu wa namna ambavyo Sheria inawapa mamlaka hayo. Nitatoa mifano, Baraza la Madiwani la Halmashauri ndiyo chombo cha nidhamu au mamlaka ya nidhamu *disciplinary authority* ya Wakuu wote wa Idara katika Halmashauri husika ukimwondoa Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, sasa tumekwenda kwenye Halmashauri kadhaa, nitatoa mfano wa Halmashauri ya Masasi. Tumekwenda pale unakuta Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa mfano, analalamika kwamba wana matatizo makubwa na Afisa Kilimo wa Halmashauri. Utendaji wa Afisa Kilimo wa Halmashauri hauridhishi, uko chini ya kiwango, anawaletea matatizo makubwa, kwa hiyo, anaomba Kamati ya *LAAC* tumsaidie.

Sasa mimi *openly* katika maeneo kama haya, nilikuwa natoa majibu ambayo yatasaidia kutoa elimu kwa wale ambao wanapaswa kuchukua hatua. Kwa mfano, nilimwambia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Masasi kwamba wewe ndiyo Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ndicho mamlaka ya nidhamu ambayo unaweza kumchukulia hatua Afisa Kilimo kama mmethibitisha kwamba uwezo wake uko chini ya kiwango. Nilimwambia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Masasi kwamba usitegemee labda Kamati ya *LAAC* au Waziri aje hapa Masasi ndiyo achukue hatua kwa Afisa Kilimo. Wewe ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani, ndiye *disciplinary authority* na hawa Wakuu wa Idara wote wako chini yenu na mnatakiwa kuchukua hatua za kinidhamu pale ambapo mnaona kwamba utendaji wao wa kazi uko chini ya kiwango ambacho kinakusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakuta kwamba Halmashauri nyingi zina matatizo kama haya. Wakuu wa Idara wanaboronga, Wakuu wa Idara wanafanya kazi chini ya viwango ambavyo vinatarajiwa lakini Mabaraza ya Madiwani hayachukui hatua.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. SELEMANI J. ZEDI]

Yapo maeneo mengine ambako Mabaraza ya Madiwani yanachukua hatua, lakini kwa kukosa mwongozo au kwa kukosa Elimu ya Sheria ya Utumishi wa Umma, unakuta wanakosea namba ya kuchukua hatua. Kwa hiyo, wanamsimamisha Mkuu wa Idara anakwenda ku-*appeal* kwenye Mahakama ya Kazi, Mahakama ya Kazi inalipitia shauri, baadaye inakuja na hukumu kwamba Baraza la Madiwani lilikosea katika taratibu za kumsimamisha kwa hiyo anarudishwa.

Utagundua pia kwamba, kuna tatizo kubwa la Mabaraza ya Madiwani kukosa elimu ya kutosha ya Sheria ya Utumishi wa Umma ili sasa wanapoamua kuchukua hatua, waweze kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ili Mkuu wa Idara ambaye ameboronga asichomoke, asikwepe kwa kupitia *loophole* ambazo zipo kwenye sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, rai yangu hapa ni kwamba, Mabaraza ya Madiwani wajue mamlaka walionayo, wajue nguvu za kisheria walizonazo na vilevile wapewe elimu ya kutosha ya namna ambavyo wanaweza waka-*apply* Sheria ya Utumishi wa Umma ili wanapoamua kuchukua hatua za kinidhamu juu ya Watumishi walio chini yao, wasichemke wasikosee na hatimaye kutoa mwanya kwa Watumishi wale ku-*appeal* halafu kurudishwa wakati kosa lipo dhahiri, lakini wanakuwa wamekosea tu namna ya kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ya kwanza ni hiyo kwamba, kuna tatizo kubwa sana la Mabaraza ya Madiwani kutojua wanachotakiwa kufanya au kutotekeleza kikamilifu yale ambayo yanatakiwa kufanywa.

Mheshimiwa Spika, lingine nililogundua ni kwamba, kuna jitihada ambazo zinafanyika, lakini naiomba Serikali jitahada hizi zifanyike kikamilifu na zifike mwisho. Kwa mfano, tumekuwa tukishuhudia matatizo katika Halmashauri nydingi ya Miradi hewa; fedha zinapelekwa katika Halmashauri husika labda za kujenga Mradi wa Josho la Kuogesha Mifugo au bwawa la umwagiliaji, lakini mwaka wa fedha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SELEMANI J. ZEDI]

unaisha, fedha zimeisha, josho halijajengwa na bwawa halijajengwa. Sasa kutokana na kanuni mpya za uendeshaji wa Serikali za Mitaa, kwa mfano, Halmashauri ya Nzega tumeshaanzisha kwamba, katika kila miezi mitatu ambapo Baraza la Madiwani linakaa, kila Diwani wa Kata husika anawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Kata yake husika.

Maana yake ni kwamba, jambo hili kama litatekelezwa kikamilifu kama ambavyo Halmashauri ya Nzega tumeanza, hakutakuwa na mwanya au uwezekano wa kuwa na Mradi hewa tena katika Kata fulani kwa sababu Mradi unatekelezwa ndani ya Kata husika. Sasa kama Diwani kila miezi mitatu katika Baraza la Madiwani anawasilisha Taarifa ya Miradi yake yote kwenye Kata yake, maana yake ni kwamba, kama katika Kata yake Mradi uliosemwa ni hewa haupo, utagundulika ndani ya miezi mitatu tu, tofauti na ilivyo kwamba mwaka mzima hakuna chochote kinachogundulika na mwisho wa siku mnakuja kugundua mwaka umeshapita au miaka miwili imepita na fedha zimekwenda.

Kanuni mpya za Uendeshaji wa Halmshauri zinazotaka kila kipindi cha miezi mitatu kila Diwani awasilishe Taarifa za Utekelezaji wa Miradi kwenye Kata yake, itasaidia sana kufichukua Miradi hewa na kuondoa kabisa uwezekano wa kuwepo kwa Miradi hewa. Kwa hiyo, hii ni *initiative* ya kupongezwa. Sisi Nzega tumeanza, Mabaraza mawili ya Madiwani yaliyopita, Madiwani wote wa Halmashauri ya Nzega waliwasilisha Miradi yao kwenye Kata husika na nadhani huu ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nizungumzie ni kuhusu Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Halmashauri zetu. Mkaguzi wa Nje (*CAG*), anakagua mara moja kwa mwaka, lakini ndani ya Halmashauri pale kuna Idara ya Ukaguzi wa Ndani ambayo inafanya ukaguzi kila siku na kila baada ya miezi mitatu wanatoa taarifa kwa Kamati ya Ukaguzi na wanatoa taarifa kwa Baraza la Madiwani la Kamati ya Fedha la Halmashauri husika.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. SELEMANI J. ZEDIJ]

Tatizo liliopo ni kwamba, Vitengo hivi *almost* kama havifanyi kazi kabisa, havina uwezo kabisa, bajeti ni ndogo mno, hawana magari, hawana kompyuta, hawana *resources*; na unakuta kwa mfano katika Halmashauri ya Nzega, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani bajeti yake kwa mwezi ni shilingi 1,500,000. Sasa unakuta Halmashauri ya Nzega bajeti yake ni bilioni 30. Sasa unakuta unakagua bilioni 30 kwa kutumia 1,500,000, *basically* ni kama ukaguzi hauwezekani. Wakaguzi wa Ndani wanakaa Ofisini tu wanafanya *voaching* wanakagua *vocha*, lakini hawawezi kwenda nje kwenye Miradi ili kukagua *value for money*, kuona majengo ya shule yanayojengwa kama yanajengwa kwa kiwango kinachotakiwa, hawawezi kwenda kuona majengo ya zahanati, hawawezi kwenda kuona madaraja, hawawezi kutoka maofisini kwa sababu bajeti yao ni ndogo mno. Kwa hiyo, rai yangu kwa Serikali hapa ni kwamba, Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ndiyo *key area* ambayo kwa kiwango kikubwa, itaweza kudhibiti ufujwaji wa fedha na kuweza kutuhakikishia *value for money* kwa maeneo mengi ambayo tunayatarajia.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Halmashauri nydingi zimeanza kutumia Mfumo wa Kihasibu, Mfumo wa Malipo ambaao unaitwa EPICAR Version 9.5. *Basically* mfumo kama mfumo hauna shida yoyote, mimi kwa mtazamo wangu naona una faida nydingi. Kwa mfano, Halmashauri inapotumia EPICAR maana yake Mhasibu hawezi kutumia fedha kwenye fungu fulani zaidi ya *ceiling* iliyowekwa, mfumo haukuruhusu. Vilevile unapotumia EPICAR maana yake ni kwamba, Mhasibu hawezi kuhamisha fedha kutoka kifungu kimoja kwenda kingine; kwa mfano, fedha zilizobajetiwa kwenye *stationery* huwezi kuzihamisha ukatumia kununua *diesel* au ukalipia posho, kwa sababu EPICAR itakuzuia. Vilevile Mfumo wa EPICAR huwezi kutoa LPO kumpa Mkandarasi kama kifungu ambacho utamlipia hakina fedha ya kutosha.

Ukiangalia *in general*, EPICAR kama EPICAR haina matatizo, lakini ninafahamu ili ifanye kazi ni lazima katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SELEMANI J. ZEDI]

Halmashauri husika kuwe na umeme wa kutosha, kuwe na *connectivity* ya mtandao. Kwa hiyo, zile Halmashauri ambazo zinapitiwa na Mkongo wa Taifa au zipo maeneo ambayo *connectivity* ya mtandao ni nzuri, *EPICAR* ni suluhisho la matatizo haya mengi.

Tuna Halmashauri nyingi sana ambazo zipo pembezoni hazina umeme, hazina Mkongo wa Taifa, hazina *internet connectivity*, kwa hiyo, unakuta *EPICAR* inashindwa kufanya kazi. Rai yangu hapa ni kwamba, kama Wizara, kama Serikali, jitihada za makusudi zifanyike ili Halmashauri zote Tanzania ziweze kufanya mifumo yake ya kiuhasibu na kimalipo kupitia Mfumo wa *EPICAR*.

Suluhisho la matatizo ya ulipaji wa Wakandarasi na utumiaji wa vifungu vya fedha visivyoruhusiwa ni kuwa na mfumo mzuri ambao utadhibiti hayo; huwezi kudhibiti bila kuwa na mfumo. Ukitumia *manual system*, hakuna namna utadhibiti. Kwa hiyo, *the only solution* ni kuwa na *proper* mfumo ambao utaweza kudhibiti hii na *EPICAR* imethibitishwa kwamba inaweza ikafanya hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunashukuru kwa Semina ya *EPICAR*. Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatia Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii na mimi nichangie. Kwanza, naomba kuipongeza Kamati ya Mtemi Chenge, kwa kazi nzuri sana inayofanya. Kwa muda mfupi imeonesha matunda mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kwenye ombi lao kwamba, Ofisi yako Mheshimiwa Spika hebu ijaribu kuona na *ku-facilitate* kupata Wataalam wa kutosha ili Kamati hii iweze kufanya kazi yake vizuri. Wameomba Ofisi na Wataalam, kwa kufanya hivyo, Kamati yako hii itakuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

inafanya kazi zake vizuri. Hilo ni ombi la Kamati na limesisitizwa sana, kwa sababu bila kufanya hivyo Kamati hii itakuwa inafanya kazi yake kwa mazoea na kadhalika. Kwa hiyo, narudia ombi la Kamati ya Mheshimiwa Chenge kwamba, sasa nafikiri ni muda mwafaka wapatiwe Wataalam wa kutosha pamoja na ofisi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine, uchumi wake unategemea sana Zao la Pamba. Lipo tatizo ambalo naomba nilisajili na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo bahati nzuri alikuja Jimboni kwangu tukatangaza bei ya mbegu za pamba kwamba, Serikali imeridhia kilo moja sasa wakulima wauziwe kwa shilingi 600 badala ya shilingi 1,200. Wakulima walishangilia sana.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ulipoanza wa kuuzwa hizi mbegu zilienda mpaka kwenye vijiji. Tatizo lililopo kwa sasa ni kwamba, mbegu hizi kwanza zimeenda kwa kuchelewa. Pili, kwa taarifa nilizonazo mpaka jana, mbegu hizi hazioti na wakati huo huo huyu mkulima amenunua shilingi 4,800 kwa kilo nane, hazikuota. Leo ni tarehe 6, mwisho wa msimu wa kulima na kupanda Zao la Pamba ni tarehe 20, mbegu hazijafika lakini hata zilizofika nazo hazikuota.

Naomba niiulize Serikali; huyu mkulima aliyecheleweshewa mbegu zake lakini hata zile zilizofika nazo hazikuota na alinunua; gharama ya kununua mbegu zile nani anailipa? Naomba Serikali ije na majibu namna gani itafidia kwa sababu mkulima huyu ...

**SPIKA:** Naomba mnielewe, kuna Kamati za Kisekta ambazo zitakuja hapa, hayo unayoyasema *yata-fit* vizuri. Hapa najaribu ku-*fit* ndani yake unakuta *hai-fit*. Naomba sana utapewa nafasi wakati wa Kamati ya Kisekta inayohusika itakuwa *relevant*, hapa hakuna atakayekujibu hilo. Haya, tuendelee.

**MHE. RICHARD M. NDASA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa mwongozo wako. Mimi niliona nianze nalo hilo kama utangulizi, lakini maelezo yako nayakubali.

Mheshimiwa Spika, kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Mtemi Chenge, kwenye Fungu Namba 69 ambalo ni Wizara ya Maji, Fungu Namba 24 ambalo ni Wizara ya Kilimo, Fungu Namba 58 ambalo ni Wizara ya Nishati na Madini, kama tukitaka kweli na tumeamua kwamba *Big Results Now* ioneckane; hivi Serikali kwa nini inachelewa kupeleka pesa ambazo Bunge lako Tukufu lilizipitisha? Hivi tatizo ni nini?

Tunajua umuhimu wa Wizara ya Maji, tulikaa hapa tukaongeza nyongeza ya pesa. Wizara ya Kilimo, Fungu Namba 24, tulikaa hapa Waheshimiwa Wabunge tukasema hapana hizi pesa hazitoshi tukaongeza. Nishati na Madini tukakaa hapa tukaongeza, lakini leo naambiwa kati ya pesa zilizopitishwa ni asilimia 78 tu ndizo zimetolewa; hivi tatizo ni nini?

Ukiuliza unaambiwa pesa zinakusanywa nyingi kweli kweli. Sasa hizi pesa kwa nini zisiende kule kwa Wananchi zikafanye kazi ambayo tumekusudia?

Mheshimiwa Spika, Wabunge humu ndani tumefunga mkataba wa miaka mitano na Wananchi ili twapelekee maendeleo na leo bado mwaka mmoja na nusu, Serikali inasuasua kupeleka pesa. Je, pesa hizi zinakwenda wapi? Naomba waje watueleze.

Kamati ya Mtemi Chenge imesema kwamba, Serikali ina matumizi makubwa sana, tofauti na pesa ambazo zinakwenda kwenye shughuli za maendeleo. Waheshimiwa Wabunge, kila siku wamekuwa wakisema humu ndani kwamba, pesa tunazopitisha hapa lazima ziende kwenye shughuli za maendeleo. Shughuli za maendeleo zimesimama kule haziendi zinachelewa kupelekwa, lakini hata zikipelekwa tulikubaliana na ndiyo maana Mheshimiwa Spika kwa busara yako ukasema kwamba, bajeti sasa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

ianze mwezi wa nne ili ikifika Juni kila kitu kiwe kimeisha, ikianza Julai pesa zianze kupelekwa kwenye maeneo. Upo ucheleweshaji ambapo hatujui ni kwa nini Serikali inafanya hivyo.

*Quarter* ya kwanza inapita hakuna pesa ya maendeleo, *quarter* ya pili hakuna pesa zilizopelekwa, unakuja kupeleka labada kwenye *quarter* ya tatu. Matokeo yake ni pesa hizi kutokutumika vizuri, kinachofuata ni hawa Maafisa Wahasibu kulaumiwa kwamba pesa hawakuzitumia kumbe pesa hizi zimechelewa.

Mheshimiwa Spika, niombe sana na kwa dhati, fedha ambazo Bunge limepitisha hapa ni lazima ziende haraka iwezekanavyo ili zikafanye kazi na Wananchi waone matokeo yake; vinginevyo, tutakuwa tunapitisha fedha hapa hakuna kazi inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto ambazo Kamati ya Mzee Chenge imezainisha na hili suala limekuwa likilalamikiwa sana. Naomba kwa mara nyingine tena, Kamati ya Mzee Chenge, iongezewe Wataalam kwa sababu kule nje suala zima la *sim card levy*, kila sehemu tulipolipitisha hapa, kila Mwananchi hata yule wa chini naye alilalamika kwamba, suala hili ni gumu haliwezekani, lakini la *transfer money* limelalamikiwa na mabenki yote pamoja na Wananchi. Naomba Serikali ifanye utaratibu mzuri, ikiwezekana nishauri tu kama inawezekana, Mheshimiwa Chenge, hebu ukae na wadau mliweke vizuri. Hii ni kwa sababu hapa tulikisia kwamba tutakusanya kiasi fulani cha pesa na suala hili nasikia liko mahakamani. Sasa nashauri kwamba, Kamati ya Mzee Chenge ikae iliangalie upya, kwa sababu *sim card levy* Mwananchi aliyeko chini inamwumiza na hili siyo ubishi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabla kengele ya pili haijalia ni nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Hili tumekuwa tukililalamikia kila mara, hivi tatizo ni nini? Hivi kule mbele wenzetu hamsikii au Serikali haisikii malalamiko ya Wananchi?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

Naiomba Serikali hebu muwasikilize Wabunge wanasema nini kuhusu matumizi makubwa ya Serikali. Ni vizuri tukajipanga kwa kila ambacho tunapitisha, tunakubaliana hapa hizi ni za mishahara, hizi ni za maendeleo, basi zile za maendeleo zikafanye kazi za maendeleo; lakini mnachukua na fedha za maendeleo mnazifanyia kazi nyngine, hapo ni kuwakwaza Wananchi wa Tanzania. Nashauri kuwa, pesa za maendeleo ziende zikafanye kazi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi ya Mwaka 2008 (*The Public Audit Act, 2008*), ambayo sasa ilikuwa ikiitaka Serikali mara kwa mara tunapojadili hoja hizi, nao wawe wamesha-*respond* kuhusu hoja za Mkaguzi. Nashukuru leo tunaingia kwenye mjadala huu wakati Serikali pia nayo kwa upande wake wamekwishajibu hoja zote zilizohojiwa na Mkaguzi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti pamoja na vielelezo muhimu; kuna maswali ya kujuliza kulingana na hoja ambazo zimetolewa hapa zote mbili, japo ile ya *PAC* hatujaisikia, zote zinaonesha kwamba, hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika katika utekelezaji wa bajeti, licha ya kubadili *budget circle* yetu kuanza Aprili na kuisha Juni na licha ya kuanzisha Kamati ya Bajeti, kwa sababu matatizo yamebaki yale yale, yanalamikiwa yale yale, fedha haziendi kwa wakati licha ya kwamba tulianza mapema kabisa. (*Makof*)

Kwa hiyo, tuna tatizo kubwa la msingi ambalo bado hatujalipatia dawa na ndiyo ambalo linatupa matatizo makubwa hapo. Hapa naangalia makusanyo ya Serikali

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

kwa robo ile, yalifkia asilimia 85.7. Katika makusanyo haya ya Serikali, mengine yanapaswa kwenda kwenye maendeleo moja kwa moja. Kwa sababu katika bajeti yetu, tumbajeti *almost 2.9 trillion* kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa fedha zetu za ndani, lakini fedha zilizoenda mpaka hivi sasa za maendeleo zote ni asilimia 11 ya robo ile. Maana yake ni kwamba, tulitarajia tungeweza kupeleka asilimia 25 katika robo ile, lakini sasa kwa mikoa ni asilimia 17 tu. Sasa ukiangalia, bado tuna tatizo kubwa la msingi ambalo hatujalipatia dawa yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna tatizo kubwa sana la kupata taarifa za uhakika ili tuweze kuifuatilia bajeti hapa nchini. Nchi zingine zinafanya, sisi hatuna *mid-year review* wala *end-year report* hatupati. Kwa hiyo, ni ngumu sana kujua bajeti kama inafanyika sawasawa au haifanyiki sawasawa, mpaka unakuja kwenye Ripoti ya CAG unakuwa umechelewa mno. Kwa hiyo, ni muhimu sana ninyi Kamati ya Bajeti mkahakikisha Serikali inatoa *mid-year review* pamoja na *end-year report* ili kulisaidia Bunge hili kutekeleza majukumu yake. (*Makofii*)

Lingine, ni mikopo inayoingiwa na Serikali. Bunge hili halijui chochote kuhusu mikopo inayoingiwa na Serikali. Hakuna *information* zozote zinazoletwa katika Bunge hili za kuonesha kwamba, tunakopa kiasi gani na kwa masharti gani. Bunge hili linaletewa kwenye bajeti tu kwamba, Serikali mwaka huu itakopa shilingi trilioni sita kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na kuziba mapengo ya bajeti. Zaidi ya hapo, nani anajua masharti ya mikopo hiyo hakuna. Nani anajua kipindi cha mikopo ile hakuna. Kwa hiyo, Bunge hili linaridhia, lakini fedha hizo ni fedha ambazo mwisho wa siku Tanzania hii lazima izilipe fedha hizo mahala ilikozitoa. Inaathiri mapato ya siku za usoni, inaathiri uchumi wa nchi.

Sasa Kamati ya Bajeti, hili lazima mhakikishe mnalishikilia, kulisaidia Bunge hili pamoja na Wabunge wengine, kuhakikisha kwamba mikopo inayoingiwa na Serikali, tunafahamu sababu za mikopo hiyo, riba na kipindi cha mikopo tukijue. Siyo Bunge linaridhia vitu ambavyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

halivifahamu sawasawa. Haya ni makosa na ninaomba kwa bajeti inayokuja lazima tulete mabadiliko hayo. Kama tatizo ni sheria, Sheria yetu ya *The Government Loans, Guarantee and Grants Act* ya Mwaka 1994 kama haina kipengele hicho, tufanye marekebisho ili iweze kuli-support Bunge hili kujua mikopo yake inapoingiwa inalisaidiaje Taifa na masharti yake yakoje.

Mheshimiwa Spika, kama tungekuwa tunashirikishwa, hata leo Kamati ya Bajeti wasingesema mikopo inaongezeka. Wangekuwa wanajua, kwa sababu wangekuwa wameshirikishwa kutoka mwanzo kabisa. Wangekuwa wanaelewa mikopo hii inakuwaje, kwa sababu wangekuwa hatua kwa hatua wanaridhia ukopaji, hatua kwa hatua wanaridhia masharti ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa bajeti uliopita, Serikali hapa Bungeni iliji-*commit* kwamba, itapunguza matumizi yake kwa shilingi bilioni 283.5; na Waziri wa Fedha kaandika kwa barua kuliambia Bunge hili kwamba, atafanya hivyo katika vikao vyake vya fedha. Wakati anawasilisha bajeti, hatukuona kitu kama hicho na tulitegemea ikifika Disemba tutaletewa kama hicho sasa cha kuonesha Serikali kupunguza matumizi yake shilingi bilioni 283.5 na kuzitoa fedha hizi kuzipeleka kwenye Miradi ya Maendeleo. Badala yake, Serikali ilikuwa na kodi mpya pamoja na kuongeza viwango vya tozo kuziba hili pengo na hili suala la kupunguza matumizi tena likawa limeachwa.

Mheshimiwa Spika, hii haikubaliki. Serikali ilisema hapa Bungeni, ikaahidi kabisa kwamba, hata tukiziondoa hizi kwenye matumizi ya kawaida, bilioni 283.5 hazitaathiri uendeshaji wa Serikali. Kwa nini mpaka sasa hazijaondolewa wala hatujaletewa ule mchanganuo wa kuondolewa na kwamba hizi fedha zitaelekezwa wapi? Hii haikubaliki, Serikali watuletee mchanganuo huo ili tuweze kulisaidia Taifa hili pamoja na kuachana na matumizi yasiyokuwa na tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoroshaji wa fedha nje

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. LUHAGA J. MPINAJ]

ya nchi; ni masikitiko yangu makubwa kwamba, hata Kamati yenye wa Bajeti, hakuna mstari hata mmoja ambao wamezungumzia suala la utoroshaji wa fedha nje ya nchi. Tatizo hili linalimaliza Bara la Afrika sasa hivi. Fedha nyingi sana zinahamishwa kwenda kufichwa kwenye mabenki kule nje ya nchi. Kamati ya Bajeti katika mkakati wao wa kuhakikisha mapato ya Serikali yanaongezeka, hawajaongelea mstari hata mmoja. Mimi nashangaa, Afrika nzima hailali sasa hivi, tatizo fedha zinaibiwa Afrika. Kwa takwimu zilizoko sasa hivi ni kati ya bilioni 50 mpaka bilioni 158 US \$ zinaibiwa Afrika kwa mwaka. Kwa takwimu zetu za hapa nchini ni zaidi ya bilioni 500 zinaibiwa, zinahamishwa kwenda kufichwa kwenye mabenki nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni tulikubaliana tukaunda Tume ichunguze suala hili. Mpaka sasa majibu ya Tume hii hayajaletwa na tulikubaliana mwezi wa nne yaletwe, mpaka leo tuko mwezi wa 12 taarifa hii hajiasomwa, hata kwenye *briefing* sikusikia maana yake haipo kabisa. Tatizo ni nini? Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba, taarifa hii ilishakamilika muda mrefu, toka mwezi Agosti kule, taatifa hii iko tayari. Tatizo na kigugumizi cha Serikali kuiwasilisha taarifa hii ni nini?

Mheshimiwa Spika, sisi hapa Bungeni wote kwa pamoja tuliridhia Serikali iende ikachunguze na ituletee. Watanzania wanataka kujua hatima ya fedha zao hizo zilizofichwa nje ya nchi. Watanzania wanataka kujua mbinu zinazotumika kuficha fedha hizi na fedha zingine zilizofichwa nje ya Uswisi na kote duniani ili tuweze kuzifuatilia na kuhakikisha Taifa linapata fedha. Taifa hili watu wanateseka hawana fedha, Rais analalamika hana fedha.

Rais wangu Jakaya Mrisho Kikwete tulikuwa kwenye mukutano mmoja akasema, angekuwa na uwezo wa Kimungu, angehakikisha kuanzia leo Watanzania hakuna hata mmoja ambaye anakosa maji. Angehakikisha kila mji unapata maji, lakini kwa sababu hana uwezo wa Kimungu, hawezo kufanya hivyo. Nami nikasema kimoyomoyo kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

sababu nilikuwa karibu naye kuwa, ningekuwa na uwezo wa Kimungu ningehakikisha wale walioficha fedha nje tungewafilisi mara moja na kuzirejesha fedha hizo ili kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais aweze kutekeleza majukumu yake sawasawa na nia njema aliyonayo kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maswali ya kujuliza ni mengi sana kwamba hii Ripoti haiwezi kusomwa? Mimi naliomba Bunge hili tuwaagize katika muda huu tutakaokuwa hapa, hii Ripoti lazima tuipate na Wabunge wenzangu naomba mniunge mkono hii Ripoti kwa vyovypote vile lazima iwasilishwe, iwe imekamilika au hajakamilika, tunaomba iwasilishwe katika Bunge hili tujue hatima ya suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yaliyozunguka ambayo najuliza kwa nini kipengele cha utoroshaji wa fedha nje ya nchi imeondolewa kwenye Mpango wa Maendeleo? Hili swalii nauliza kila siku sijajibowi mpaka leo. Mambo yanayochangia kwa kiasi kikubwa utoroshaji wa fedha nje ya nchi ni rushwa katika manunuzi pamoja na mikataba inayoingiwa na Watendaji wa Serikali kwa niaba ya nchi. Lingine ni wizi na ufujaji wa fedha za umma na wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia haya ndiyo hasa mchango mkubwa unaosababisha utoroshaji wa fedha nje ya nchi; unakuja sasa kwenye Taifa, Taifa linafanya nini katika mambo haya? Taifa kama Taifa, sisi tunayo Sheria yetu ya *Income Tax of 2004*, ambayo inazungumzia suala la *Transfer Pricing*, lakini Sheria ile haina kanuni na miongozo inayotulinda sisi kudhibiti mianya hiyo.

Mheshimiwa Spika, *TRA* kwa muda mrefu, leo ni zaidi ya miezi minane, walishawasilisha miongozo pamoja na kanuni kwa Waziri wa Fedha ili aweze kuridhia na sisi tuwe na kanuni. Ukienda Uganda wana kanuni hizi, ukienda Kenya wana kanuni hizi; sisi Tanzania hatuna kanuni. Kwa hiyo, hili ni shamba la bibi. Wafanyabiashara wanafanya wanavyotaka, wanaiba wanavyotaka; hakuna sheria

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

inayowazuia kutuibia. Suala hili ni la dharura, Waziri wa Fedha analo mikononi kwa zaidi ya miezi minane ameshapelekewa na *TRA* hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Manunuzi ambayo ilirekebishwa mwaka 2011, ambayo inawabana hawa mafisadi wanaohujumu kupitia manunuzi, mpaka leo imeshindwa kutoka. Miaka mitatu iko mezani kwa Waziri wa Fedha. *PPRA* walishamaliza zoezi hilo, wakakamilisha wakaweka mezani kwa Waziri, leo tunaingia miaka mitatu hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna tatizo kubwa ambalo yavezekana mpaka hata Serikali yetu sasa Watendaji wetu walishaingiliwa, wanaongozwa na haya mafisadi kiasi kwamba hawawezi hata kufanya maamuzi. Hili ni tatizo kubwa ambalo Taifa linatakiwa liliangalie. Chochote ambacho unataka kuziba mianya ya wizi wa ubadhirifu wa fedha za umma, lina mikwara mizito na haliwezi kupita; ndiyo unavyoona, hata ripoti haiwezi kusomwa.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza suala la Matokeo Makubwa sasa. Matokeo Makubwa sasa, ni lazima na tunamwunga mkono Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kinana, kwa kazi kubwa anayoifanya na kusema upungufu huu bila woga wowote kwamba ni lazima. Nasi hatuwezi kuzungumza Matokeo Makubwa kama hatuwezi ku-*transform government system*. *Transformation* ya *government system* ndiyo itakayotufanya tufikie matokeo makubwa. (*Makofii*)

Mhehimiwa Spika, Mawaziri wanajipa majukumu makubwa; unakuta Waziri ni Mjumbe wa Kamati Kuu, Waziri ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu. Wanajipa majukumu makubwa haya wakati kazi hizi zina watu wa kuzifanya. Mimi ninam-*support* Mheshimiwa Kinana na namwomba atoe tangazo la kuwataka Mawaziri wote wajiu zulu nafasi zao za Kamati Kuu na nafasi zao za u-*NEC*; kwa sababu wengine wanazitumia kama kinga za uzembe wao wa kuwajibika. Uzembe tu wa kuwajibika, kwa sababu kazi hizo zingeweza kufanya hata na Mwanachama mwingine.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

Matokeo yake wanajikuta wako kwenye Vikao vya Chama muda mrefu, huku majukumu yao ya kisera na ya kisheria na kusimamia bajeti hayana mtekelezaji. Wakati mwingine wanawatisha Wabunge wasemaji kama Mpina, siku ya kugombea jina litafutwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine wanaogopa kuzungumza baada ya Mawaziri kujigeuza kuwa wasimamizi wa Serikali; kwa sababu vikao vile ni Vikao vya Chama Tawala, ambavyo Kimsingi vinaisimamia Serikali. Waziri anajigeuza naye anakuwa Mamlaka ya Usimamizi, wakati yeze ni mtekelezaji. Kwa hiyo, namwunga mkono Katibu Mkuu aendelee na zoezi hilo. Watu ambao hawana uwezo wa ku-*perform* wakae pembedni, tupate Viongozi ambao watalifikisha Taifa hili mahala ambapo panastahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inatosha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Moses Machali, atafuatia Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, haiwezekani tukayafikia malengo ya nchi yetu kwa maana ya Matokeo Makubwa Sasa kama suala la nidhamu mionganini mwa Viongozi wa Serikali na mionganini mwa Watendaji wa Serikali halijaweza kuimariswa. Haiwezekani tukafikia malengo yetu kama nidhamu haijaimariswa mionganini mwa Viongozi wa Serikali na Watendaji wa Serikali. Hapa ndipo ambapo utakuja kuona kwamba, ndiyo chanzo cha matatizo yote ambayo yameweza kubainishwa na taarifa ambazo zimeasilishwa na Wenyeviti wa Kamati mbili.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia, yako matatizo ambayo yamekuwa *addressed* leo lakini haya matatizo siyo kwamba ni mara ya mwanza tunyasikia.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MOSES J. MACHALI]

Imekuwa ni kama nyimbo ambazo zinainmbwa kwenye maeneo mbalimbali, matatizo haya yanaendelea kujitokeza. Kwa mfano, Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika ukurasa wake wa 17, imetueleza kwamba, bado kuna tatizo la watuhumiwa wa ujisadi kuhamishwa vituo vya kazi. Mtu anaharibu katika Halmashauri moja, lakini kwa sababu kuna kulindana, wana mtando wao wa kifisadi kuanzia kwenye Wizara mpaka huko chini kwenye Halmashauri, watamtoa kwenye Halmashauri hiyo watampeleka kwenye eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, hili siyo tatizo la leo, ni tatizo ambalo linazidi kuota mizizi na ndiyo maana imefika mahala, watu wengine tunasema kwamba hakuna sababu ya kuendelea kuwa na sheria, maana yake wanajificha. Kuna lugha moja sasa hivi ambayo pia inazidi kukua wanasesma, Watumishi wa Umma watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni za taratibu; wanazunguka mle mle mamlaka ya nidhamu ni fulani, nani ni nani. Sheria hizi na kanuni hizi hazina shida, tatizo ni kukosekana kwa *integrity*, uadilifu kuanzia kwa Mawaziri mpaka kwenye Mamlaka hizo za Nidhamu ambazo zinajitokeza kwenye mamlaka mbalimbali huko chini.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Kamati inayoshughulika na Hesabu za Serikali za Mitaa, imeweza kuainisha hawa watu ambao walihamishwa kutoka katika Halmashauri wamepelekwa Mwanza, Mvomero, Kisapu, Kilindi, Bagamoyo, Same na Masasi. Hata kwangu nimekuwa nalalamika siku zote nasema, Mkurugenzi ambaye leo namtaja jina, Bi. Dorothy Rwiza, amelalamikiwa kwa kiasi kikubwa. Wabunge wa Majimbo ya Uyui, Igalula na Tabora Kaskazini kwa Mheshimiwa Sumar, wamelalamika na waliwahi kumwandikia Waziri Mkuchika, wakilalamika kuwa utendaji mbovu wa Mkurugenzi huyu anayeitwa Bi. Dorothy Rwiza, ambaye mmemtoa kule Uyui ameharibu mmemlela katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kana kwamba Kasulu wanahitaji watu ambao wana mienendo mibaya. Ni kitu gani? (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MOSES J. MACHALI]

Mheshimiwa Spika, nimefika mara kadhaa, nimemweleza Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, wamesema watachukua hatua. Hatua zinachukuliwa mpaka lini? Watueleze wanachukua hatua mpaka lini au pengine mpaka ifike mahala mtushawishi Wabunge na Wananchi twende tukavunje sheria. Ipo siku tutafika mahala tutafunga zile ofisi, kwa sababu yako matatizo mengi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia Ripoti ya CAG. Ukiangalia, kwa mfano, katika ukurasa ule wa 415, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ilifanya manunuzi juu ya mpango kazi wa manunuzi ya Shs. 204,165,640, ikiwa ni sawa na asilimia 158 ya jumla ya matumizi yaliyopangwa kutumika katika maeneo mawili yaliyochukuliwa katika ukaguzi kama sampuli, ambayo ni manunuzi ya mafuta na matengenezo ya magari katika Idara ya Afya na hii ni kinyume na Kifungu cha 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 na Kanuni ya 25, Na. 49(9), za Kanuni za Manunuzi za Mwaka 2005. Wame-cite pale na gazeti ambalo lilitumika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mafuta peke yake, mpango kazi ilikuwa watumie Shs. 93,290,000; lakini wametumia Shs. 210,000,000, tofauti ya Shs. 117,000,000; vitu gani hivi? Leo tukisema Mawaziri wanaohusika tumewataarifu wawachukulie hatua, wawajibike wao kwa nini wasiwajibike? Nenda kwenye matengenezo, walipanga kutumia shilingi milioni 36 Idara moja, wametumia shilingi milioni 122, tofauti ya Shs. 86,640,639. Hilo ni eneo moja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pia nieleze kuwa, Mheshimiwa Waziri namshukuru alifanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Namshukuru vizuri kabisa, ameweza kushuhudia matatizo yaliyopo Kasulu, kwa sababu hata ye ye wamemsumbuwa, watamweleza taarifa hizi hapa, baadaye wanamweleza taarifa nyingine, lakini hachukui hatua, hawa watu wako chini yake kuna nini?

Ninayo *compact disk* ambayo imemrekodi Waziri

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. MOSES J. MACHALI]*

anazungumza anazozana na Watendaji. Mheshimiwa Waziri, wamekushinda hawa watu; wewe una rungu kwa nini usiwapige au huwa wanakuletea bahasha? Tusaidie, maana humu unalalamika kweli, wewe unamwambia Kaimu Mkurugenzi anakujibu, Mkurugenzi anakujibu hovyo hovyo tu. Wewe una rungu kwa nini usipige? Hivi ni vitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mashaka na utendaji wa Mawaziri wetu, kwa sababu wanayaona, wanakwenda *field* wenyewe, lakini hawachukui hatua. Haya matatizo ambayo tunalalamika yatakwisha lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingine; nimewahi kueleza pia matatizo mbalimbali. Ukijaribu kuangalia, kwa mfano, Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu peke yake ilikuwa ina dhamira ya kutaka kuwadhlumu fedha za *Basket Fund*, Kituo cha Afya kimoja cha Shunga, ambazo ni za Serikali. Wale watu wametoa huduma ya kuwahudumia Mama na Mtoto, zaidi ya shilingi milioni 18. Kilichotokea ni nini? Nimeandika barua mara kadhaa, namwandikia Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri, hakuna hatua ambazo zimechukuliwa.

La ajabu, mwaka huu mwezi wa Aprili na hili tatizo nilikuwa nimeliripoti muda mrefu TAMISEMI, hawachukui hatua. Mheshimiwa Aggrey Mwanri, akachukua jukumu la kuwapigia simu, akawapa saa tatu ndiyo wanakuja kutoa fedha. Fedha za mwaka 2010/11 zinakuja kutolewa mwaka wa 2013! Sasa swalii linakuja, wametoa kwenye fungu gani hizo zaidi ya shilingi milioni 18; leo ni 2013? TAMISEMI wana taarifa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya *RAS*, wana taarifa; kote tumewaeleza. Pale Halmashauri, *Internal Auditor* wana taarifa. Unamweleza Mkurugenzi, hakuna kitu ambacho wanafanya.

Sasa Mheshimiwa Waziri nitaomba unisaidie wakati una-*wind up* baadaye au vinginevyo; hii Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu zaidi ya milioni 18 za Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 wamezilipa mwaka 2013 wamezitoa kwenye

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MOSES J. MACHALI]

fungu gani na hizi fedha walikuwa wamezipeleka wapi kwa kipindi chote hicho? Nitaomba niweze kupata ufanuzi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo mengine, tumekuwa tukipitia Mpango wa Bajeti katika Halmashauri hizi na bahati nzuri nakushukuru kwa kunipanga katika Kamati ya Tawala na Serikali za Mitaa, tunapita huko tunakutana na matatizo mbalimbali. Ninaitumia Halmashauri ya Wilaya Kasulu kama *case study* kwa sababu natoka kule, lakini kumekuwa na lugha moja ambayo wanasema wewe ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Mpango kwenye Baraza la Madiwani. Kuwa Mjumbe kama ilivyo katika Bunge letu mambo mengine hatukubaliani hata kama watu wengine wameamua. Kwa hiyo, hilo naomba ku-register kwamba lieleweke.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, juzi wamemdanganya Naibu Waziri wa Maji wakati anajibu wakati wa Bunge la Bajeti. Zilitengwa fedha za Mradi wa Maji katika Kijiji cha Lujuhu ambao ni Mradi wa *Rehabilitation* za kuanzia. Mradi unapaswa kugharimu shilingi milioni 282 kwa mujibu wa Taarifa ya Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Kasulu kwa niaba ya Mkurugenzi. Waziri alipowauliza baada ya kuwa nina swali hapa Bungeni, wakamwambia Mradi utagharimu zaidi ya milioni 500. Taarifa ya mwaka jana aliyonipa Mhandisi ambayo nina maandishi yake, ninayo *softcopy* yake, akasema ni milioni 282. Sasa ninajiuliza hizi gharama nyengine ambazo zinaongezeka kwa kipindi cha mwaka 2012, tena mwezi Novemba ndiyo alinipa taarifa hizi; hizi gharama kutoka milioni 282 leo makisio pengine mpaka Mradi uje ukamilike zaidi ya milioni 500 inatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Halmashauri yangu ilipanga kwamba, kila mwaka itakuwa inatenga fedha kidogo kidogo. Katika bajeti ya mwaka jana tulitenga milioni 85, kwa mfano, kwa ajili ya kuanza kuufanya *rehabilitation* ule Mradi. Maajabu fedha zimetolewa na Serikali, hakuna kazi yoyote ambayo imefanyika katika Mradi ule. Nimefika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MOSES J. MACHALI]

mara kadhaa TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri wewe tupo wote kwenye Kamati, nimekuwa nikiripoti matatizo haya. Imefika mahali nikasema hatuna *good governance*, kama kuna uwezekano vunjeni Halmashauri ile, kwa sababu hata Uongozi wa Halmashauri pia ni tatizo; mwenyewe umeshuhudia wamekusumbua.

Mheshimiwa Spika, mwisho nitaomba nikukabidhi hii *CD*. Naomba hii *CD* mwishoni nikuletee kwa sababu utasikia

...

**SPIKA:** Unanikabidhi mimi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Naomba aje mtu hapa aichukue akupatie utamsikia Waziri analalamika wanavyomsumbu mwenyewe. Haya matatizo yapo, lakini anashindwa kuchukua hatua; ni *vitu gani?* (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, sasa tujiulize kama kweli Serikali inapeleka fedha halafu wakamdanganya Naibu Waziri wa Maji kwamba fedha zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ni shilingi milioni 75 badala ya milioni 85, wamemdanganya Naibu Waziri ambapo majibu ninayo hapa. Zile fedha ambazo walisema millioni 75 hata nazo bado wamefanya uchakachuaji, wamefanya *reallocation*, sijui mliwapa kibali? Nilikwenda kufuatilia TAMISEMI wamesema hawana taarifa ya kufanya *reallocation* ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, wakasema kule itabidi milioni 50 ndio zianze kutumika, hizo milioni 50 kama ambavyo zilipaswa zifanyike Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 mpaka leo hakuna kazi inayofanyika. Wakati mwingine naanza ku-*question* pia Ofisi ya CAG, kwa sababu watu wa CAG nao niliwataarifu tatizo hili, wakasema watakuja kufanya kazi malalamiko haya, lakini hawajaja. Hawajaja na sijaona kazi iliyofanyika au kama wamefanya mimi sina taarifa kwamba wamefanya kazi mambo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano hii michache,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MOSES J. MACHALI]

unaweza kuangalia ni kwa kiasi gani ambavyo Serikali kama ambavyo nimezungumza mwanzoni, kama nidhamu haitaimarishwa mionganoni mwa Watendaji na Viongozi wa Serikali, tusitegemee hayo Matokeo Makubwa Sasa, ambayo tunayahitaji, kwa sababu watu wamepewa rungu lakini hawajui kulitumia, hawataki kulitumia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante.

**SPIKA:** Haya ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hapa mnaanza kupandisha mori, muwe mnanitaja mimi ambaye mkinisema sisemi, mjisema Mawaziri watapata matatizo.

Mheshimiwa Munde Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtinda, halafu atafuatiwa Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Juma Njwayo ajiandae na Mheshimiwa Azza ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Hotuba hizi mbili zilizopo Mezani.

Kwanza kabisa, nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuchangia Hotuba hii. Pili, nawapongeza Wenyeviti wa wote wawili wa Kamati zilizowasilisha Taarifa zake hapa. Nampongeza Mwenyekiti wa LAAC na nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuunga mkono Kamati ya Bajeti kwa kuomba Wataalam zaidi. Tunajua umuhimu wa Kamati ya Bajeti, kwa hiyo na mimi pia ninaunga mkono watu hawa wapewe Wataalam zaidi, ili kuiwezesha Bajeti yetu ikae kwenye mfumo mzuri. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye Kamati ya LAAC. Nikiri kabisa kwamba, Wizara ya TAMISEMI ina changamoto nyingi, changamoto kubwa na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nikatae kwamba hakuna kitu chochote kizuri ambacho kimefanywa na Serikali, vipo vizuri vilivyofanywa na Serikali na vipo vizuri vilivyofanywa na Mawaziri. Kwa mfano, usimamizi umekuwa mzuri ukilinganisha na ulivyokuwa zamani. Zamani Hati Chafu zilikuwa nyingi kweli kweli. Miaka kumi iliopita unaweza kukuta Hati Safi ni nne tu. Mwaka 2007/2010, kulikuwa na Hati za Mashaka 61, ukilinganisha na sasa kuna Hati za Mashaka 29. Mwaka 2007/2008 Hati Zisizoridhisha zilikuwa sifuri na mpaka leo hii ni sifuri. Mwaka 2007/2008 Hati Mbaya zilikuwa sifuri, lakini 2011/2012 kumekuwa na hati moja mbaya. Hayo ni mafanikio, naipongeza sana Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuunda Kanuni mpya za Halmashauri. Wameunda Kanuni mpya ambazo zitasaidia kudhibiti wizi na ubadhirifu mkubwa uliopo kwenye hizo Halmashauri. Sasa hivi wameanzisha mchakato wa Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi kuhojiwa na Madiwani kwa maswali ya papo kwa papo. Nawapongeza sana Wizara. Vilevile kila Diwani sasa atatoa taarifa ya Kata yake kwa miezi mitatu mitatu.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia sana kutokuwa na Miradi hewa. Zamani ulikuwa unaambiwa kuna Kata fulani imejengwa bwawa, lakini Kata hiyo haina bwawa, Diwani haelewi. Kwa kuwashirikisha Madiwani sasa waseme taarifa zao za miezi mitatu mitatu, hii pia itasaidia. Naipongeza sana Wizara, imefanya kazi nzuri na kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi kule Tabora tumepata RC mzuri sana. RC wetu amejikita kudhibiti mapato ya Halmashauri, nampongeza sana Mkuu wetu wa Mkoa, Bi. Fatuma Mwasa, anafanya kazi nzuri sana ya kudhibiti

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]

mapato ya Halmashauri. Hii kazi ni kubwa inabidi wote tushirikiane kuifanya. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha *Lawson System*. Mfumo huu utasaidia sana kupunguza mishahara hewa. Tumekuwa Wabunge tukipiga makelele kwa muda mrefu kuhusu suala la mishahara hewa, suala sugu, lakini Serikali imekuja na mfumo huu ambao naamini mwaka 2013/2014 huenda hatutaona kabisa mishahara hewa. Naipongeza sana Serikali. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kuna tiba moja kubwa ya *EPICAR*, ambayo Makamu Mwenyekiti wa *LAAC* ameitolea ufanuzi mzuri mpaka Mheshimiwa Spika amesema amewapa semina. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Machali kuwa, mambo ya kuzidisha bajeti hayatakuwepo tena kutokana na *EPICAR*, kama alivyosema kwamba watu wanazidisha bajeti haitakuwepo tena.

Suala la kuhamisha fedha, labda imeweke fedha ya kununua dawa watu wakajilipa posho, hilo suala kutokana na *EPICAR* halitakuwepo tena. Fedha hazitahamishwa, kwa sababu kutakuwa na *ceiling*, ukitoa fedha kutokana na *item* iliypopo ikiisha imeisha hutaweza kuhamisha tena. Suala la kuhamisha fedha kwenye akaunti moja kwenda akaunti nyingine lilikuwa linatoa *loophole* kubwa sana ya kuiba fedha Halmashauri. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa suala zima la *EPICAR* ambalo Makamu Mwenyekiti amelielezea vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, suala hili lisiishie njiani, tumekuwa na uzoefu vitu vingine vizuri vinaishia njiani. Tunaomba wahakikishe suala hili linakamilika na linafika nchi nzima. Ninaamini kuna Watumishi wa Halmashauri, Wahasibu wana *Masters*, wana *CPA*, wanakwambia hawaelewi *EPICAR!* Ninashinda kuelewa; ni vitu vyaa makusudi mazima, mtu anafanya makusudi kwa sababu anajua *EPICAR* inabana. Mheshimiwa Waziri, tunakuomba sana hili suala liendelee, ambaye hawezи *EPICAR* aachie

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]*

ngazi, watoto wanamaliza vyuo kila siku watapata ajira. Kwa hiyo, naiomba tena Serikali ifuatilie suala hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakuja sasa kwenye asilimia 20 za ruzuku za Halmashauri. Serikali Kuu inatoa fedha inapeleka kwenye Halmashauri. Halmashauri kama Mawakala wa Vijiji vyetu wanatakiwa wachukue asilimia 20 waipeleke kwenye vijiji vyetu. Baadhi ya Wakurugenzi kwa makusudi mazima hawachukui hizo fedha kuzipeleka kwenye vijiji, ukiwaliza wanasema hizi fedha kulikuwa na matumizi ya dharura tukazitumia. Huo ni wizi na ubadhirifu mkubwa ambao tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri uwaandikie Wakurugenzi wako barua, zile fedha za nyuma wanazodaiwa, asilimia 20, wazipeleke kwenye vijiji husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi kule ni Madiwani, tukasimamie hizi asilimia 20 tukahakikishie zinakwenda kwenye vijiji vyetu kufanya kazi zilizoundwa na Sheria za humu Bungeni kwenye Serikali yetu. Sisi wote hapa ni Madiwani na tunaweza kumhoji Mkurugenzi kwa nini fedha hizi hazikwenda kama ilivyostahili.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna fedha za Vijana na Wanawake. Asilimia tano wanatakiwa wapate Vijana za *own source*, mapato yote ya Halmashauri na asilimia tano wapate wanawake. Baadhi ya Wakurugenzi wetu kwa makusudi mazima hawazipeleki hizi fedha na hatimaye Vijana wetu wanakosa hela. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikikumbuka juzi tu kwenye Bunge la Bajeti, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imepitisha mamilioni ya fedha kwenda kwa Vijana, fedha hizi hizi zinapitia kwenye Halmashauri; tunapata shida sana kuamini kwamba, fedha hizi zitafika kwa Vijana, wakati asilimia tano tu ya makusanyo ya hizi fedha haziwafikii vijana kama inavyotakiwa. Unakuta kuna milioni 300 za vijana hazijaenda, milioni 68 za wanawake hazijaenda. Suala hili linatumiza sisi kama Serikali kwa sababu fedha hizi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]

zingekwenda kwa Wananchi zingeleta maisha bora kwa Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wakurugenzi ambao hawajapeleka fedha hizi wazipeleke na Mheshimiwa Waziri awaandikie barua fedha ziende panapostahili.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vyta mapato vya Halmashauri vingi sana vimechukuliwa na Serikali Kuu. Mimi naiomba Serikali Kuu iangalie upya, vitu vidogo vidogo waachiwe Halmashauri ili Halmashauri nazoziveze kuijendesha. Unakuta mapato ni kidogo, Halmashauri zenyefedha ni zile zenyecess za tumbaku labda, pamba, korosho na nini, zingine zinakosa kabisa mapato kwasababu Serikali Kuu imebana sana. Serikali Kuu iangalie, vitu vidogo vidogo, tunaomba wawaachie Halmashauri. Vitukama *hotel/levy*, sijui nini, vitu vidogo vidogo waachiwe Halmashauri nazoziveze kumudu mahitaji yao; kwasababu Halmashauri fedha zao zinaenda moja kwa moja kwa Miradi ya Maendeleo ya Wananchi. Zinaonekana moja kwa moja. Tunaomba sana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuna fedha asilimia 20 ya ardhi, kule kwenye Halmashauri wanakusanya *property tax*, wanakusanya fedha za malipo ya kodi za nyumba, zile fedha zikikusanya eti zinatakiwa zipelekwe Wizarani kwasilimia 100, *then* Wizara itarudisha baadaye asilimia 20! Mimi naomba hiyo Sheria tuibadilishe, Muswada uletwe hapa Bungeni hizo fedha zinazokusanya na Halmashauri wachukue asilimia 80 wapeleke Wizarani, asilimia 20 ibakiekwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hizo fedha zikienda zote kurudisha ni shida, wanaanza kufuatilia wiki mbili mtuanatumwa analipwa posho, kufuatilia asilimia 20 na hiyo asilimia 20 hapati, posho amelipwa. Mnaanza kuzungushwa, watu wana miaka mitatu hawajapati asilimia 20 inayotakiwa kurudi kwenye Halmashauri. Kwa nini zirudi kwenye Halmashauri wakati wanazikusanya Halmashauri? Kwa nini ile asilimia 20 isibakiekwenye pale pale ikaenda asilimia 80

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]

kwenye Serikali Kuu? Tunaomba sana, Mawaziri wote mko hapa mnanisikia, hili suala liangalieni vizuri.

Mheshimiwa Spika, ruzuku haziji kwa wakati, tunalaumu Halmashauri hawakamilishi Miradi; wanakamilishaje wakati ruzuku haziendi kwa wakati? Kwa mfano, Halmashauri yangu ya Manispaa ya Tabora, kuanzia Julai mpaka Desemba, imelipwa ruzuku ya miezi miwili tu; hivi huyo Mkurugunzi atakamilishaje hiyo Miradi? Atatumia uchawi gani wa kukamilisha Miradi hiyo? Hatimaye Miradi inabaki viporo na haieleweki, ukiuliza unaambiwa fedha zake hazijaja, *value for money* haionekani. Pagale limekaa mwaka mzima, mnaenda mnalalamika kwamba jengo limepasuaka, lazima papasuke, mwaka mzima hakuna fedha lazima ule Mradi uharibike. Tunaiomba sana Serikali, kama tunapitisha Bajeti Bungeni, hiyo bajeti iwe ya ukweli na fedha ziende kama zilivyopitishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la visima, *value for money*, mimi ni Mjumbe wa LAAC nimetembea nimeona Serikali inavyotoa fedha mpaka unaumia. Tumeenda Shinyanga, tumekuta Miradi, Serikali imetoa shilingi bilioni hakuna kisima hata kimoja ambacho kinatoa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huyo aliyefanya upembuzi yanikifu yupo hajachukuliwa hatua, bilioni tatu za Wananchi zinakwenda. Tabora Manispaa tumeletewa bilioni moja, wamekuja kufanya upembuzi yakinifu wamesema kuchimba hapa, kuchimba hapa, wamechimba hakuna maji. Wanaofanya upembuzi yakinifu hawachukuliwi hatua yoyote, wametoka Wizarani, wanakuja kwenye Halmashauri wanasema chimba hapa, chimba hapa, hakuna maji. Hao wanaofanya upembuzi yakinifu ni watu gani? Mimi sielewi.

Mheshimiwa Spika, fedha zote za Serikali zimeenda hizo, watu wamekaa kimya! Ninataka Mheshimiwa Waziri aje na majibu, watu hao waliofanya upembuzi yakinifu na maji hayakutoka Serikali imewachukulia hatua zipi za Kisheria? (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala zima la kada za chini. Leo Mheshimiwa Celina Kombani, wakati anajibu swali asubuhi ameongea kwamba, baada ya mwezi mmoja sasa atatoa barua kwa Halmashauri kuajiri kada za chini.

Mheshimiwa Spika, ninapata shida, toka tumeingia humu Bungeni, mimi nilikuwa wa kwanza kuongea mwaka 2011 kuwa, tunaomba kada za chini ziajiriwe na Halmashauri za Manispaa. Nakumbuka Waziri wa Utumishi alikuwa Mheshimiwa Hawa Ghasia akakubali. Tatizo ni nini mpaka leo mwaka 2013 Waziri anatuambia bado mwezi mmoja tu, miaka mitatu wanafanya mchakato, mchakato upi?

Mheshimiwa Spika, kule tumekuta watu wanakaimu; Mwenyekiti wa Kijiji, Afisa Mtendaji wa Kijiji Kaimu, Afisa Utumishi kaimu, Mweka Hazina kaimu, Afisa Mpango kaimu, Mchumi kaimu, mpaka watu wa chini makaimu. Sasa hawa watu wa chini wawaachie Halmashauri, tatizo ni nini miaka mitatu mizima wanafanya mchakato tu; mchakato upi? Tunaomba sana watu hawa wakaajiriwe na Halmashauri zetu; dereva, sijui karani, sijui nani. Anatokaje dereva Tabora kuja kufanya *interview* Dar es Salaam? Kila siku tunasema, tunaomba sasa Serikali ichukue hatua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala zima la semina za Madiwani, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, sisi kwetu kule Tabora kulikuwa na Watumishi waliochukuliwa hatua na Madiwani; *Engineer*, Mchumi na Mweka Hazina wakachukuliwa hatua wakafukuzwa kazi kutokana na madhambi yaliyokuwepo. Wakaenda Tume ya Utumishi wakakata rufaa, watumishi wake wamerudishwa kazini na wana madhambi, lakini inasemekana *process* tu hazikufuatwa.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wetu wapewe semina waweze kufanya kazi kwa kujiamini. Wanapofanya kazi wananyong'onyea, wanaona wao wanakamata kitu, lakini hakiwi. Tumeonana siku moja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Monduli, tulikuwa kwenye Kamati ya LAAC,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]

alitamani kulia machozi. Anasema kuna *Engineer* mmoja ameiba hela, amefanya moja, mbili, tatu, tumemfukuza, ninyi Wabunge mnafanya nini huko Bungeni? Huyu karudishwa sasa hivi Mtumishi, sisi tunafanya kazi gani? Tuwaache hatuna mamlaka ya kufanya chochote. Kwa hiyo, tunaomba sana muwape semina hawa Madiwani wafuate hizo taratibu ambazo mnazihitaji ili mambo yakija huko juu yawe yamefika kwa uhakika zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mnakaimisha watu, sisi kule Tabora tuna Waweka Hazina wawili, maana wale walivyorudishwa wakakuta wengine wapo. Sasa kama mmewarudisha wapelekeni basi kwenye vituo ambavyo kuna makaimu; maana kuna Wachumi wawili, kuna Waweka Hazina wawili, kuna *engineers* wawili na wote ni Wakuu wa Idara, kiti kimoja.

Mheshimiwa Spika, ni shida sana. Kwa hiyo, naomba hawa ambao wamerudishwa sasa, wawaondoe kwa sababu kazi hazitafanyika pale. *Imagine* watu wamefukuzwa kazi, wamerudishwa pale, watafanyaje kazi na wale Madiwani? Wawaondoe wale haraka iwezekanavyo wapangwe kwenye vituo vingine. Tulilifanya hivyo, tukaongea na Mkurugenzi akasema ameshalfikisha Wizarani, nadhani Wizara inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Christowaja Mtinda, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Amour na Mheshimiwa Juma Njwayo.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, nami nichangie hoja zilizoko mbele yetu. Nianze kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja zote zilizowasilishwa na Kamati mbili.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kusema yafuatayo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDAJ]

Nimefurahishwa na Hotuba au Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, pale alipoanza kwa kusema matatizo makubwa yaliyojitokeza katika Halmashauri zetu mojawapo ni ubadhirifu, ujisadi na utovu wa nidhamu juu ya matumizi ya fedha za umma. Nawapongeza sana Kamati hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema hivi makusudi, Kamati hii ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria na ambayo inawakilisha Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Wananchi wa Tanzania nzima, imeinyoshea mkono Wizara ya TAMISEMI kuhusika moja kwa moja ama kwa kutokusimamia kikamilifu au yenye kuhusika moja kwa moja na ujisadi huu. Tumekuwa tukipiga kelele hapa Bungeni, maswali mengi yalikuwa yakielekezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu hususan hii Wizara ya TAMISEMI kwamba, kumekuwa na ujisadi mkubwa sana katika Halmashauri zetu na kumekuwa na uzembe mkubwa sana wa kuwachukulia hatua wale Watendaji wabadhirifu au watovu wa nidhamu ambao wanatafuna fedha za Serikali, kodi za Wananchi, kwa manufaa yao wenye.

Mheshimiwa Spika, mfano ambao wameutoa wamesema kwamba, kwa mwaka 2011/2012 jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 1.7 zilitumika nje ya bajeti, iliyoidhinishwa bila kibali kutoka mamlaka husika, kinyume na Kifungu Namba 10(3) cha Sheria ya Fedha Na. 9 ya Mwaka 1992, iliyorekebishwa mwaka 2001. Hizi shilingi bilioni 1.7 ni katika Halmashauri 38 tu. Kama Wizara yenye husika inanyooshewa kidole na Kamati ambayo sisi tunaiamin na tunaituma kwa niaba ya Wananchi kwa ubadhirifu mkubwa namna hii; ina maeleo gani kutuambia sisi Wabunge? Naomba maeleo ya kina ili tunapokwenda kule kwenye Halmashauri zetu, Wabunge wa Majimbo wanapokwenda kwenye Halmashauri zao au kwenye Majimbo yao, wasinyoshewe vidole kwa sababu tu Wizara inahusika kwa asilimia mia moja kutokuchukua hatua hizi.

Mheshimiwa Spika, ujisadi mwengine ambao umeoneshwa na Kamati hii ni ujisadi kwenye maduhuli

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA]

yasiyowasilishwa na Mawakala wa Ukusanyaji toka mwaka 2007/2008 mpaka 2011/2012; na hii ni Ripoti ya CAG, wametoe Jedwali katika ukurasa wao wa 11. Toka mwaka 2007/2008 mpaka 2011/2012, mapato ambayo tayari yalishakusanya ni jumla ya shilingi bilioni 13.1; hizi hazionekani ziko wapi, lakini wahusika wapo! Nani amewahi kuwajibishwa kwa utovu wa nidhamu wa kiasi hiki wa kutokuwasilisha maduhuli ambayo yamekusanya katika Halmashauri? Ni nani amewajibishwa hatujasikia, tunayoyasikia ni kupigapiga chenga. Tunataka maelezo ya kina ni kwa nini fedha nydingi kiasi hiki zimekusanya lakini hazifanyi kazi yake sawa sawa?

Mheshimiwa Spika, Kamati kutokana na Jedwali lao wamezungumzia, kwa mwaka 20011/2012, kiasi cha shilingi bilioni 4.5 ambazo zimekusanya, maduhuli ambayo yamekusanya hayakuwasilishwa na Halmashauri 56. Hizi ni kwa fedha za mwaka mmoja tu. Shilingi bilioni 4.5 zingejenga maabara ngapi na vifaa vyake vyote katika Sekondari zetu za Wananchi au Sekondari za Kata ambazo kila siku tunapiga kelele hapa? Hizi fedha zingenunua vifaa vya kiasi gani kwa ajili ya akina mama wajawazito na watoto huko vijijini ambao kila siku wanakufa kwa kukosa vifaa au kukosa dawa au kukosa matunzo kule hospitalini? Fedha kiasi gani ambazo zingetumika kujenga vitu hivi, lakini hazijawasilishwa. Shilingi bilioni 4.5 kwa mwaka mmoja tu 2011/2012!

Mheshimiwa Spika, Wizara ipo na inafahamu ni kwa nini hatua kali hazichukuliwi haraka iwezekanavyo kuwajibishwa wadokozi wa hizi fedha au kuwajibishwa hawa wezi ambao pia wanaitia aibu Serikali ya Chama cha Mapinduzi, wanaitia aibu Wizara ya TAMISEMI? Kwa nini hawachukuliwi hatua? Sisi huku tunasema tunashukuru *Alhamdulillahi*, mnafanya vibaya sisi tunakwenda mbele. Sisi tunashukuru tunatoa maovu hayo. Nitahitaji majibu ya kina kutoka Serikalini ni kwa nini uzembe wa namna hii unaendelea mwaka hadi mwaka toka mwaka 2007/2008 mpaka leo mwaka 2012 na huu ni mwaka 2013?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDAJ]

Mheshimiwa Spika, kilio kingine kikubwa ni fedha za Miradi ya Maendeleo ya Halmashauri kutokutolewa kwa wakati. Kilio hiki kimekuwa kikitolewa kila mwaka na Wabunge wote wamekuwa wakipigia kelele fedha za maendeleo kuchelewa. Mimi leo nina mfano halisi; katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, mimi ni Mbunge wa Singida, nahudhuria Vikao vya Halmashauri. Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambayo pia imetoa Halmashauri nyingine ya Wilaya ya Ikungi, katika bajeti ya mwaka huu ilitengewa shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya maendeleo. Cha kusikitisha, *quarter* ya kwanza haikupelekwa, *quarter* ya pili ambayo imepelekwa wiki iliyopita zimepelekwa jumla ya shilingi 304,567,000, ambayo ni sawa na asilimia 8.9 tu kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hii ni *quarter* ya pili, *quarter* ya kwanza hakuna kilichopelekwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri mpya ya Ikungi, yenyewe ilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 3.1. Cha kusikitisha fedha zilizotolewa wiki iliyopita ambayo ni *quarter* ya pili ni shilingi 279,000,000, ambayo ni sawa na asilimia tisa tu. Sasa kwa hali hii pia Miradi ya Maendeleo itatekelezwa vipi na hizi Halmashauri watatoa wapi fedha? Hili linapelekea sasa wale Watendaji amba siyo waaminifu, wanatumia hiki kiasi kidogo cha fedha kwa matumizi mengine. Hilo ndiyo linakuwa tatizo lingine. Hivi sasa Halmashauri hii nimesema imegawanywa na Halmashauri nyingine ya Wilaya ya Ikungi. Kwa hiyo, bado zina-share akaunti moja, fedha hizi zinapelekwa kwenye Halmashauri iliyokuwa ya mwanzo Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Sasa kuna mgogoro mwingine umeibuka tena. Fedha hizi zikiplekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Singida mpaka zigawiwe kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, ni mbinde wana mgogoro mpaka wamefikishana kwa *RAS*.

Naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie, nia njema ya kuanzisha Halmashauri ya Ikungi iwe ileile nia njema ya kupeleka fedha ya Halmashauri ya Ikungi kwenye akaunti yake ili huu mgogoro uishe. Hii imepelekea fedha za Mradi wa Maji shilingi 400,000,000 zimeshindwa kugawanywa mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa hazijagawanywa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA]

kwa sababu ya huu mgogoro ambao upo wanagombana kwanza. Kama Halmashauri ya Ikungi ipo, naomba ipelekewe fedha zake, Halmashauri ya Singida ipelekewe fedha zake katika akaunti zake ili hii migogoro isiyokuwa na tija tusikwambie wewe. Hakuna haja ya kuja kukwambia wewe tena, fedha zitumike vizuri ili suala la aibu hatutaki kufikishana tena mbele yako.

Mheshimiwa Spika, cha mwisho ambacho ninataka kukizungumzia ni kutokana na Ripoti ya CAG. Katika Halmashauri zetu hakuna mifumo madhubuti ya ndani ya kudhibiti matumizi sahihi ya fedha. Hii nimesema kutokana na mfumo madhubuti pia kunasababisha wale Watendaji wasio waaminifu kutoa *excuse* kwamba, fedha zilizotumwa kwa maendeleo hazijafika au zimefika kidogo, kumbe wakati mwingine zimefika kwa wakati au zimefika za kutosha, kwa sababu hakuna mfumo madhubuti wa kusimamia, Mtendaji mwingine anazitumia kwa manufaa yake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, hili nina mfano mmoja; Mkurugenzi wa Manispaa wa Singida, ambaye kwa bahati mbaya amehamishwa, alitumia jumla ya shilingi milioni 48 kununua pikipiki nne kwa ajili ya Maafisa Ugani. Pikipiki nne, maana yake pikipiki moja ni shilingi milioni 12; hivi pikipiki gani hiyo? Pikipiki ya aina gani inapaa angani ya shilingi milioni 12?

Mheshimiwa Waziri huwa unatuambia kila siku hili suala mkaliulize kwenye Vikao vya RCC. Tuliliuliza kwenye Vikao vya RCC na nakwambia niliuliza na Mkuu wa Mkoa alilisemea vizuri sana na akatoa maagizo kwamba, huyu Mkurugenzi na Mhasibu wake washughulikie watuletee majibu ya kutosha kikao kinachofuata. Bahati mbaya mmemhamisha huyu Mkurugenzi sasa tutamwuliza nani? Tutamwuliza nani hizi shilingi milioni 12 pikipiki moja; hakuna wa kumwuliza amehamishwa ameletwa mwingine, maana fedha zimekwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu na ni uchungu na ndiyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDAJ]

maana watu wanalamika hapa kwamba, anakosea hapa anapelekwa kwingine akaibe. Sasa safari hii atanunua baiskeli kwa shiliingi milioni 20 mtamwuliza wapi mkimwuliza atahamishwa tena! Tunapata matatizo makubwa sana kwa ajili ya mambo haya. Hebu tusikilize mapendeleko ya Kamati kwamba, kabla mtu hajawajibishwa kwa kile alichokifanya asihamishwe kwanza atujibu majibu haya, kwa sababu nitakwenda kwenye RCC sitauliza pikipiki tena hayupo. Mimi nasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Abdallah Amour!

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, ni-*declare interest* na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Katika kuchangia nitajikita sana katika changamoto ambazo tulipewa na Kamati ya Bajeti, lakini sitazieleza kwa kirefu. Ucheleweshaji wa kutoa fedha za maendeleo, kwa mfumo huu tulikuwa nao sasa wa *cash budget*, siyo rahisi *quarter* ya kwanza kutolewa fedha kwa wakati kwa sababu tunangojea tupate zile fedha ndiyo tutoe. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwa hii *quarter* ya kwanza tukope fedha ili tuweze kutoa kwa wakati na naamini kama tutafanya hivyo *quarter* ya pili fedha zitakwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nitakalolizungumza ni kuhusu vifungu ambavyo vimepangiwa kwa kila sekta vinaongezeka bila idhini ya Bunge. Tumelisemea sana jambo hili lakini bado linaendelea. Kuna vifungu tayari vimeshakuwa bajeti kwa kiasi fulani na ile bajeti imeshakuwa kiasi fulani imegawanywa kwa vifungu. Ukichukua kifungu kimoja ukakipa fedha zaidi, vifungu vingine vitapata fedha zilizokusudiwa wapate. Kwa hiyo, naishauri Serikali ikiwa kweli wanataka kifungu hiki kukihamisha, kabla ya kuleta *supplementary budget* kunako Bunge, angalau wakae na sisi Kamati ya Bajeti, watueleze kumetokea dharura kwa hiyo kifungu hicho tunakizidishia kiasi fulani cha fedha, lakini

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR]

kimya mpaka tuwaalize ndiyo wanasema. Kuna kifungu hivi sasa kimeshamalizika hakina fedha hata kidogo na bado wanataka kufanya kazi na hivi sasa wanatumia fedha za dharura. Sasa nataka kumwuliza Waziri mkishamaliza hizo fedha za dharura mtachukua kifungu kipi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea nakuja kwenye makusanyo ya fedha. Tayari sasa hivi tumekusanya fedha, tumebuni vyanzo vipyta nya mapato, lakini hayo mapato tunaona yanavuja tu hayaendi kunakohusika. Kamati ya Bajeti tayari imependekeza vyanzo vipyta nya mapato, lakini pia hawa wataalamu hawajavishughulikia mpaka sasa wakaona vipyta nya kuweza kukusanya na vipyta nya kuweka mwaka kesho. Kwa vile wanaona bajeti tayari, wote nafikiri wanataka kuvileta mwaka kesho. Hivi sasa tunahitaji fedha, fedha za maendeleo haziendi za kutosha, kwa hiyo, naiomba Serikali ione vyanzo tulivyoipanga wavipitie na ikiwezekana vianze kukusanya fedha.

Mheshimiwa Spika, nikija katika suala la kutoa fedha kidogo za maendeleo; tayari bajeti imeshapangwa, fedha za maendeleo zinakwenda kiasi gani kwa mwaka huu halafu usizipeleke zile fedha, matokeo yake bajeti ya mwaka wa pili unapanga Miradi mipyta ile hujaimaliza. Sasa ile Miradi mipyta haiwezi kufanyakia, zile fedha zinakwenda kulipa Miradi ya zamani. Lazima tujipange vizuri na tuwe na *timeframe*, Mradi huu unaanza tarehe ngapi au mwaka gani unakwisha mwaka gani na fedha zake kiasi gani tunamaliza kiasi gani. Pia tusianzishe Miradi mipyta kabla ile mikongwe hatujaimaliza. Kwa nini tunafanya Miradi 200, Miradi mitano inatushinda kuimaliza? Bora sasa tujikite ile Miradi kidogo tuifanyie kazi, tuipe fedha za kutosha imalizike tuanze Miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nitazungumzia kuhusu Sheria ya Manunuzi. Hii Sheria ya Manunuzi kila siku tunapiga kelele irekebishwe haifai. Bei ni tofauti na iliyokuweko kwenye soko hasa kwa vifaa nya ujenzi. Ukitazama saruji kule shilingi 15,000, ukija huku kwenye soko unaweza ukaambiwa saruji ni shilingi 10,000 au 8,000; ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR]

mfano tu natoa. Sasa kwa nini hatuipitii Sheria ya Manunuzi tukairekebisha na matokeo yake fedha za Serikali nydingi zinapotea kwenye Sheria ya Manunuzi?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni matumizi makubwa ya Serikali. Katika kugawa bajeti, kuna mfumo mbaya tunaoutumia. Ni vizuri kwanza tukajikita tukatimiza zile fedha za maendeleo nydingine tukaweka matumizi ya kawaida. Kwa namna hiyo, Serikali haitopata nguvu kuchukua fedha wakatumia bila mpangilio.

Kwanza, tatizo la Serikali wanunu magari ya gharama, wanajilipia safari za nje kila siku, Serikali kila siku wanataka kutibiwa kwenye hospitali kubwa kubwa, mradi mambo mengi kwa hiyo zile gharama za hospitali zinakuwa kubwa. Ikiwa fedha zile tutazipeleka kwenye maendeleo, tukajifunga mkanda tukasema sasa basi hicho kidogo kilichokuwepo tugawane kidogo kidogo, hivyo tuna uwezekano wa kupata maendeleo, lakini kwa mgao huu unaokuja wa kutosheleza matumizi ya Serikali halafu kidogo kuwapa maendeleo, maendeleo hayatopatikana maisha.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuzungumzia habari ya vyanzo vya mapato. Ni kweli tunajitahidi kukusanya vyanzo vya mapato, lakini kinachojitokeza mapato yanavuja, kwa sababu kukusanya mapato jambo moja na kusimamia ni jambo lingine. Ikiwa tunabuni Miradi tu, tunabuni vyanzo vya mapato lakini usimamizi mbovu, hatutoweza kuongeza mapato ya nchi. Kwa hiyo, ni vizuri tukasimamia mapato haya yaliyokuwepo kabla ya kutafuta vyanzo hivyo vingine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hilal Hamad!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi kuzungumzia Taarifa za Kamati hizi mbili ambazo ni muhimu; Kamati ya Bajeti na Kamati ya Serikali za Mitaa. Nianze na Kamati ya Bajeti, nawapongeza kwa Taarifa nzuri, mmeweka mambo wazi. Naunga mkono hoja ya kuishawishi Serikali izungumze na mamlaka zinazotuungezea ile *ceiling* ya kukopa tukope zaidi.

Mapendekezo yangu tunapokopa tukope na tuwekeze kwenye tija. Nina mfano, kama tungelikopa tukatengeneza miundombinu ya kilimo, watu wakajengewa miundombinu ya kumwagilia, halafu wazawa wenyewe bila kuleta watu wa nje wakapewa majoruba yale ya kisasa kama wanavyofanya nchi za China, tutazalisha zaidi na kwa sababu tutazalisha mazao mengi zaidi tutatengeneza *silos*, tutakuwa na hifadhi ya chakula cha miaka mitatu au minne na Tanzania itakuwa soko la chakula kwa Afrika yote. Nashauri Serikali isifikirie hilo, iende kuomba, msibabaishwe na *World Bank*, msibabaishwe na *IMF*, tunaruhusiwa kukopa na sisi tunakopesheka mkope na mtumie kwa tija.

Mheshimiwa Spika, katika suala la bajeti, kama alivyosema Mbunge aliyetangulia, tumeona *quarter* ya kwanza hatuvezi kuzipata zile fedha na mfumo huu ambao wewe ulijasiria kuanzisha, tulitegemea *quarter* ya kwanza tungepata fedha zile kumbe haziwezi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mbunge aliyezungumza awali kwamba, sasa tukope kusudi pesa tunazokopa matumizi ya *first quarter* yatusaidie kuanzisha ule mchakato wa kuzunguka ili tuondoe tatizo la pesa za *quarter* ya nne kuja kuangukia *quarter* ya kwanza ya mwaka mwingine. Mantiki nzima ya mzunguko mpya wa Bajeti yetu tutakuwa tumeiokoa kwa kufuata mtindo huo.

Mheshimiwa Spika, upande wa Bajeti sina mengi, niende TAMISEMI. Nawapongeza ndugu zangu wa TAMISEMI na namwomba Mwenyekiti, Kamati yenu ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE]

TAMISEMI, kipindi kijacho mtembelee Wilayani kwangu nako mkaangalie myaweke wazi. TAMISEMI inahitaji kitu kimoja, tunahitaji kujenga taswira ya TAMISEMI. TAMISEMI kwa Kiingereza ina *poor image*, naweza nikawaambia kwa kifupi hivyo. TAMISEMI au *Local Government* zilikuwepo nchi hii ilikuwa na *Local Government*, Serikali ikafanya maamuzi ikaondoa *Local Government*. Tunajaribu ku-copykuzirudisha na tunashindwa kutengeneza *Local Government* kama tulivyokuwa nazo.

Mheshimiwa Spika, tumefanya makosa kama alivyosema Mheshimiwa Zedi na mimi nataka kuwashauri, kosa liliolofanyika mlichukua watu na kuwaweka kwenye nafasi ambayo katika Menejimenti ya Utawala ni kosa. Kuna watu ni Wakurugenzi lakini hawapaswi kuwa Wakurugenzi, kuna watu ni *Directors* wa Fedha, *DT*, hawana sifa za kuwa *DT*, matokeo yake ndiyo haya yanayotokea.

Mimi sielewi mtu ananunua pipipiki shilingi milioni kumi na mbili sasa unasubiri nini? Niwape mfano mmoja wa Wilayani kwangu; kuna watu katika Wilaya ya Muleba walikuwa wanaiba pesa ya wafanyakazi, wanakata shilingi moja moja wanakula, Mkuu wa Wilaya akasema waende Mahakamani wakaenda wakashinda; lakini walioibiwa pesa wapo, walioiba pesa wapo na cheki zilizotumika zipo halafu mnafanyaje?

Mheshimiwa Spika, mnachopaswa kufanya, naishauri Serikali ni kujenga taswira. Kujenga taswira ni kwamba, wewe Mahakama imekuona una hatia, sisi tunakuondoa kwa manufaa ya umma, anatoka ofisini anakwenda asihamishiwe sehemu nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yanaweza kuwa yapo matatizo kama alivyosema mjukuu wangu Mheshimiwa Kafulila kwamba, sijui ya taratibu, kanuni na matumizi. Hizo taratibu kama zinaleta matatizo zirudisheni Bungeni. Kinyume chake, Mawaziri rafiki zangu, mtasakamwa mtapandwa *pressure bure*. Kama kanuni, taratibu na sheria zinakuwa ni kikwazo zirudishwe zilikotoka na zilikotoka ni Bungeni. Mtu hawez

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE]

kununua pikipiki shilingi milioni kumi na mbili ukaenda kwenye RCC, unakwenda polisi. Mheshimiwa Rais amewahi kusema kwamba, *auditors* huandamana na polisi, ndivyo mfumo ulivyokuwa, alikuwa anawaelekeza kwamba fanyeni hivyo, amelisema na siyo mara moja.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha watu wanaposhindwa ku-realise ile *value for money*. Niliwaeleza kwamba, tulikosea *recruitment* hatuku-recruit lakini sasa tulipo tufanye nini? Tafuteni watu ambao mnadhani wanaweza ku-manage position hizo za Idara na Ukurugenzi wapelekene vyuoni. Peleka hamsini wafundishe, wafanyie *vetting*, ukirudi ondoa hamsini weka hamsini nenda hivyo, msiogope kuandaa. Unajua Watanzania mna tatizo la kuogopa kuandaa watu, lakini *succession program* ni kuandaa.

Nchi nyingine kama Marekani hata Rais anaandaliwa. Unachukua miaka kumi, ishirini, unamwandaan Rais, siyo unachukua mtu unaweka utapata matatizo. Kwa hiyo, muwaandae hawa watu tuepuke makosa haya. Niwaeleze kitu kimoja, gharama ya kuandaa ni ndogo kuliko hasara tunazopata. *We are loosing a lot of money*, kama mtu aliyetumwa pikipiki ya milioni sita akanunua ya milioni kumi na mbili!

Mheshimiwa Spika, bado nipo hapo hapo kwenye *recruitment process*. Tumekuja katika *recuitment process*, TAMISEMI mlichopoteza kitu kingine na bahati mbaya mpo kwenye *Big Results Now; Big Results* haiwezi kufanikiwa isipoandamana na *discipline*. Kama mtu hana nidhamu ya kufika kazini, kama hana nidhamu ya matumizi, hawezi kufanikiwa na hiyo huwezi kuipata mpaka ufanye *vetting*, mpaka mtu umpe maandalizi. Sasa unakuta mtu yupo, hana malengo wala hajawahi kufundishwa malengo, lakini anaendelea hivyo hivyo. Kitu kingine, TAMISEMI niwaambie, ukiazima falsafa au *literature* za *Council* za zamani, Halmashauri zilikuwa na mamlaka na uwezo wa kukusanya rasilimali (*resoure mobilization*).

Halmashauri, Serikali za Mitaa, sasa hivi hazina

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE]

uwezo, unaona Mtendaji ili aweze kuwa-*mobilise* watu wakusanye mawe au matofali mpaka atumie rungu; haikuwa hivyo. *Bukoba Council* haikufanya kazi hivyo, watu walijenga madaraja, barabara au wale Wamisionari. Kule kwetu Wamisionari walijenga shule nyingi lakini hawakumpiga mtu viboko. Kwa hiyo, mna tatizo TAMISEMI katika *resource mobilization*, katika *peoples mobilization*, kuhamasisha watu wakaleta pesa, kukusanya mawe na kazi zikafanyika.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kama mngetathmini nguvu za Wananchi zinaweza kuzidi hizi fedha ambazo zinatoka Serikalini. Unaweza ukachimba mitaro kwa gharama nafuu, kaulize *quotation* ya kuchimba mtaro kwenye *quotation* wanazoleta kuchimba maji inatisha. Mtu anakwambia kuchimba mita moja shilingi laki moja, lakini ungeweza ku-*mobilise* watu wakachimba kwa kuwa mambo ni ya kwao. Angalieni suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuishauri TAMISEMI kama alivyosema rafiki yangu Bwana Zedi kwamba, ye ye anashauri na mimi nishauri, ushauri upo katika namna ya kuijandaa sasa kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine nilirudie, nimekuwa nikilisema mara kwa mara, *problem yetu ipo wapi TAMISEMI?* Meneja mzuri, Mtendaji mzuri, ana mambo matatu, nairudia mara ya kumi katika Bunge hili; unakuwa na *authority, responsibility* na *accountability*. Kama hauna vitu vitatu unafungua mlango na mizigo yako unaondoka. Mmewapa watu *responsibility* bila *authority*. Mmewapa watu *authority* na *responsibility but they are not accountable to anybody*. Ndiyo maana mtu akanunua pipipiki ya milioni kumi na mbili halafu Mkuu wa Mko a anatoa maelezo mazuri, maelezo mazuri gani aliyo yatoa Mkuu wa Mko wa Singida? Maelezo mazuri ni kumfunga mtu, angefungwa huyo mtu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kama inasikia watu wenye makandokando kama hayo na mimi nawaambia wale

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE]*

walioiba pesa za Wafanyakazi Muleba, TAMISEMI muwafutie kwa kuwapeleka, msiwapeleke Kasulu. Walioiba pesa za Wafanyakazi kwa kukata mishahara Mahakama imemaliza kazi yake, lakini imemaliza ilivyojuu yenye. Hatuwezi kukaa na watu wenye kasoro katika ofisi. *Image* ya TAMISEMI, ndiyo maana wanasema zikishakatwa kule Wilayani kuna mahali zinapelekwa na mimi siwezi kutafuna maneno, wanasema zinarudishwa TAMISEMI. Wanasema zinarudishwa kwa wakubwa. Sasa hatuwezi kukubali, namna yakujikomboa, namna ya kusafisha *image* ya TAMISEMI, anayepatikana na kasoro anatoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alisema, Mke wa Mfalme alisingiziwa kuzini, jopo la Mfalme wakachunguza na Wazee wa busara wakasema Malkia kweli hakuzini na kijakazi. Mwalimu anasemaje hukumu iliviotoka kwamba, kwa sababu amehisiwa hana sifa tena ya kuwa Malkia. Sasa TAMISEMI mtu yule ye yote atakayehisiwa mrudishe kwenye *profession* yake, kama alikuwa bwana nyuki arudi kwenye bwana nyuki, kama alikuwa anafagia akafagie, kama alikuwa anakata manyasi arudi kule, nenda kwenye kuandaa. Andaa watu waadilifu, tafuta vijana watengeneze, kuna namna ya kutengeneza watu, Viongozi wanaandaliwa. Kwa kufanya hivyo mtajenga taswira ya TAMISEMI. (*Makofii*)

Msibebi matatizo ambayo siyo yenu. Mawaziri siwatetei lakini mnabebe matatizo ambayo siyo yenu. Mimi huwa nawasikia na wengine unamwambia kitu na yeye analalamika; sasa mimi nilalamike, Mwananchi alalamike, Waziri alalamike; nchi gani ya kulalamika!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namna ya kufanya, nimewapa maelekezo, mkinihitaji naweza kuja kuandika hata *paper*. Tafuta watu msichoke kufukuza. Afadhali niwaambie, ukimfukuza mtu ukamlipa milioni thelathini ni bora kuliko kubaki naye akakuingiza hasara ya *1.5 billion*. Miradi inayokwenda TAMISEMI inachukua pesa yote ya nchi. Pesa nyingi inakwenda kule, sasa mwachishe bwana

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE]

kwa masilahi ya Taifa unaondoka hufai, kiinua mgongo chako milioni thelathini. Aende mtaani tubaki na watu wachache tuweze kuleta Matokeo Makubwa mara moja. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba niunge mkono hoja. (*Makofij*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed atafuatia.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema, hatimaye nimeweza kusimama ndani ya Ukumbi wako na kuchangia Taarifa ya Kamati ya Bajeti na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Taarifa iliyoletwa na Mwenyekiti mbele yako nimeipitia. Nianze kwa jambo ambalo linazisumbua Halmashauri zetu. Kwa muda mfupi ambaao nimekuwepo katika Kamati hii, Halmashauri nyingi zinaonekana kutopelekewa fedha kwa wakati husika.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja tu wa Halmashauri ambayo ninatoka, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga; mpaka sasa hivi imepokea fedha za maendeleo shilingi milioni mia sita na tano peke yake. Sasa najiuliza hiyo Miradi inatekelezwa vipi halafu inafika pahala tunaanza kushangaa kwa nini Miradi haijakamilika?

Juzi nilikuwa na swali humu ndani la Wizara ya Maji, nilijibowi nikaambiwa fedha zimekwenda, lakini nasikitika sana kwa majibu yale, kwa sababu ninachoongea ninakifahamu. Mfano wa Wizara hiyo ya Maji, fedha walizopelea Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, hiyo shilingi milioni mia sita aliyonijibu Naibu Waziri wa Maji ni

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]

fedha ambayo imekwenda kwenye Miradi iliyokwishakamilika; Miradi ya Didia na Mishepo. Miradi hii pamoja na kukakamilika, Halmashauri bado inadaiwa zaidi ya shilingi milioni mia mbili halafu Waziri ananiambia fedha inatosha na ni fedha nyingi; ninasikitika kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, bado kwa mwaka huu wa fedha, kuititia kitabu ambacho kimetolewa na Wizara ya Maji, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuonekana kumetengwa shilingi milioni mia tisa na kidogo kwa ajili ya Miradi mitatu ambayo Halmashauri iliamriwa kutangaza zabuni, imeshatangaza zabuni lakini katika Miradi hiyo mitatu Mendo, Nyashimbi na Manyaga, thamani yake ni bilioni moja pointi saba. Sasa najiuliza; hizo fedha nyingi nilizokuwa naambiwa tumetengewa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni zipi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutangaza zabuni fedha hiyo haijafika hata shilingi moja. Sasa kule Halmashauri wanajiliza wasaini mkataba au wasisaini kwa sababu pesa hawajapokea na muda ndiyo unakwenda!

Mheshimiwa Spika, hili linasikitisha sana na sielewi kwa nini haya mambo yanaendelea kufanyika wakati tumepitisha Bajeti kwa muda unaostahili, lakini fedha hizi haziendi kwa wakati. Miradi ya Barabara mpaka hivi sasa fedha hazijafika katika Halmashauri zetu. Halmashauri karibu zote hazijapokea, kama zipo sijui kama zinafika tano, lakini mfano mzuri Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mpaka sasa haijapokea fedha ya aina yoyote. Masika ndiyo imeshaanza, matokeo yake barabara zinatengenezwa kipindi cha masika, halafu unakwenda kufanya ukaguzi wakati mvua zimenyesha na barabara ile imetengenezwa, thamani ya fedha haionekani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwenye Miradi ya Maji. Huyu mtu anayetwa Mpembuzi Yakinifu anayetoka Wizarani na kwenda kule kwenye Halmashauri na kusema hapa maji yanapatikana matokeo yake hayapatikani; hivi anachukuliwa hatua gani na Serikali? Kwa sababu ni

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. AZZA HILLAL HAMADJ]

maeneo mengi ambayo wamepita wakasema hapa maji yanapatikana. Mfano mzuri tu katika swali langu hilo hilo la juzi, kuna vijiji vitano katika vijiji kumi na tano ambavyo vilipaswa kuchimbiwa visima vya maji, Halmashauri ya Shinyanga vijiji vitano havikuweza kupata maji. Katika vijiji hivyo vitano, kuna Wataalamu waliotoka Wizarani na wakasema hapa maji yanapatikana. Vijiji hivyo ni vya Midati, Jom pale Mji Mdogo wa Tinde, Bugogo na Ikonda.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi najiuliza fedha iliyotumika kwa kufanya utafiti ule inarudishwa vipi kwa sababu maji hayajapatikana? Kama maji hayajapatikana Serikali mnawaambia nini Wananchi hawa ambao mpaka sasa wana shida kubwa sana ya maji? Maji hayajapatikana na aliyefanya utafiti mmemlipa. Sijui, labda kuna ubia na hawa waanokuja kufanya utafiti wa haya maji! Mimi naomba nielezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende juu ya upungufu wa Watumishi katika Halmashuri zetu. Halmashauri karibu zote ambazo Kamati yetu imezizungukia zina upungufu mkubwa wa Wakuu wa Idara na Vitengo. Kila Halmashauri ukienda unakuta Makaimu, sasa najiuliza hivi mtu anayekaimu kwa miaka mitano, miaka sita, miaka mitatu, anafanyaje kazi yake kwa ufanisi?

Halmashauri zingine unafika unakuta Mtumishi ambaye ameharibu amehamishwa kapelekwa Halmashauri nyingine halafu pale anabakia Kaimu. Yule anayekaimu naye sielewi kama anaweza akafanya kazi yake kwa usahihi kwa sababu kwanza anakuta pameshaharibiwa sasa na ye ye sijui aendeleee kuharibu au sijui afanye nini?

Bado hawa Makaimu wamekuwa wanakaimu kwa muda mrefu na Halmashauri zimekuwa zikiomba hawa Wakuu wa Idara hazipewi. Nitoe mfano tu, Mheshimiwa Spika, utaniwia radhi napenda kutoa mfano wa Halmashauri ninayotoka kwa sababu ninaifahamu vizuri. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, *DMO* hatuna, Afisa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]

Kilimo hatuna, Mhandisi wa Maji hatuna, Afisa Mifugo hatuna, Kitengo cha Uchaguzi ambacho ndiyo jicho la Halmashauri hatuna, Mwanasheria hatuna; sasa mimi najiuliza hivi Halmashauri inakuwaje haina Watumishi wote hawa halafu tunasema tuna Wizara pale ya TAMISEMI; TAMISEMI hamyaoni haya?

Mheshimiwa Spika, hili linanisikitisha sana na ukiangalia katika Halmashauri zetu zote, Halmashauri yoyote ambayo imapelekwa Mahakamani siku zote inashindwa kesi. Sasa mimi najiuliza hawa Wanasheria tulionao huko wanafanya kazi gani kama kesi hizi haziwi mionganoni mwa kesi ambazo zinatengezwa halafu ikifika pale Serikali inashindwa? Ninajiuliza kwa Halmashauri ambayo haina Mwanasheria, kwa sababu ninavyotambua Mikataba yote ya Halmashauri lazima isainiwe Mwanasheria akiwepo pale. Sasa Halmashauri ambazo hazina Wanasheria wanafanya kitu gani?

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa kwa TAMISEMI, kwa sababu tumelikuta katika Halmashauri nyingi na niombe tu walitafutie ufumbuzi kuliko kukaa tunaweka kila Idara Kaimu; watakaimu mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Miradi iliyopo katika Halmashauri zetu. Inasikitisha sana, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajitahidi inatoa fedha nyingi. Lakini fedha hii inapofika kule, watu wanaoitwa Wahandisi sielewi wanafanya kazi gani! Tumekwenda Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe tumekuta zahanati imejengwa pale, zahanati ile huelewi kama ni ukumbi wa mikutano, huelewi kama ni godauni, zahanati ile hajjamaliza hata miaka mitano imepasuka nyufa kuta zote, sakafu imepasuka, Halmashauri ile ukiuliza Mhandisi unaambiwa yupo. Sasa mimi najiuliza hii zahanati ilipojengwa Mhandisi alikuwa wapi?

Halmashauri ile ile ya Korogwe tumekwenda kwenye shule moja tumekuta madarasa matatu hayajamaliza hata miaka mitatu jengo lile halifai na sasa hivi limefungwa wanafunzi hawaingii, mle kwa sababu jengo lote lina nyufa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]

na halifai tena kwa matumizi. Sasa sijui TAMISEMI huku juu mnafanya nini kama yote hayo yanafanyika halafu mtu anayeitwa Mhandisi yupo kule anafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, pale pale Halmashauri ya Korogwe tumekuta choo ambacho wanafunzi wanatumia hakifai. Kamati ilfikia pahala tukasema labda tuchukue jukumu la kukibomoa ili kisitumike. Sasa sijui, nakosa majibu lakini naomba Waziri atujibu nadhani anaelewa vizuri haya tunayoyangea kwa Wahandisi kama hao wanawachukulia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, suala hili la Miradi hii mibovu halipo Korogwe peke yake. Tumekwenda Halmashauri ya Nzega sijui, nadhani waliposikia Kamati inakwenda katika Miradi ile tumefika katika shule moja, jengo ambalo limeanza kutumika toka mwaka jana mwezi wa kumi tutakuta kule ndani mafundi wanabomoa, yaani ni kazi ambayo ilikuwa inaanza siku ile ile baada ya kuonekana Kamati tunakwenda pale. Katika kuanza kuwahoji wanaobomoa wanasesma sisi hatuelewi, tumepegiwa simu asubuhi tumeambiya tubomoe hii sakafu. Ina maana kuna jambo lilikuwa limejificha pale ndani ambalo hawakutaka Kamati ilione. Sasa Muhandisi alikuwa wapi wakati yale yote yanafanyika? Fedha inayotumika pale tena kubomoa inatoka wapi kwa sababu tuliuliza tukaambia aliyefanya kazi ile alishalipwa fedha yote; sasa ni fedha ipi inayorudi kwenda kufanya kazi pale?

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri hiyo ya Nzega tumekwenda kutembelea Miradi mmoja wa Soko. Tumefika pale tukakuta siku hiyo hiyo soko lile sakafu yake yote inabomolewa mle ndani. Tukaanza kujiuliza kuna nini siku zote hawakuona kuna matatizo wamesikia leo Kamati inakuja ndio wakaanza kufanya marekebisho? Hili linaitesa Serikali ya Mapinduzi na nimwambie Mheshimiwa Waziri asipoyatazama haya, Wahandisi hawa katika Miradi ya Serikali wanatupeleka pabaya.

Nitoe ushauri katika Miradi hii. Sijui niseme ni

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]*

mwongozo ambao mmeutoa TAMISEMI, kwa maana ya kwamba, Halmashauri sasa Kamati ya Fedha peke yake ndiyo itakwenda kukagua Miradi; sioni kama mpo sahihi. Kwa sababu Kamati ya Fedha peke yake kwenda kukagua Miradi ya Halmashauri nzima haiwezekani kwa Halmashauri ambayo ina vijiji 120, ina Kata 30, Kamati ya Fedha inapewa siku mbili kwenda kukagua ile Miradi hivi watatazama Mradi gani waache Mradi gani? Matokeo yake Mradi unakuja kuonekana ni mbovu, mtu alishalipwa pesa, hakuna suluhu yoyote ya kufanya.

Mimi nakushauri Mheshimiwa Waziri hebu rudisheni ule utaratibu wa mwanzo, Kamati zote za Kudumu ziende zikakague Miradi ya Halmashauri, kwa sababu watakuwa na uwezo wa kuipitia Miradi yote iliyopo pale Halmashauri. Kwa utaratibu wa Kamati ya Fedha peke kukagua Miradi, hakuna tutakachokifanya, daima tutaendelea kupokea Miradi mibovu. Kwa hiyo, naomba sana Kamati zote za Kudumu za Halmashauri zirudishiwe mamlaka iliyokuwa nayo zamani ya kwenda kukagua Miradi iliyopo katika Halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Mfuko wa Akina Mama na Vijana. Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilitengeneza utaratibu mzuri kabisa. Utaratibu huu katika kuwa kwangu ndani ya Kamati hii, naomba nipongeze Halmashauri ya Hai, ndiyo Halmashauri pekee ambayo nimeona imepeleka pesa zake kwa kiwango kinachotakiwa. Halmashauri zingine zote, Halmashauri inadaiwa milioni 500 mpaka milioni 700 za Wanawake na Vijana. Sasa mimi najiuliza; suala hili lipo kisheria siyo hisani kwamba ni lazima Halmashauri inapokusanya mapato yake ya ndani asilimia tano ipeleke kwa Vijana na asilimia tano ipeleke kwa Akina Mama.

Sasa hivi asilimia kumi mfano Halmashauri ambayo inakusanya mapato kidogo labda milioni 700, ikitoa asilimia ile kumi ikapeleka tano kwa Vijana na tano kwa Wanawake; hivi tutakuwa na vijana wanaozurura mitaani mbona tuna fedha ya kutosha kabisa? TAMISEMI hili

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]

mnalionaje ni sahihi? Hatutaweza kuwakosa vijana wanaozurura mitaani kwa sababu fedha ambayo wanatakiwa kuipata hawaipati na mimi niulize kwa nini Halmashauri zinatumia fedha hizi? Kwa nini fedha hizi hazipelekwi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mchungaji Natse. Nimesema Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae na Mheshimiwa Hamad Rashid ajiandae.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Kamati hizi mbili; Kamati ya Bajeti na Kamati *LAAC*. Nazipongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri na *nina-declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, mwenendo tunaokwenda nao katika Halmashauri zetu ambapo fedha nydingi za Serikali zinapelekwa hasa kwa ajili ya maendeleo siyo mzuri. Takwimu ambazo tumeziweka katika Taarifa hii zinasikitisha na tunapotaka kuzungumza juu ya Matokeo Makubwa Sasa ni ndoto. Hii imejidhihirisha moja kwa moja kwa kukosa mambo makuu matatu kwa Watumishi wetu na hata kwa Wananchi wetu wa Tanzania. Jambo la uaminifu, jambo la uwajibikaji na jambo la uwazi, halipo kwa Serikali yetu na hata kwa Wananchi wetu wa Tanzania.

Nasema hivi kwa sababu sasa kuna usemi ambaou unadhihirika kwamba, ukiwa Kiongozi ukipata nafasi ukatumika kwa uaminifu kwa miaka yako ambayo Bwana alikujalia, jamii inakuona wewe ni wa hovyo. Ukitumika hata kwa wakati mfupi ukatenda mambo ya ajabu ambayo hayapimiki, jamii inakuona wewe ni mwanaume kweli. (*Makofii*)

Kwa hiyo, haya ni mambo yanayosikitisha katika nchi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE]

yetu na ndiyo maana nadiriki kusema, kwa sababu baada ya kufanya huu utafiti kutembelea Halmashauri zetu, Watumishi wengi siyo waaminifu. Hoja ni ile ile, chukua chako mapema maana hujui kesho. Takwimu hizi ambazo tumeziainisha hapa, maduhuli yasiyowasilishwa na Mawakala katika ukusanyaji wa mapato kwa Halmashauri zetu bilioni 4.5, maana yake inanishawishi kuamini kwamba, kati ya Watendaji Wakuu na hao Mawakala, kuna mwingiliano unaoashiria kwamba wanakula pamoja na ndiyo maana maduhuli haya hayakusanywi, mapato ya Halmashauri hayapatikani. Maana yake Viongozi hawana uzalendo, hawana uchungu na Halmashauri zao.

Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri, tena tumezungumza sana na Wenyeviti wa Halmashauri, ninyi Halmashauri ni zenu, mmoja akadiriki kusema sasa mimi nitafanyeje! Alikuwa Mwenyekiti wa ajabu sana, Halmashauri yake anapaswa kuisimamia, maana yake *ancollude* na Watendaji ili wale fedha za Halmashauri. (*Makofi*)

Sasa ninajumlisha haya yote katika usemi mdogo sana; *we have a giant sleeping, a sleeping giant called TAMISEMI*. Tunataka tuipige kidogo ili iweze kuamka ifanye kazi sawasawa. Nilitamani sana Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI awe hapa asikie. Naona wadogo zake tu wapo hapa tena mmoja tu. Wadogo hawa, mwenye dhamana ya TAMISEMI yupo?

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kweli lazima tufike mahali tubadilike na kosa letu kubwa tulilonalo suala la uwajibikaji halipo; nani amfunge paka kengele?

Taarifa yetu imeonesha wazi. Kwa kuwa ukiwa mlaji mzuri, umekula *point X*, wakati unataka kushughulikiwa na wahusika unapelekwa *point B*. Hii inanishawishi kuamini kuwa huu ni mtandao wa ufsadi, mtandao wa wizi, kutoka TAMISEMI mkapa Hazina. Nitaeleza ya Hazina hapa. Hazina kuna kitu tumeeleza juu ya *Excess Vote*. Kule Tanga walipeleka bilioni mbili; unauliza Bunge limepitisha Bajeti

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE]

kifungu kwa kifungu hii *Excess Vote* inatoka wapi na ni nani ameidhinisha billioni mbili?

Sasa jibu ambalo naweza kushawishika kuliamini haraka hili linatoa mianya ya rushwa, ya wizi na ujisadi, hii *Excess Vote*. Naomba Mawaziri hapa mnisikilize sawa sawa; inawapa mianya toka Hazina, *technical know-who and know-how* kupeleka hizo fedha huko. Kwa nini hiyo fedha isiwe *budgeted* na ndiyo kazi ya Bunge, halafu unatoa *amount* kubwa ya fedha namna hiyo, milioni 500, billioni mbili, unapeleka Halmashauri fulani. Zingine zinateseka hata yale mafungu yaliyokuwa *budgeted* hawapati. Wengine wanapata *Excess Vote*, we are not serious Serikali, tunahitaji tubadilike kwa ajili ya nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumza juu ya masurufu yasiyorejeshwa. Jamani, kulikoni kuna nini masurufu yasirejeshwe; billioni 1.9. Watumishi, Watendaji, *DTs*, Mkurugenzi na wengine, Viongozi Wakuu wa Idara, kwa namna hii tusipobadilika haya Matokeo Makubwa Sasa hatuwezi kuyaona. Shida moja kubwa ndugu zangu Wabunge, kule kwenye Halmashauri zetu, sisi ni Madiwani pia, lakini tumehoji watu matatizo ni nini, wengine wamesema ni Sheria zetu. Sasa Waziri kama Sheria ni tatizo, mahali pake ni hapa uilete ili tuweze kuifanyia marekebisho kwa afya ya nchi hii. Haya hayatendeki na hakuna wa kumwajibisha mwagine, jaribuni sasa kutumia rungu. Serikali fukuza mtu mahali atakapoharibu. Mimi najiuliza kitu kimoja; kama siyo mtandao Mkurugenzi anatoka Mwanza kaharibu, tumeenda kule anakwenda kwenye Halmashauri nytingine anakuwa *promoted?* (*Makof!*)

Aibu kwa TAMISEMI. Tumeuliza TAMISEMI umekuwa mzigo wa matatizo katika Halmashauri zetu. Tunahitaji Serikali mui-overhaul TAMISEMI. Hatuwezi kwenda namna hii, hatuwezi kwa mwendo huu tukafanya mabadiliko makubwa nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Miradi hii ambayo kimsingi ingelisimamiwa vizuri, Watanzania wangeelewa kwamba,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE]

tume-move from point A to point B, ndani ya miaka mitano hakuna kitu hata kidogo; ni kwa sababu ya ulaji katika Halmashauri zetu. Hakuna usimamizi wa Miradi. *Chain* inaanzia Hazina Wizarani mpaka kule kwenye Halmashauri *chain* ipo. Kuna kitu tumekiuiliza na kukitafuta, *Exchequer Notification* hasa kwa Miradi ya Barabara TANROADS inasikitisha mno, *Road Fund* inasikitisha mno.

Fedha zimetoka Hazina, *RAS* amekuwa *notified* kwamba, Halmashauri ya Karatu na Halmashauri ya Bagamoyo imepata fedha hizo na Wakurugenzi wametakiwa wathibitishe mapokezi ya fedha hizo, lakini hakuna fedha. Sasa unauliza, mmoja akatuambia hizo walizi-track zikiwa safarini kwenda huko baada ya kuonekana kuna haja nydingine kubwa huko. Kwa hiyo, inaonesha kuna mtando toku Hazina, TAMISEMI mpaka Halmashauri. Tuokoke, tuongoke, tukitaka mabadiliko nchi hii na *the only solution* wahuksika wawajibishwe bila huruma. (*Makofii*)

Mradi mmoja wa Maji kule Karatu ambao kimsingi husaidia sana Wananchi wa Karatu kwa sababu wanahitaji maji, lakini ukiangalia *value for money* kwa Mradi ule hakuna kitu. Serikali tunadanganyana wenyewe kwa wenyewe, hatutaki kuelezana ukweli na kwa sababu ya kulindana lindana. Tufike mahali na hii nafikiri ndiyo tatizo kubwa kwamba Waziri ni Mbunge mwenzangu, kwa hiyo, Waziri atakaa hapa kama Serikali, kidogo atakaa kama Mbunge asimamie Serikali; ngumu sana. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tunahitaji tubadilike ili tuweze kuonesha tofauti kwa maendeleo ya nchi yetu. Tabia ya kuwa ofisini ukafanya mambo hovyo hovyo, halafu unalindwa kwa kisingizio kwamba huyu ndiyo anachapa kazi vizuri, naomba tuache. Kwa hiyo, Taarifa hii ya *LAAC* ambayo imetoka hapa, tutaomba Serikali ifanyie kazi mapendekezo na Bunge litoe kama azimio, yafanyiwe kazi kwa afya ya nchi yetu. Nitaomba sana Serikali ifanyie kazi, Bunge lako niliombe baadaye liweke maazimio na Serikali iyafanyie kazi pasipo ajizi. Ndugu yangu Mwaijage alisema fukuza andaa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE]

wengine, fukuza 50 andaa 50, gharama yake ni ndogo kuliko kukaa na hawa panya wanaokula. Tuthubutu na tufanye pasipo kuogopa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, nataka nianze kuchangia kwa upande wa Kamati ya Bajeti. Natoa pongezi kubwa kwa kuunda Kamati hii, ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania, kwa sababu kila kitu tunachokifanya lazima kinaenda kwa njia ya Bajeti. Ninataka nianze kwa kusema kwamba, mapato ya Taifa letu yanategemea Miradi mbalimbali ambayo tunayo na mapato haya yanatokana na makampuni ambayo yamewekeza katika nchi yetu.

Sasa nataka niishauri Serikali hasa kwenye Kamati hii ya Bajeti, inapotuletea bajeti hapa na sisi Wabunge tunapitisha, lazima tuangalie vizuri sana ile *source of income* inatoka wapi? Ukiangalia unaweza ukaona kuna Halmashauri nyingi sana zina wawekezaji, lakini bado hazijapata faida kubwa na wawekezaji. Ukienda kwa wawekezaji wanasema wenyewe wanalipa kodi kwenye *Basket Fund*. Kwa hiyo, unaweza ukaona zile Halmashauri husika hazipewi, kuna kitu kinaitwa *loyalties* au mrabaha. Sasa ule mrabaha kwa Halmashauri hautolewi. Kwa hiyo, unaweza ukaona Halmashauri nyingi sana zinashindwa kupata ile tunasema *own source income* kwa sababu haina vyanzo vyaa mapato.

Vyanzo vyaa mapato vingeweza vikatokea kwa makampuni kulipa huu mrabaha kwa Halmashauri ili iweze kutekeleza kazi zake za Halmashauri. Kwa mfano, unaweza ukaona Halmashauri ina makampuni mengi lakini ina

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

matatizo mengi. Unaweza kuona Halmashauri inakosa maji, inakosa zahanati zile zikawa zimeisha. Halmashauri inaweza ikakosa vitu vya msingi kabisa kwa mfano unaweza ukaona hata barabara vijijini bado hazipitiki.

Unaanza kujiuliza hata kwangu kule Jimbo la Mufindi Kusini wanasema tuna makampuni mengi sana. Katika makampuni mengi haya mbona hatuoni kama tuko tofauti na watu ambao hawana makampuni. Kumbe yale makampuni yanatoa kodi ambayo inakusanya na *TRA*, inaenda kwenye *Basket Fund*, ambayo inagawiwa kwa nchi nzima. Hiyo ni sahihi kabisa wala hakuna utata wowote. Bado kuna hela ile ambayo tunasema mrabaha ambayo inabidi itolewe kwa Halmashauri, hiyo hela bado haitolewi.

Sasa naiomba Serikali kuwepo na Sheria, makampuni wafuate sheria kwamba lazima fungu fulani litolewe kwa Halmashauri ili liweze kusaidia maendeleo ndani ya Halmashauri yake. Hilo nimeona ni la msingi sana niliongelee kwa sababu makampuni mengi tukiyafuata kuomba msaada yasadie wanasema wanalipa kodi kwenye Serikali Kuu. Sasa wakilipa kodi kwenye Serikali Kuu sisi bado watu wetu wanabaki kuwa maskini wakati kuna makampuni makubwa.

Suala la pili kwenye makusanyo haya ya kodi, matumizi ya fedha yanafuata makusanyo. Serikali isipokusanya kwa makini, ikakusanya labda bila kufuata Sheria hata matumizi yake hayatafuata Sheria. Sasa ukiangalia hata ulipaji wa kodi, Serikali inajikita sana kupata kwa walipaji wa kodi wadogo wadogo hawa, lakini bado haijajikita kuhakikisha makampuni makubwa ambayo tunayo, yanaweza yakakusanya kodi ya kutosha. Wananchi ili wajue kweli makampuni makubwa yanakusanya kodi kama inavyotakiwa; kwa mfano, kuna kitu kinaitwa *Financial Report Analysis*, zile *Financial Report* za Makampuni zingekuwa zinaoneshwa hata kwenye mitandao kama nchi nyingine.

Nchi nyingine Ripoti za Fedha zinasomwa tu, mtu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

yeoyote anaweza akasoma Ripoti ya Fedha kufuatana na uzalishaji, lakini sisi makampuni yetu bado yanaficha *Financial Report Analysis*, kwa hiyo, hatuelewi makampuni yanalipa kiasi gani kwa Serikali. Kuna Makampuni mengine hayalipi kabisa, yanaweza yakawa yanalipa *percent* ndogo sana, kwa hiyo, inatuletea kutokukusanya kodi vizuri. Sasa naishi Serikali kwamba, wawekezaji kwanza lazima watuneshe *Financial Analysis* wanayoipata kwa kila mwaka tuwe tunaiona ili tuje wanachangia shilingi ngapi kwa kodi.

Suala lingine, nakuja kwenye kipengele cha Miradi ambayo tunaiendesha katika Halmashauri yetu. Kuna tatizo kubwa linajitokeza, Miradi inakuwepo na imekuwa *budgeted* tayari, lakini fedha kutoka Serikali Kuu inachelewa; kuna tatizo gani? Ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikali Kuu, mpaka sasa Halmashauri yangu ya Mufindi hawajapata fedha ya maendeleo na sisi tunaenda na muda tunasema *time-frame* na sasa hivi tunasema *Big Results Now*, huwezi kusema *Big Results* wakati fedha unachelewesha. Hii *Big Results Now* nayo unaifuta kwa *design*. *Big Results Now* inaenda kwa mfumo wa kifedha kama mfumo wa kifedha ukienda vizuri na watendaji wetu kule wakapata fedha kwa muda unaotakiwa ndiyo tunaweza kutamka *Big Results Now*.

Hatuwezi kutamka hiyo kwa sababu fedha nyingi za maendeleo hazifikasi kule. Kwa mfano, sasa hivi hata Miradi ya Maji, juzi nimeuliza swali kwa Waziri wa Maji, tumesema hii Miradi bado imesimama kwa sababu fedha hajafika pale, lakini fedha zikifika kwa muda unaotakiwa na Miradi itaisha kwa muda unaotakiwa. Wabunge hatuwezi kuuliza maswali, utauliza swali gani kama Mradi wa Maji umeshatekelezwa tayari Wananchi wanapata kule maji? Utauliza swali gani kama Kituo cha Afya kimeshapewa *ambulance* tayari? Utauliza swali gani kama Wananchi wako kule wameshafurahia na barabara za vijijini zimeshajengwa?

Tunauliza kwa sababu fedha hajapelekwa pale na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

sasa hivi Wabunge wengi hata tukifanya mkutano utafanyaje mkutano wakati uliahidi vitu vingi kwa Wananchi lakini Serikali haitekelezi. Tunasema *Big Results Now*, itakuwaje *Big Results Now*, kama tunataka tuseme *Big Results Now* tuwe kitu kimoja, fedha zipelekwe kwa wakati, hii itatusaidia sana hii.

Kitu kingine, lazima tusimamie vizuri hapa Wabunge wengi wanalamika wanasema matumizi ya fedha, hiyo tunasema nidhamu ya fedha. Kwa mfano, mfanyakazi wa benki anamiliki hela nyingi sana lakini hutasi kia siku moja anasema *vocha* ya mteja haipo. Hiyo tunasema *missing document*, sasa sisi kwenye ukaguzi unaenda kukagua Miradi wanasema *document* haipo. Mtu amefanya malipo, amemlipa mteja tayari halafu anasema hiyo *document* haipo. Mimi hii *missing document* huwa sii lewi kwenye kichwa changu.

Unaweza kuona Mradi wa bilioni mbili, bilioni moja, unasema *missing document* haipo. Huu ni uhasibu wala siyo uhasibu sijui ni kitu gani kunyanga'nya hela, yaani sawa sawa na mtu anakunyanga'nya hela halafu anasema hawakutoa risiti lakini ameshachukua hela. Sasa naiomba Serikali, itengeneze mfumo mzuri; kwa mfano, sasa hivi tuna mfumo huu wa *EPICAR*, ambayo ni *system* nzuri ya ku-control malipo. Huu ni mfumo mzuri sana, lakini bado tuna-lack wataalam pale, wataalam bado hawaja-control. Wenzetu nchi za Ulaya kule kwanza hawajasikia hata siku moja mtu anatoa *Financial Report* au *Narrative Reports* ya pesa, ukasema *document* moja alinipa lakini ushahidi wa *document* ambayo amenipa haupo. Hii hajawahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, kuna Miradi mikubwa unaenda kukagua wanasema kwamba, Mradi umefanyika lakini *Bill of Quantity* haipo ile BoQ. Hivi unaweza kutekeleza Mradi mikubwa hakuna *document* ambayo ina-support Mradi! Mbona hiki kitu naona kama ni kipywa sana. Ndiyo maana Wabunge wengi wanachangia wanasema labda TAMISEMI. Siyo kwamba TAMISEMI wanafanya utofauti labda kuna tatizo la *supervision* katika miradi. *Supervision*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

ikisimama vizuri katika Miradi ya Halmashauri na ile Miradi ya Halmashauri tunajua kabisa inakabidhiwa Halmashauri na kule Halmashauri kuna Madiwani ambao wanasmamia vizuri sana, bahati nzuri na sisi Wabunge ni Wajumbe katika *Council*, hata Kamati ya Fedha ya Halmashauri ni Wajumbe pale.

Tukisaidiana kwa pamoja kutoka TAMISEMI na sisi Wabunge na Madiwani, tukikaa pamoja hauwezi kutokea wizi katika Halmashauri hata siku moja. Madiwani *waki-raise issue* wakasema kuna kitu kimetokea Halmashauri kuna ubadhirifu, lakini upande wa Serikali ukakaa kimya, hapo tayari ni *gap* na tayari ni tatizo.

Sasa naomba Serikali iwasikilize Madiwani, Madiwani wakisema kuna kitu kimetokea lazima wawasikilize halafu wachukue hatua. Kwa Mfano, *CAG* amekagua, sisi wa Kamati ya Fedha tunaenda kukagua, wanabaini pale kwamba, kuna ubadhirifu wa fedha na kwenye Ripoti ya *CAG* ametoa *opinion* yake kwamba, ubadhirifu huu umetokana na moja, mbili, tatu. Sasa ile hoja inapelekwa kwa Serikali, Serikali inakaa kimya. Ikkiaa kimya zile fedha hatuwezi kuona zimeenda wapi, Miradi ya Wananchi kule inasimama halafu huku tunasema *Big Results Now*, hii mbona inachanganya watu vichwa! Hatuwezi kutamka hivyo na ni lazima tufuate maoni ya *CAG*, *CAG* anaisaidia Serikali kubana vizuri matumizi mazuri ya Serikali. Sasa kama Ripoti ya *CAG* ambayo imekaguliwa na Wataalamu ikapelekwa na Kamati ya Fedha ambayo ni *LAAC* au *PAC* waka-recommend wakabaini *transactions* hazijaenda kisahihi, Serikali ikaletewa halafu nayo ikasema hapa labda tungepeleka Polisi, hapa nani atapeleka Polisi au atapeleka Mahakamani.

Sasa hiyo *statement* inabaki ina-hang, kila mwaka utakuta hoja haifungwi, kuna hoja nyingine tunakagua za mwaka 1998 huko, kila mwaka tunasema hii hoja haifungwi. Wengine wanasema ufute, unaweza kufuta hoja ya bilioni mbili utaifutaje? Huwezi kufuta. Kisheria, Kiutaalamu wa Fedha wanasema fedha huwezi ukafuta ukasema hii fedha

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

imepotea tu. Tunasema kama mtu amefilisi labda Kampuni ilikopa halafu ikafilisika huwa tunauza mali zao.

Halmashauri ikitumia vibaya utauza mali ya Halmashauri ili warudishe; hapana, inabidi Serikali itengeneze kitu cha kuchukua hatua kwa fedha ambazo zimetumika bila kuonesha *supporting documents* zake. Lazima Serikali ioneshe kuchukua, lakini kama tutakuwa tunakagua halafu hakuna hatua inayochukuliwa, basi tunakagua lakini hakuna kitu kinachotendeka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, hoja za Wabunge ambazo zinakuja hasa zinazolenga masuala ya fedha, fedha ambayo ni kodi ya Wananchi, lazima isimamiwe vizuri na Serikali iweze kuangalia vizuri ili twende na usemi wetu vizuri wa kusema *Big Results Now*. Kuna Mbunge mmoja hapa anasema kuna pikipiki inanunuliwa kwa milioni kumi na mbili; kama kuna ushahidi wa kutosha pikipiki hiyo imenunuliwa kwa milioni kumi na mbili kumbe inawezekana kuna vitu vingi vimejificha. Hebu tuanze na hatua hiyo tuoneshe tumeanza na hatua ya kukomesha, kwa kukomesha hao watu wanaotuharibia.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine tunasema kwamba, kuna uhamishaji wa Wakurugenzi, kwa mfano, akifanya vibaya anahamishiwa sehemu nyingine. Hili ni tatizo tayari, kama mtu anafanya vibaya abaki pale aweze kujibu hoja vizuri. Masuala ya hesabu mtu anaweza kuwa hajaiba lakini amekosea kimahesabu, *records* amekosea, lakini kama umeshamhamisha atashindwa kujibu zile hoja vizuri.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wasipohamishwa na sisi kama tunaenda kukagua pale tunawakuta, wanaweza kutupatia maelezo ambayo yanajitosheleza. Yakishajitosheleza yale maelezo tukipeleka Ripoti kwa Wananchi wanakuwa na imani, lakini kama maelezo hayapo basi hilo ndiyo tatizo linalojitokeza kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nimeona hilo niliongee vizuri kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

sababu bado nidhamu ya fedha katika Halmashauri zetu hazijakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa fedha tunajua kabisa wataalamu wa fedha kuanzia Wakurugenzi lazima wawe *professional*, siyo mtu ambaye hajasomea masuala ya fedha unampa Ukurugenzi. Hii ni hatari sana, kwa sababu yeye hajui ku-*control* fedha. Wataalamu wale wadogo wa chini wanakuwa wanajua *accounting system* vizuri sana, lakini wewe unaenda kuidhinisha malipo hujui zile *accounting system*, lazima watakuzunguka hawa wadogo, wakikuzunguka wewe unaidhinisha kitu ambacho hukijui, hilo linakuwa ni tatizo.

Kwa hiyo, nataka niishauri katika Serikali inapoajili Wakurugenzi lazima waangalie wale ambao wana *basic* ya *accounting system*. Hauwezi kuwa na Mkurugenzi ambaye hana *basic accounting system*. Mimi nashukuru pale Wilaya yangu ya Mfindi, Mkurugenzi waliyemleta pale ni *professional*, yeye ni *accountant*. Kwa hiyo, *issue* ikitokea sisi tuna haja ya kumhoji vizuri kwa sababu ni mtaalamu. Wewe sawasawa na Daktari, unampeleka mtu ambaye hajasomea Udaktari halafu unasema atibu atatibuje! Hata akikosea anaweza kujitetea umeniweka tu mimi siyo mtaalamu, ndicho kinachotokea kwenye fedha, kwenye fedha huwezi kumshitaki mtu aliyeiba kumbe yeye siyo mhasibu, anasema mimi siyo mhasibu utachukua Sheria gani?

Sasa Wakurugenzi lazima wawe na *profession* ya uhasibu ili fedha ikiibiwa tuwabane vizuri. Halafu vilevile Mkurugenzi ni Mshauri wa Serikali, Mkurugenzi ndio anaengalia Bajeti ambayo inapitishwa na Halmashauri. Sasa kama hajasomea hizi hesabu atapitishaje zile Bajeti za Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, bajeti lazima zianzie Halmashauri, sasa katika kuanzia Halmashauri bajeti yetu unaweza ukaona hata Mifuko ya Afya, Mifuko ya Maji ambayo ni kitu muhimu sana kwa jamii, tunaweka *dash* tunasema afya

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MENDRAD L. KIGOLA]

tunategemea wafadhili, sijui maji tunategema wafadhili!  
Sasa haya ni maeneo muhimu sana inabidi kwenye *own resource* ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** Mheshimiwa Spika,  
naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hamad Rashid  
Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika,  
nakushukuru. Nami niungane na wenzangu kuwapongeza  
sana Wenyeviti wa Kamati ya Bajeti na nina-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na  
Kamati ya LAAC, kwa Taarifa nzuri zilizowasilishwa. Naunga  
mkono hoja zote mbili.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa, nitazungumzia  
zaidi kwenye Kamati ya Bajeti kwa sababu Kamati ya LAAC  
imezungumzwa sana. Niseme tu kwamba, baada ya Serikali  
kuleta Muswada wa Fedha Bungeni na baadaye Bunge  
kuridhia, huo Muswada wa Sheria unatakiwa usimamie  
kutekelezwa. Katika bajeti ya mwaka huu tumepitisha  
hana Muswada wa Sheria ya kutoza kodi, inasikitisha sana  
Serikali imegwaya katika kusimamia makusanyo ya kodi.  
Matokeo yake ndiyo imeanza vikao na vikao, jambo  
ambalo lilikuwa lifanyike kabla Miswada yenyeWE haijaletwa  
ndani ya Bunge. Matokeo yake inakuja wanassema Kamati  
za Bunge zimependekeza hivyo.

Kwa mujibu wa Katiba ni Serikali peke yake na Rais  
peke yake ndiyo mwenye mamlaka ya kuongeza au  
kupunguza matumizi ya Serikali au kodi ya Serikali. Kwa hiyo,  
mapendekezo tunayoyatoa ndani ya Bunge tukaikabidhi  
Serikali, wakipitisha ni ya Serikali siyo ya Wabunge tena, kazi  
yetu Wabunge ni kusimamia utekelezaji wake.  
Mnaposuasua Serikali katika kusimamia mapato, hilo ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

tatizo la msingi, ndiyo maana *enforcement of law* katika nchi yetu imekuwa *very week*, tuna-negotiate baada ya Sheria kuitishwa *it is wrong*. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nidhamu ya bajeti. Nakushukuru sana kwa kuanzisha Kamati ya Bajeti, ni muda mfupi imefanya kazi, haina utaalamu, haina wataalamu, lakini tumeweza kugundua mambo mengi ambayo moja ni kwamba, *discipline* ya bajeti katika Serikali hakuna ni *zero*. Leo ni *quarter* ya kwanza ya bajeti, katika mfumo wa bajeti tuliounda sasa hivi tulitegemea Hazina watakuwa angalau wameshaanza zile *seven hundred million dollars* walizokuwa wazipate hawajatafuta hata senti moja.

Pesa zilizopatikana za bajeti ya mwaka jana ni bilioni mia moja na kumi na nane, za mwaka huu hata senti tano. Kwa hiyo, Miradi ya Maendeleo hajapata hela, halafu unategemea Serikali na Wananchi wanasesma, aah basi sitaki kutumia lile neno baya la Mheshimiwa Beatrice Shellukindo; *Better Resign Now*. Siyo *Better Results Now* ni *Better Resign Now*. Huwezi *quarter* nzima hujakusanya hela za maendeleo halafu useme utakuwa na *Better Results Now* utazitolea wapi? Matokeo yake imekuwa inafanya *reallocation*, Mafungu mengine yanakosa fedha na hatimaye matumizi mengine makubwa yanatokea. Hilo la pili nalionna linatokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, kukosekana kwa nidhamu ya matumizi, kumepelekea hata matumizi yanayofanyika, nina hakika uhakiki wake haupo. Sasa hivi kwa mfano, ukichukua safari tu, zimeshatumika bilioni 30 katika bilioni kumi na tano za bajeti ya mwaka mzima. Safari moja *in-a-range between billion* mbili na nusu hadi tatu, safari moja ya wiki moja. Sasa unasema hawa watu wako *serious?* Kweli tunataka mabadiliko haraka. *Discipline* ya bajeti hakuna, mimi nakushukuru sana umeunda Kamati ya Bajeti sasa tufanyeje.

Tumeomba *Budget Act*, kwa utaratibu wa Serikali tutachukua miaka kumi haiji. Naomba ofisi yako na sisi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

Kamati tutengeneze *Budget Act* wenyewe, tuilete Bungeni tuijishe hapa. Tisisubiri Serikali haitafanya na wenzetu wengine tuliokwenda kujifunza wengi wametunga *Budget Act* wenyewe hawakuingoja Serikali. Hilo naomba sana tulifanye na tukilifanya hilo sasa, maana yake Bunge litakuwa na *power* ya kusema hapa fedha hazikutumika vizuri na tunachukua hatua sisi wenyewe kwa kutumia bajeti yetu ya Kamati. (*Makofi*)

Haya mambo ya kulalamika lalamika huku hayana maana yoyote, tutaendelea kulalamika, Serikali italalamika na wengine watalalamika. Sasa Bunge lazima litumie madaraka yake ya Kibunge, lichukue hatua kwa watu wote ambaao hawatimizi masharti ya fedha ambazo zimepitishwa na Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la nne, suala la Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti. Naelewa na mimi bahati nzuri ni Kamishna wa Bunge, hatujapata ule Mfuko wetu wa Bunge hasa kuudhibiti wenyewe vizuri. Tunahitaji tuudhibiti ule Mfuko sasa ili tuwe na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti, lakini tuwe na Sekretarieti nzuri za Kamati zetu zote za Kudumu na Wabunge wawe na *freedom* ya kwenda kutembelea Miradi na kukagua kwa kutumia Kamati zao za Kiseka, hatutakuja hapa kulalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa utaratibu huu tunaoenda nao tutalalamika tu, kwa sababu Kamati hazina muda wa kutosha wa kufanya kazi, hakuna fedha za kutosha na hazina wataalamu wa kutosha. Vilevile meno tunayo, unajua Kanuni yetu inaturuhusu hata kumfichia Rais; meno gani unataka zaidi ya hayo? Tuna meno makali tu, lakini ni vizuri taratibu ya kuyatumia vizuri tuyatumie. Hilo lipo nitatizo la mzingi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine kubwa sana, tumegungua katika Kamati ya Bajeti, siyo tu kwamba fedha hazitoshi, fedha zinatosha. *One third* ya bajeti tunayopitisha hapa inaenda mifukoni na bahati nzuri hili hata Mheshimiwa Rais alilisema. Matatizo yalilopo ni mawili; moja, hili la ufisadi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

na pili, *absorption capacity* iliyoko kule ni ndogo sana. Unapeleka fedha kwenye Halmashauri, Watendaji walio kwenye Halmashauri hawana uwezo wa kuzitumia hizo fedha.

Leo Wizara ya Maji ina fedha, lakini wakandarasi wa kutengeneza Miradi ya Maji hawapo wa kutosha. Wizara ya Kilimo ina fedha za kutosha, makandarasi wa kutengeneza mifereji ya *irrigation* hawapo; ndiyo Waziri alivyotuambia. Lipo tatizo, tunahitaji kukaa kitako katika Kamati za Kisekta namna gani tunakabili matatizo haya ili fedha zinazotolewa zitumike kwa wakati na ziweze kutumika kwa maana ya *value for money*. Hili ni tatizo moja kubwa liliopo, kwa hiyo, bajeti tuliyonayo wala siyo ndogo hata kidogo. Usimamizi wa fedha ndiyo tatizo la msingi.

Mheshimiwa Spika, la tano, naishukuru sana Kamati yako ya Bajeti. Wizara ya fedha iwe wabunifu, inaendelea mpaka leo kuelemea kwenye Mashirika ya kawaida ya kukopesha, *interest rate* kubwa na kadhalika, wakati kuna *holding companies* nyingi sasa hivi zinatoa mikopo mikubwa na hasa baada ya Soko la Ulaya kuanguka, watu wanakuja Afrika sasa kuwekeza kwa wingi sana. Nenda upate maamuzi katika hilo jambo, *is a nightmare*. Badilikeni Wizara ya Fedha kule ndani. Badilikeni kabisa, ulimwengu wa leo ni ulimwengu wa kuwahi. (*Makofii*)

Tumekwenda Kuwait juzi, wenzetu waliokuja na Miradi mikononi wameondoka na hela. Sisi tumeondoka na kurudi mikono mitupu; ni kuwahi tu, kujipanga vizuri tu. *Delegation* inakwenda hata kuandaliwa haikuandaliwa, hatuwezi kwenda namna hiyo. Mchezo mdogo mdogo, *we are not serious*. Naomba tubadilike kabisa. Nami nasema Bunge hili lina mamlaka ya kuvisimamia Serikali sawa sawa, tutumie wajibu wetu tuisimamie Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja zote. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitaomba mniruhusu *just* kwa sababu ya kutoa tahadhari tu, tutumie Kifungu cha 28(5) ili nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atoe hoja ya kutengua kifungu kinachohusika kwamba, tufanye kazi Siku ya Jumamosi. Kama mlivyoona, Bunge letu ni fupi safari hii, kwa maana ya kwamba, tuna kazi nyingi za Kamati, lakini inabidi tumalize tarehe 20 kwa sababu maandalizi ya Ukumbi huu kwa ajili ya Bunge la Katiba yanatakiwa yaanze sasa hivi.

Mnaona hata Katibu wa Bunge hayupo, wanajaribu kwenda kupata vyombo vingine ambavyo vinapasa kuhudumia Ukumbi huu kama Bunge la Katiba. Kwa hiyo, hatuna budi kufanya kazi Siku ya Jumamosi, kesho.

Lingine, nilikuwa nashangaa kumbe ninyi *Budget Act* mlitegemea Serikali ndiyo itatengeneza, mimi nilifikiri Kamati yenyewe tutapendekeza Bungeni. *Budget Act* ni ya Bunge siyo ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hoja ya kutengua Kanuni za Bunge!

#### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, chini ya Kifungu cha Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu ya Mwaka 2013, naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni hiyo kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge wa kushughulikia Taarifa za Mwaka za Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa kumalizika tarehe 20 Desemba;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]*

NA KWA KUWA ratiba ya shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Nne zimepangwa kwa kuzingatia Kalenda ya Mikutano ya Bunge;

NA KWA KUWA Ratiba hii inaonesha kuwa majadiliano ya Taarifa za Kamati za Bunge yataendelea kesho Siku ya Jumamosi;

NA KWA KUWA kwa Mujibu wa Kanuni ya 28(1)(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, Bunge haliwezi kukutana na kufanya kazi Siku ya Jumamosi na Jumapili au Siku za Mapumziko;

NA KWA KUWA ili kuwezesha Bunge kuweza kukutana Siku ya Jumamosi tarehe 7 mwezi Desemba ni lazima Bunge litengue Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1);

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Nne, Kanuni ya 28(15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge halikutana Siku ya Jumamosi, Jumapili na Siku za Mapumziko itenguliwe na badala yake Bunge likutane Siku ya Jumamosi, yaani kesho, tarehe 7 Desemba, 2013 kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa saba mchana. Isipokuwa kwamba, siku hiyo hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza, inabidi tutumie muda wetu vizuri zaidi na kama mtaona ile Ratiba ya Kamati, tukianza Kamati za Kisekta, hatuna budi itakuwa Kamati mbili kwa siku moja. Kwa hiyo, unakuta nayo pia ni kubanana sana, lakini hatuna namna. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, nawahoji muamue hoja iliyotolewa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni za Bunge iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kesho tutakutana saa tatu. Kwa kuwa sina matangazo mengine, naomba kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.43 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,  
Tarehe 7 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*